TANZANIA FOOTBALL FEDERATION
SHIRIKISHO LA MPIRA WA MIGUU TANZANIA

# KANUNI

## Ligi Kuu

Toleo la 2026


KISHO LA MI
MIGUU TANZA

## UTANGULIZI

Kanuni hizi za Ligi Kuu ndio mwongozo wa Uendeshaji na Uchezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo Klabu za Ligi Kuu kwa kuwepo kwake katika Ligi Kuu zinawajibika na kulazimika kufuata, kuheshimu na kutii Kanuni hizi.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania huzifanyia Marekebisho Kanuni za Ligi Kuu ili kuziboresha na kuendana na wakati. Mabadiliko ambayo lengo ni kuwa na Ligi iliyo bora zaidi, ambayo italeta Ushindani kwa Timu shiriki na pia kutoa Burudani zaidi kwa Watazamaji, pamoja na kuchochea wadhamini zaidi kujitokeza kwa ajili ya Kudhamini Ligi na Timu shiriki.

Ligi iliyo Bora itawezesha kupata Wachezaji Bora watakaounda timu Bora za Taifa zitakazoweza kufanya vizuri katika Mashindano ya Kimataifa na pia kupata Klabu zitakazowakilisha vema Tanzania katika Mashindano ya Kimataifa kwa ngazi ya Klabu. Mafanikio haya yataweza kukuza na kuendeleza kiwango cha Mpira wa Miguu katika nchi yetu na pia kuijengea heshima Tanzania katika Ulimwengu wa Mpira wa Miguu.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania linafahamu na linaamini kuwa Mpira wa Miguu ni Mchezo wenye nguvu, Unaopendwa na watu wengi Duniani na Unaoweza kuvutia watu kutoka sekta mbalimbali kuwekeza iwapo Kanuni, Taratibu na Sheria za mchezo huu zitafuatwa na kuheshimiwa na pia Kanuni za Uchezaji wa Kiungwana (Fair Play) zitazingatiwa na Wachezaji, Makocha, Waamuzi, Viongozi, Washabiki na wengine wote ambao kwa njia mojawapo wanahusika na mchezo wa Mpira wa Miguu.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania linaagiza Klabu, Makocha na Waamuzi kuzisoma kwa makini Kanuni hizi na kuhakikisha zinaeleweka na kufuatwa kwa faida ya Ligi Kuu na Mchezo wa Mpira wa Miguu. Shirikisho linapenda kuwakumbusha watu wote kuwa Mchezo wa Mpira wa Miguu unalindwa na Sheria, Kanuni na Taratibu. Bila Sheria na Kanuni, Mpira wa Miguu utakuwa Vurugu tupu. Shirikisho la Mpira wa Miguu linaziomba Klabu kuhakikisha kuwa Kanuni hizi pia zinaeleweka vizuri kwa Wachezaji na washabiki wake kwa lengo la kusaidia kuwafanya wafahamu Kanuni na Taratibu za Mpira wa Miguu vizuri zaidi na kwa kuzifahamu Kanuni zaidi zitawafanya kuwa wachezaji Bora zaidi watakaojiepusha na kuadhibiwa kwa makosa yanayoweza kuepukika.

Kanuni na Sheria zimewekwa kwa ajili ya Kuufanya mchezo uwe na Ladha katika kuucheza na pia uwe na Ladha katika Kuutazama na hivyo kukamilisha Burudani na kupata Burudani zaidi. Tukitumia Nguvu, Ari na Misingi ya Mpira wa Miguu inavyotakiwa tutaweza kujenga jamii na Dunia Bora yenye Afya zaidi, Upendo, Amani, Furaha na Usawa.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania litahakikisha siku zote Ligi Kuu inakuwa na Heshima kwa kusimamia kwa Uadilifu Kanuni hizi za Ligi Kuu na Sheria za Mpira wa Miguu kwa kutoa Adhabu inapobidi, kuelimisha na kuhakikisha siku zote Mshindi anapatikana Uwanjani kwa Kufuata kanuni na Taratibu za Mchezo na siyo kwa Matumizi ya Njia chafu zisizokubalika. TFF Itahakikisha Matumizi sahihi ya Kanuni hizi kama yalivyokusudiwa.

**Michezo ni Burudani, Afya na Ajira**

# YALIYOMO


| SURA | KANUNI | Namba | Ukurasa |
|---|---|---|---|
| **SURA I Uchezaji wa Kiungwana** | Uchezaji wa Kiungwana | 1 | 1 |
| **SURA II Kuundwa, Matumizi na Tafsiri** | Kuundwa | 2 | 5 |
| | Matumizi na Tafsiri | 3 | 5 |
| | Tafsiri ya Kanuni | 4 | 6 |
| **SURA III Ligi** | Daraja la Ligi | 5 | 8 |
| | Mfumo wa Ligi | 6 | 8 |
| | Michezo ya Mchujo | 7 | 8 |
| | Mshindi | 8 | 9 |
| | Uwanja | 9 | 10 |
| | Ushiriki Mashindano ya Kimataifa na Mengineyo | 10 | 11 |
| | Vikombe na Tuzo | 11 | 12 |
| **SURA IV Utawala** | Usimamizi wa Ligi | 12 | 16 |
| | Uthibitisho wa Kushiriki | 13 | 17 |
| | Leseni ya Klabu | 14 | 17 |
| | Msimu na Ratiba | 15 | 17 |
| | Udhamini | 16 | 18 |
| **SURA V Mchezo** | Taratibu za Mchezo | 17 | 22 |
| | Michezo ya Kirafiki | 18 | 30 |
| | Ngao Ya Jamii | 19 | 31 |
| | Matumizi ya Teknolojia ya Video Support System (VS) | 20 | 33 |
| **SURA VI Tiba na Bima** | Huduma ya Kwanza | 21 | 36 |
| | Bima | 22 | 36 |
| **SURA VII Malalamiko na Rufaa** | Malalamiko | 23 | 38 |
| | Utaratibu wa Malalamiko | 24 | 38 |
| | Pingamizi katika Mchezo | 25 | 38 |
| | Rufaa | 26 | 39 |
| | Utaratibu wa Rufaa | 27 | 39 |
| | Vyombo vya Maamuzi | 28 | 40 |
| **SURA VIII Mapato na Gharama** | Mgawanyo wa Mapato | 29 | 43 |
| | Gharama za Mchezo | 30 | 43 |
| **SURA IX Yasiyotarajiwa** | Kujitoa | 31 | 46 |
| | Kutofika Uwanjani | 32 | 47 |
| | Kuvuruga Mchezo | 33 | 48 |
| | Kupanga Matokeo | 34 | 49 |
| | Kuahirisha Mchezo | 35 | 50 |
| **SURA X Usimamizi wa Mchezo** | Msimamizi wa Kituo | 36 | 52 |
| | Kamishna | 37 | 52 |
| | Mratibu wa Mchezo (GC) | 38 | 54 |
| | Mtathimini Waamuzi | 39 | 54 |
| | Waamuzi | 40 | 55 |

| SURA | KANUNI | Namba | Ukurasa |
|---|---|---|---|
| SURA XI | Udhibiti Kimashindano | 41 | 60 |
| Udhibiti na Adhabu | Udhibiti kwa Wachezaji | 42 | 62 |
| | Udhibiti kwa Waamuzi | 43 | 65 |
| | Udhibiti kwa Kamishna | 44 | 66 |
| | Udhibiti kwa Mtathimini Waamuzi | 45 | 68 |
| | Udhibiti kwa Makocha na Maofisa Wengine wa Ufundi | 46 | 69 |
| | Udhibiti kwa Viongozi | 47 | 70 |
| | Udhibiti kwa Klabu | 48 | 73 |
| | Udhibiti kwa Maofisa habari wa klabu | 49 | 77 |
| | Adhabu kwa Klabu | 50 | 78 |
| | Dawa Haramu | 51 | 79 |
| SURA XII Hadhi ya Wachezaji | Wachezaji wa Ridhaa na Kulipwa | 52 | 81 |
| | Kupata Upya Hadhi ya Ridhaa | 53 | 81 |
| | Kuacha Shughuli | 54 | 81 |
| | Wachezaji Wasiosajiliwa | 55 | 81 |
| | Kuachwa Huru | 56 | 81 |
| | Wachezaji Waliopandishwa | 57 | 82 |
| | Wachezaji Huru | 58 | 82 |
| | Wakala wa Mchezaji | 59 | 82 |
| SURA XIII | Wachezaji wa Kuhamishwa | 60 | 84 |
| Uhamisho wa Wachezaji | Uhamisho | 61 | 84 |
| | Uhamisho Zanzibar | 62 | 85 |
| | Uhamisho Nje | 63 | 86 |
| | Wachezaji wa Kigeni | 64 | 86 |
| | Hati ya Uhamisho Kimataifa | 65 | 87 |
| | Uhamisho kwa Mkopo | 66 | 87 |
| SURA XIV | Usajili | 67 | 90 |
| Usajili | Vipindi vya Usajili | 68 | 92 |
| | Pasi ya Mchezaji | 69 | 92 |
| | Majina na Idadi | 70 | 92 |
| | Maombi ya Usajili | 71 | 93 |
| | Pingamizi la Usajili | 72 | 94 |
| | Katazo | 73 | 94 |
| | Uthibitisho wa Usajili | 74 | 95 |
| | Kutengua Usajili | 75 | 95 |
| | Mikataba | 76 | 95 |
| | Vijana na Watoto | 77 | 97 |
| SURA XV | Viongozi wa Ufundi | 78 | 101 |
| Dawati la Ufundi | Makocha | 79 | 101 |
| | Daktari wa Timu | 80 | 102 |
| SURA XVI | Maamuzi Yasiyokatiwa Rufaa | 81 | 105 |
| Mamlaka | Ufafanuzi | 82 | 105 |
| | Marekebisho ya Kanuni | 83 | 105 |
| | Kufuta Kanuni | 84 | 105 |
| | Yasiyomo | 85 | 105 |
| | Azimio | 86 | 106 |

# SURA: I

## UCHEZAJI WA KIUNGWANA



| SURA : I | UCHEZAJI WA KIUNGWANA |
|---|---|
| **Kanuni : 1** | **Uchezaji wa Kiungwana** |

Wachezaji wanatakiwa kuzingatia Kanuni 10 za FIFA za mchezo wa Kiungwana *(fair play)* ndani na nje ya uwanja wa mchezo.

### 1: Cheza Kiungwana

Ushindi hauwezi kuwa na thamani iwapo umepatikana katika njia isiyo halali au kwa udanganyifu. Kudanganya ni rahisi lakini haileti raha ya ushindi. Kucheza kiungwana inahitaji moyo na tabia njema. Pia hufurahisha zaidi. Mchezo wa kiungwana siku zote una malipo yake hata kama utapoteza mchezo. Kucheza kiungwana kunakujengea heshima wakati kudanganya kunaleta aibu. Kumbuka kuwa mpira wa miguu ni mchezo na mchezo wowote hauwezi kuwa na maana kama hautochezwa kiungwana kwa kuzingatia kanuni na taratibu ili mshindi halali aweze kupatikana.

### 3: Heshimu Sheria za Soka

Michezo yote inalindwa na sheria. Bila sheria itakuwa ni vurugu tupu. Sheria za mpira wa miguu ni nyepesi na rahisi kujifunza. Hakikisha unajifunza; itakusaidia kuufahamu mpira wa miguu vizuri zaidi. Kuufahamu mchezo zaidi itakufanya uwe mchezaji bora zaidi. Pia ni muhimu kufahamu madhumuni ya sheria zilizowekwa. Zimekusudiwa kuufanya mchezo uwe na ladha katika kuucheza na kuuangalia. Kwa kufuata sheria, mchezo wa mpira wa miguu utakuwa na burudani zaidi.

### 5: Dumisha Maslahi ya Mpira

Mpira wa miguu ndiyo mchezo unaoongoza duniani. Lakini siku zote unahitaji msaada wa kila mmoja kuufanya uendelee kuwa mchezo wenye kupendwa zaidi. Fikiria maslahi ya mpira kabla ya maslahi yako mwenyewe. Fikiria ni vipi vitendo vyako vinaweza vikaupaka matope mchezo wa mpira wa miguu. Zungumzia mambo mazuri ya mchezo wa mpira wa miguu. Shawishi watu wengine kuuangalia na kuucheza kiungwana. Wasaidie wengine kupata burudani ya kutosha katika mchezo wa mpira wa miguu kama unayoipata wewe. Kuwa balozi wa mchezo wa mpira.

### 2: Tafuta Ushindi, Kubali Kushindwa

Kushinda ndiyo lengo la kushiriki katika mchezo wowote ule. Siku zote usijiandae kushindwa. Iwapo huchezi kwa nia ya kushinda utakuwa unawadanganya wapinzani wako, unawadhulumu watazamaji na pia unajifanya mwenyewe kuwa ni mjinga. Usikate tamaa hata siku moja unapopambana na wapinzani wenye nguvu zaidi lakini pia usidharau hata siku moja unapopambana na wapinzani dhaifu. Ni kumkosea adabu mpinzani unapocheza chini ya kiwango chako. Cheza kwa nia ya kutafuta ushindi hadi dakika ya mwisho lakini kumbuka hakuna anayeshinda wakati wote. Siku nyingine utashinda na siku nyingine utashindwa. Jifunze kukubali kushindwa. Usitafute visingizio unapofungwa. Sababu za kweli siku zote zitadhihirika. Wapongeze washindi bila kinyongo. Usilaumu waamuzi wala mtu mwingine yoyote. Jizatiti kufanya vizuri zaidi wakati mwingine. Walioshindwa na kukubali wanapata heshima zaidi kuliko washindi wanaolazimisha.

### 4: Heshima kwa Wote

Mchezo wa kiungwana unamaanisha kuheshimu wapinzani. Bila ya wapinzani kutakuwa hakuna mchezo. Kila mmoja ana haki sawa, ikiwemo haki ya kuheshimiwa. Wachezaji wa timu moja ni wenza. Tengeneza timu ambayo kila mmoja kwenye timu atakuwa na haki sawa. Waamuzi wapo kuhakikisha nidhamu na mchezo wa kiungwana unadumishwa. Siku zote kubali maamuzi yao bila ya ulalamishi, na wasaidie waweze kuwafanya washiriki wote waufurahie zaidi mchezo. Viongozi pia ni sehemu ya mchezo na wanatakiwa wapewe heshima wanayostahili. Watazamaji wanaufanya mchezo uwe na msisimko. Wanahitaji kuuona mchezo ukichezwa kiungwana kwa kuzingatia kanuni, lakini pia wanatakiwa kuwa waungwana na kujiheshimu.

### 6: Heshimu wanaolinda Heshima

Jina zuri la mchezo wa mpira wa miguu limeendelea kudumu kwa sababu idadi kubwa ya watu wenye kuupenda mchezo huu ni wakweli na waungwana. Wakati mwingine mtu hufanya jambo kubwa ambalo linastahili tulitambue. Watu kama hawa wanastahili kutuzwa na mambo mema waliyofanya yatangazwe. Hii itashawishi wengine kuiga mifano yao. Saidia kuendeleza mpira wa miguu kwa kuyatangaza mazuri yake.

### 8: Wasaidie Wengine Kupambana

Wakati mwingine unaweza kusikia wachezaji wenzako au watu wengine unaowafahamu wanashawishiwa wadanganye kwa njia moja au nyingine au washiriki katika vitendo visivyokubalika katika mchezo wa soka. Wanahitaji msaada wako. Usisite kusimama upande wao. Wape nguvu ya kukataa vishawishi. Wakumbushe wajibu wao kwa wenzao na kwa mchezo wenyewe. Tengeneza umoja wenye mshikamano, kama ngome ngumu kabisa kwenye mchezo wa soka.

### 10: Soka Kujenga Dunia Bora zaidi

Soka ina nguvu ya ajabu inayoweza kutumika kuifanya dunia kuwa sehemu bora zaidi ya kuishi. Tumia nguvu hii kudumisha amani, usawa, afya na elimu. Ifanye soka iwe bora zaidi, ipeleke kwa jamii kujenga dunia bora zaidi.

### 7: Kataa Mambo yote ya Hatari

Umaarufu mkubwa wa mchezo wa mpira wa miguu wakati mwingine huufanya uwe rahisi kuathiriwa na mambo mabaya ya nje. Jichunge na vishawishi vitakavyokufanya ushawishike kushiriki kwenye kudanganya au kutumia madawa yaliyokatazwa. Madawa yaliyokatazwa hayana nafasi katika soka, mchezo mwingine wowote na jamii kwa jumla. Sema hapana kwa madawa ya kulevya. Saidia kuupiga teke ubaguzi kwenye soka. Wachukulie wachezaji wote na wengineo kuwa ni sawa bila kujali dini zao, kabila, jinsia au utaifa wao. Usivumilie hata kidogo kamari katika michezo unayoshiriki. Inaporomosha kiwango chako cha uchezaji na inasababisha hali ya mgongano wa maslahi. Thibitisha kuwa soka haihitaji fujo, hata kutoka kwa washabiki wako wenyewe. Soka ni mchezo na michezo huleta amani.

### 9: Waibainishe Wachafuzi

Usione aibu kusimama dhidi ya yoyote yule ambayeuna hakika anashawishi wengine kudanganya au kushiriki katika vitendo vingine visivyokubalika. Ni vyema kuwafichua waovu wote ili waweze kuondolewa kabla ya kuleta madhara. Ni uovu kushirikiana na watu waovu. Usiseme tu hapana, wafichue wanaotaka kuichafua soka kabla hawajafanikiwa kuwashawishi wengine.

## Wachezaji pia Wanawajibika Kuzingatia na kudumisha

### (a) Nidhamu

Kudumisha tabia njema nje ya uwanja na wakati wote wa mchezo kwa kucheza bila ya kuwaumiza au kuhatarisha usalama wa wachezaji wa timu pinzani.

### (c) Kutorejeshea

Kutorejeshea *(retaliation)* iwapo mchezaji atafanyiwa rafu au kukashifiwa.

### (b) Mchezo wa Kiungwana

Kutodanganya kuumia au kufanyiwa rafu, kutotumia mbinu zisizo za kiungwana mchezoni au kujiingiza katika vitendo visivyokuwa vya kiuanamichezo kama vile kutukana kwa maneno, ishara au kujihusisha na vitendo vyovyote vya kibaguzi

**(d) Malalamiko**

Ni nahodha pekee anaruhusiwa kuzungumza na waamuzi. Iwapo patatokea malamiko yoyote wakati wa mchezo wachezaji wengine wote wanatakiwa wawe hatua zisizopungua kumi kutoka kwa mwamuzi.

**(e) Kumheshimu Kocha**

Mchezaji wakati wote anatakiwa atii maagizo ya kocha wake. Mchezaji anatakiwa akubali kubadilishwa uwanjani na kuadhibiwa kutokana na vitendo vya utovu wa nidhamu au visivyokuwa vya kiuanamichezo.

**(f) Kuheshimu Nahodha**

Mchezaji anatakiwa amheshimu na atii maagizo ya nahodha wake nje na ndani ya uwanja hususan katika masuala yahusuyo timu na tabia njema kwa jumla.

**(g) Kuheshimu Wachezaji**

Mchezaji awaheshimu wachezaji wenzake, awatie hamasa nje na ndani ya uwanja. asimkashifu mchezaji mwenzake mwenye kufanya makosa.

**(h) Kuheshimu Wapinzani**

Mchezaji awape wachezaji wa timu pinzani heshima yao, awe tayari kutoa msaada kwa mchezaji aliyeumia na kushikana mikono kabla na baada ya mchezo.

**(i) Kuheshimu Waamuzi**

Mchezaji anatakiwa wakati wote kuheshimu maamuzi ya waamuzi na kutozozana nao au kutumia lugha ya matusi au kashfa dhidi yao.

**(j) Kujiheshimu Mwenyewe**

Mchezaji anatakiwa ajiheshimu mwenyewe na ajitunze na asitumie madawa yaliyokatazwa

# SURA: II

## KUUNDWA, MATUMIZI NA TAFSIRI



| SURA : II | KUUNDWA, MATUMIZI NA TAFSIRI |
|---|---|

**Kanuni : 2** — **Kuundwa**

Kanuni hizi zimeundwa chini ya Ibara ya 75(3) ya Katiba ya TFF ya mwaka 2026 na zitatumika kwa Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

**Kanuni : 3** — **Matumizi na Tafsiri**

Katika Kanuni hizi isipokuwa pale ambapo imeainishwa vinginevyo itatafsiriwa na kumaanisha kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| TFF | *Tanzania Football Federation*<br>Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania |
| FIFA | *Federation Internationale de Football Association*<br>Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Mpira wa Miguu |
| CAF | *Confederation of African Football*<br>Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika |
| CECAFA | *Council of East and Central Africa Football Associations*<br>Baraza la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati |
| ZFF | *Zanzibar Football Federation*<br>Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar |
| FA(M) | *Regional Football Association*<br>Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa |
| FA(W) | *District Football Association*<br>Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya |
| FRAT | *Football Referees Association of Tanzania*<br>Chama cha Waamuzi wa Mpira wa Miguu Tanzania |
| TAFCA | *Tanzania Football Coaches Association*<br>Chama cha Makocha wa Mpira wa Miguu Tanzania |
| TASMA | *Tanzania Sports Medicine Association*<br>Chama cha Wataalamu wa Tiba za Wanamichezo Tanzania |
| SPATA | *Soccer Players Association of Tanzania*<br>Umoja wa Wachezaji Mpira wa Miguu Tanzania |
| KAMATI ya UTENDAJI | Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania |
| TPLB | *Tanzania Premier League Board*<br>Bodi ya Ligi Kuu Tanzania |
| KLABU | Klabu ya timu ya Mpira wa Miguu inayoshiriki Ligi |
| KLABU BINGWA | Klabu ambayo timu yake imeshinda kupata nafasi ya kwanza katika msimamo wa Ligi Kuu baada ya Ligi kwisha. |
| TIMU | Timu ya Mpira wa Miguu ya Klabu ya Ligi Kuu |
| MPIRA | Mpira wa Miguu wa kuchezea |
| LIGI KUU | Mashindano ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara |
| CHAMPIONSHIP | Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara |
| KIWANJA | Kiwanja cha kuchezea (Pitch) |

## Kanuni : 4 Tafsiri ya Kanuni

Kikao cha juu kuliko vyote kwa ajili ya tafsiri ya Kanuni hizi kitakuwa ni Kamati ya Utendaji ya TFF na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

# SURA: III
## LIGI



## SURA : III LIGI

### Kanuni : 5 Daraja la Ligi

Kanuni hizi ni kwa ajili ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara tu. Ligi Kuu inaweza kutajwa kwa kutumia jina la Mdhamini wake Mkuu au Mdhamini wa Jina la Ligi.

### Kanuni : 6 Mfumo wa Ligi

(1) Ligi Kuu itashirikisha timu kumi na sita (16), timu kumi na mbili (12) zinazobaki Ligi Kuu, timu mbili (2) zinazopanda moja kwa moja kutoka Ligi Daraja la Kwanza (Championship) na timu mbili (2) zinazopatikana baada ya michezo ya mchujo (playoff) itakayohusisha timu zilizoshika nafasi ya kumi na tatu (13) na kumi na nne (14) kwenye msimamo wa Ligi Kuu na timu mbili (2) zilizoshika nafasi ya tatu (3) na nne (4) kwenye msimamo wa Championship.

(2) Timu mbili (2) za mwisho, zilizoshika nafasi ya 15 na 16 kwenye Ligi Kuu zitashuka moja kwa moja kucheza Ligi Daraja la Kwanza (Championship) msimu unaofuata.

(3) Ligi Kuu itachezwa kwa mtindo wa ligi ya mikondo miwili kwa michezo ya nyumbani na ugenini.

(4) Michezo ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara inaweza kuchezwa kwenye viwanja vilivyopo Tanzania visiwani (Zanzibar) kwa mazingatio ya Kanuni 9 kuhusu Uwanja.

### Kanuni : 7 Michezo ya Mchujo

(1) Kutakuwa na michezo ya mchujo baada ya kumalizika Ligi Kuu na Championship.

(2) Michezo ya mchujo kwa hatua ya kwanza itazikutanisha timu za Ligi Kuu zilizoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye msimamo wa Ligi itakayochezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini, timu iliyoshika nafasi ya 14 itaanzia nyumbani.

(3) Kama timu zitafanana idadi ya mabao katika michezo miwili ya nyumbani na ugenini, mshindi atapatikana kwa kuangalia timu iliyofunga mabao mengi zaidi kwenye mchezo wa ugenini.

(4) Kama timu zitafanana kwa idadi ya mabao ya ugenini au kama hakutakuwa na bao lililofungwa katika michezo yote miwili, mshindi atapatikana kwa mapigo ya penati kwa mujibu wa sheria za mpira wa miguu.

(5) Timu mshindi wa jumla itabaki Ligi Kuu na timu iliyoshindwa itacheza michezo ya mchujo hatua ya pili dhidi ya timu mshindi wa jumla wa michezo ya mchujo ya Championship (kwa nafasi ya Ligi Kuu) ambayo itaanzia nyumbani.

(6) Timu mshindi wa jumla wa michezo ya mchujo hatua ya pili (Kanuni 7.3) itapata hadhi kushiriki Ligi Kuu na mshindwa atapata hadhi ya kushiriki Championship msimu unaofuata.

(7) Katika michezo ya mchujo, timu iliyomchezesha mchezaji aliyethibitishwa usajili wake lakini aliyebainika kubadili jina kwa nia ya kudanganya au kubainika kutumika udanganyifu mwingine wowote kufanikisha kukamilisha usajili wake au mchezaji aliyebainika usajili wake kuwa na kasoro baada ya kuthibitishwa, italipa faini kati ya shilingi milioni (1,000,000/-) na shilingi milioni tano (5,000,000/-) na itakuwa imepoteza mchezo huo na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata, timu pinzani itapewa alama tatu na mabao matatu pamoja na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata bila kujali matokeo ya mchezo wa mkondo mwingine uliochezwa.

(8) Katika michezo ya mchujo timu itakayobainika kumchezesha mchezaji ambaye hajasajiliwa itapoteza mchezo husika, italipa faini ya shilingi milioni mbili (2,000,000/-) na mchezaji husika atafungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili (12) bila ya kujali kulalamikiwa au la, itakuwa imepoteza mchezo huo na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata, timu pinzani itapewa alama tatu na mabao matatu pamoja na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata bila kujali matokeo mchezo wa mkondo mwingine uliochezwa.

## Kanuni : 8 Mshindi

(1) Katika mchezo wowote wa Ligi Kuu mshindi itakuwa timu iliyofunga goli/magoli mengi zaidi ya timu pinzani ambapo itapata pointi 3 (tatu) na endapo timu zitatoka sare zitapata pointi moja kila moja na timu itakayoshindwa itakosa pointi.

(2) Mshindi katika Ligi Kuu ni timu iliyopata pointi nyingi zaidi ya timu zote zilizoshiriki katika Ligi Kuu kwa msimu husika.

(3) Endapo timu zitalingana pointi mshindi itakuwa timu iliyo na wastani bora katika matokeo ya michezo iliyokutanisha timu hizo (head-to-head aggregate).

(4) Endapo timu zitalingana pointi na wastani bora katika matokeo ya michezo iliyokutanisha timu hizo, mshindi itakuwa timu iliyo na tofauti bora ya magoli ya kufunga na kufungwa (goals difference).

(5) Endapo timu zitalingana pointi, wastani katika matokeo ya michezo iliyokutanisha timu hizo na tofauti ya magoli ya kufunga na kufungwa (goals difference), mshindi itakuwa timu iliyofunga magoli mengi zaidi.

(6) Endapo timu zitalingana pointi, wastani katika matokeo ya michezo iliyokutanisha timu hizo, tofauti ya magoli ya kufunga na kufungwa (goals difference) na idadi ya magoli ya kufunga, mshindi itakuwa timu iliyofungwa mabao machache zaidi.

(7) Endapo timu zitalingana pointi, wastani katika matokeo ya michezo iliyokutanisha timu hizo, tofauti ya magoli ya kufunga na kufungwa (goals

difference), idadi ya magoli ya kufunga na idadi ya mabao ya kufungwa, mshindi itakuwa timu iliyoshinda michezo ya ugenini mingi zaidi.

(8) Endapo timu zitalingana pointi, wastani katika matokeo ya michezo iliyokutanisha timu hizo, tofauti ya magoli ya kufunga na kufungwa (goals difference), idadi ya magoli ya kufunga, idadi ya mabao ya kufungwa na idadi ya ushindi katika michezo ya ugenini, mshindi itakuwa timu iliyoonesha nidhamu zaidi (idadi ndogo ya kadi walizooneshwa wachezaji na maofisa wa ufundi).

(9) Endapo hatua zote za kanuni 8:3,4,5,6,7 na 8 hazitoi mshindi, timu hizo zitacheza mchezo mmoja katika uwanja utakaochaguliwa na TPLB, na taratibu zote za kupata mshindi zitafuatwa kama inavyosomeka kwenye Kanuni ya 8.10

(10) Timu itakayomaliza ikiwa mshindi wa kwanza wa Ligi Kuu itakuwa ndio Klabu Bingwa ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

(11) Klabu Bingwa ya Ligi Kuu itawakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya CECAFA ya Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki na Kati.

(12) Klabu Bingwa ya Ligi Kuu itaiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya CAF ya Ligi ya Mabingwa Afrika *(CAF Champions League)*.

(13) Klabu Mshindi wa pili wa Ligi Kuu itawakilisha Tanzania Bara katika Kombe la Shirikisho la CAF iwapo hakutakuwa na Kombe la Shirikisho la TFF au katika Mazingira ya Bingwa wa Ligi kuwa pia ndiye Mshindi wa Kombe la Shirikisho.

(14) Iwapo Klabu Bingwa ya Ligi Kuu ndiye pia Bingwa wa Kombe la Shirikisho la TFF, klabu mshindi wa pili wa Ligi Kuu atawakilisha Tanzania Bara kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho la CAF *(CAF Confederations Cup)*.

(15) Uteuzi wa Uwakilishi wowote wa Mashindano yoyote ambao msingi wake unatokana na Ligi Kuu utafuata ubora wa nafasi ya timu husika katika msimamo wa Ligi Kuu. Timu yoyote itakayochaguliwa kucheza mashindano yatakayoandaliwa ama kuidhinishwa na TFF kutokana na nafasi yao katika Ligi Kuu itawajibika kucheza.

## Kanuni : 9 Uwanja

(1) Uwanja wowote kwa michezo ya Ligi Kuu ni lazima uthibitishwe na TFF. Klabu itachagua na kutambulisha uwanja wake wa nyumbani na kuitaarifu TPLB katika kipindi cha Uthibitisho wa ushiriki Ligi Kuu.

(2) Katika mazingira maalum timu inaweza kucheza mchezo wake wa nyumbani katika uwanja mwingine endapo kuna sababu nzito na za msingi, utambulisho wa uwanja katika mazingira haya pia unawajibika kufanywa katika kipindi cha uthibitisho wa kushiriki ligi au kwa maombi maalum kwa TPLB angalau siku 7 (saba) kabla ya tarehe ya mchezo husika.

(3) Katika kutambulisha uwanja wake wa nyumbani, klabu inawajibika kuhakikisha kuwa uwanja huo unakidhi vigezo vyote na masharti kama vilivyoainishwa kwenye kanuni za leseni za klabu.

(4) Endapo timu yoyote haina uwanja wa nyumbani unaofaa kwa mchezo wa Ligi Kuu inaweza kuchagua uwanja mwingine katika mji au mkoa jirani na mkoa wa timu husika ndani ya Tanzania Bara ulio na sifa zinazokubalika na uthibitishwe au kuidhinishwa na TFF, baada ya uteuzi wa uwanja timu haitaruhusiwa kubadilisha uwanja huo kinyume na sababu za kikanuni.

(5) Kutokana na sababu za kiusalama, uwanja kutofikika, kushindwa kukidhi vigezo vya Leseni za Klabu au sababu nyingine yoyote ya msingi, TFF kwa kushauriana na timu mwenyeji inaweza kuhamishia mchezo husika katika uwanja wa mji au mkoa jirani unaokidhi haja hiyo.

(6) TFF/TPLB ina mamlaka ya mwisho ya kuhamishia mchezo wowote katika uwanja mwingine tofauti na uliochaguliwa na kutambulishwa na timu mwenyeji au kubadilisha kituo cha mchezo kwa sababu inazoona zinafaa kwa mchezo na wakati husika.

(7) Timu ya Ligi Kuu inaweza kuteua viwanja vingine miongoni mwa viwanja vilivyokaguliwa na kukidhi vigezo vya kikanuni kutumika kwa michezo ya Ligi Kuu kwa michezo yake miwili tu ya nyumbani ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwasilisha uteuzi wake huo siku ishirini na moja (21) kabla ya mchezo husika inaokusudia kucheza kwenye uwanja wa uteuzi. Masharti ya uwasilishaji yatazingatia pia Kanuni ya 9.3 ya Kanuni hizi. Uwanja ukishapitishwa hautabadilishwa isipokuwa kwa mazingatio ya Kanuni ya 9.6.

(8) Uwanja wa michezo ya Ligi utakaofunguliwa baada ya kuwa umefungiwa na Kamati ya Leseni za Klabu, hautaruhusiwa kupangiwa mchezo na TFF/TPLB mpaka kitakapokamilika kipindi cha siku saba (7) za uangalizi, maandalizi na kukidhi haja ya matumizi ya uwanja huo.

## Kanuni : 10 Ushiriki Mashindano ya Kimataifa na Mengineyo

(1) Endapo Tanzania Bara itapata nafasi nne (4) za uwakilishi kwenye mashindano ya CAF, bingwa na klabu iliyoshika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu wataiwakilisha Tanzania Bara kwenye Ligi ya Mabingwa ya CAF na bingwa wa Kombe la Shirikisho la TFF na

timu iliyoshika nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu wataiwakilisha Tanzania Bara kwenye Kombe la Shirikisho la CAF.

(2) Iwapo itatokea kati ya Klabu Bingwa Ligi Kuu na Klabu mshindi wa Pili Ligi Kuu mmoja wapo kutoshiriki kwa namna moja au nyingine, Klabu Mshindi wa Tatu wa Ligi Kuu itashiriki mashindano hayo.

(3) Endapo klabu bingwa wa Ligi Kuu au timu iliyoshika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu itakuwa ndiye Mshindi wa Kombe la Shirikisho la TFF, timu zilizoshika nafasi ya tatu (3) na nne (4) kwenye msimamo wa Ligi Kuu zitaiwakilisha Tanzania Bara kwenye Kombe la Shirikisho la CAF.

(4) Endapo Kombe la Shirikisho la TFF halipo/halikufanyika, mshindi wa tatu (3) na wa nne (4) wa Ligi Kuu watashiriki Kombe la Shirikisho la CAF.

(5) Endapo Klabu Mshindi wa Kombe la Shirikisho ndio huyo huyo mshindi wa tatu (3) wa Ligi Kuu, Mshindi wa nne (4) wa Ligi Kuu atashiriki Kombe la Shirikisho la CAF.

(6) Endapo Klabu Mshindi wa Kombe la Shirikisho la TFF atakuwa ndio Klabu Bingwa Ligi Kuu ama Mshindi wa pili wa Ligi Kuu, Mshindi wa tatu (3) na wa nne (4) wa Ligi Kuu watashiriki Kombe la Shirikisho la CAF.

(7) Timu inayoshiriki mashindano ya kimataifa inawajibika kufuata na kuheshimu ratiba ya michezo ya Ligi Kuu kama ilivyotolewa na Bodi ya Ligi Kuu.

(8) Kutakuwa na shindano la Kombe la Muungano ambalo litahusisha timu zitakazoteuliwa kutoka Tanzania Visiwani na Tanzania Bara. Timu shiriki kutoka Tanzania Bara zitapewa taarifa rasmi na TFF/TPLB.

## Kanuni : 11 Vikombe na Tuzo

(1) Timu Bingwa wa Ligi Kuu itakabidhiwa kikombe cha ubingwa wa Ligi Kuu ambapo Bodi ya Ligi Kuu itapanga utaratibu wa sherehe.

(2) Endapo timu itachukua ubingwa kabla ya ligi kumalizika itapata heshima kutoka kwa timu pinzani kwa kila mchezo uliosalia wa Ligi Kuu itakaocheza kwa kujipanga kusalimiana kwa pongezi *(guard of honour)* kabla ya ukaguzi wa kuanza mchezo.

(3) Klabu Bingwa wa Ligi Kuu itahodhi kikombe cha ubingwa ilichokabidhiwa mpaka itakapotakiwa na Bodi ya Ligi Kuu kukirejesha. Endapo Klabu Bingwa itatakiwa kurejesha kikombe itapewa kikombe kingine kinachofanana badala yake.

(4) Medali, tuzo na kikombe kingine chochote kinachotolewa kama zawadi kwenye Ligi Kuu hakitarejeshwa, kitakuwa cha kudumu kwa aliyetunukiwa.

(5) Wachezaji, Kocha Mkuu na Maafisa wa Benchi la Ufundi wa Klabu Bingwa ya Ligi Kuu watapewa Medali za Ubingwa wa Ligi Kuu. Wahusika wengine wa kutunukiwa Tuzo/Medali watatunukiwa kwa Utaratibu utakaowekwa.

(6) Rais wa TFF ndiye atakayetoa Medali, Kombe na zawadi nyinginezo kwa Timu Bingwa na wahusika wengine. Endapo kutakuwa na Mgeni Rasmi aliyealikwa, Rais wa TFF atamshirikisha ipasavyo Mgeni Rasmi husika na wageni wengineo katika zoezi la Utoaji zawadi mbalimbali kwa wahusika.

(7) TFF kwa kushirikiana na TPLB itaweka miongozo, sifa na vigezo vya ushindi *(zitakazosomeka pamoja na kanuni hizi)* kwa wahusika/makundi maalum yatakayoshinda kwa kupewa tuzo za Ligi Kuu. Washindi wa Tuzo mbalimbali za Ligi Kuu watapatikana kutokana na kupata alama zaidi ya washindani wao kwa mujibu wa sifa na vigezo vilivyowekwa.

(8) Hairuhusiwi kwa Timu, Kiongozi, Kocha, Mwamuzi, Mchezaji na Ofisa mwingine yeyote wa timu ya Ligi Kuu kushiriki au kuchukua kikombe au tuzo yoyote kuhusiana na Ligi Kuu au ushiriki wake kwenye Ligi Kuu kutoka kwa mamlaka nyingine yoyote bila idhini ya TFF au kukaidi miongozo kuhusiana na Tuzo kwa Ligi Kuu. Ukiukwaji wa sharti hili utavutia adhabu ya faini au kifungo au vyote kwa pamoja kwa mhusika.

(9) Muhusika yoyote aliyeteuliwa katika Orodha ya wanaowania Tuzo za Ligi Kuu anawajibika kufuata maelekezo ya TFF kwa ajili ya Tuzo za Ligi Kuu ikiwemo ulazima wa kuhudhuria Sherehe za Tuzo. Mteule yoyote kuwania Tuzo za Ligi Kuu atakayeshindwa kufuata Utaratibu, maelekezo na Kuhudhuria Sherehe za Tuzo bila ridhaa ya TFF/TPLB atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo faini, kufungiwa michezo au kipindi fulani pamoja na kupoteza nafasi ya kuwa Mshindi na nafasi yake kuchukuliwa na mshindani anayemfuatia kutokana na vigezo.

(10) Bodi ya Ligi Kuu kwa kushirikiana na TFF itatayarisha na kusimamia utaratibu wa kupatikana kwa mchezaji Bora wa mchezo kwa kila mchezo wa Ligi Kuu.

(11) Sherehe za tuzo zitafanyika baada ya kumalizika kwa msimu husika katika tarehe itakayotangazwa na TFF.

(12) Kutakuwa na Tuzo ya Mfungaji Bora kulingana na mashindano mbalimbali ambayo Kamati ya Tuzo itakuwa imeamua kutoa tuzo kwa wahusika.

12 . 1 Mashindano yaliyokuwa na mfumo wa hatua ya kwanza na fainali zake kwa pamoja, magoli ya wafungaji bora yatahesabika kuanzia hatua ya awali hadi fainali.

(13) Mshindi wa tuzo ya Mfungaji Bora ni mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kuliko wengine katika shindano husika. Ikitokea

wachezaji zaidi ya mmoja wamefungana idadi ya mabao, vigezo vifuatavyo vitatumika kwa kufuata mpangilio ili kumpata mshindi;

13.1 Magoli yaliyofungwa kwa njia ya kawaida yatakuwa na alama mbili (2) na magoli yaliyofungwa kwa njia ya penati yatakuwa na alama moja (1). Mchezaji mwenye alama nyingi atakuwa mshindi.

13.2 Endapo watalingana alama, mchezaji aliyecheza muda mchache zaidi atakuwa mshindi.

13.3 Endapo watafanana katika vigezo vyote viwili hapo juu, mchezaji aliyefunga mabao mengi ugenini atakuwa mshindi.

13.4 Katika mashindano ya mtoano, Mshindi atakuwa mchezaji ambaye timu yake imefika hatua ya juu zaidi kuliko mwingine na endapo hatua hii haitatoa mshindi kipengele cha i-iii vitatumika kwa mpangilio wake.

# SURA: IV

## UTAWALA



## SURA : IV UTAWALA

### Kanuni : 12 Usimamizi wa Ligi

(1) Ligi Kuu itasimamiwa na kuendeshwa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) kwa mujibu wa kanuni hizi. Bodi ya Ligi Kuu katika uendeshaji wa Ligi Kuu itawajibika kushirikiana na vyombo vingine vya TFF katika masuala yaliyo katika mamlaka ya vyombo hivyo.

(2) TFF/TPLB inaweza kushughulikia/kufanyia uchunguzi na kufanyia uamuzi kwa mujibu wa Kanuni hizi, au Kanuni nyingine za adhabu za TFF, CAF na FIFA jambo lolote lisilo la kawaida, la hatari, la kimaadili, la kinidhamu, la kibaguzi au lisilo la kiuanamichezo lililotokea katika mchezo wa Ligi Kuu au katika mwenendo wa shughuli za Ligi Kuu.

(3) TFF/TPLB inaweza kusimamisha kwa kipindi maalum au muda usiojulikana matumizi ya Kituo cha Ligi Kuu au uwanja wowote kwa michezo ya Ligi Kuu endapo itabainika katika kituo/uwanja huo kukithiri vitendo vya fujo na vurugu au kuthibitika kwa mazingira ya kutopatikana haki kwa timu yoyote na/au maofisa wa mchezo.

(4) Kutakuwa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi ya TPLB itakayokuwa na jukumu la kusimamia uendeshaji/mwenendo wa michezo na matukio katika Ligi Kuu pamoja na Usimamizi wa Kanuni za Ligi Kuu.

(5) Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi ya TPLB itaundwa na Mwenyekiti wa TPLB, na kuthibitishwa na Kamati ya Uongozi ya TPLB na itadumu kwa kipindi cha miaka miwili.

(6) Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi itakutana katika hali ya kawaida kwa ratiba ya vikao itakayoratibiwa na Sekretarieti ya TPLB kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kamati. Aidha Kamati ya Uendeshaji itakutana kwa lazima kwa dharura ndani ya saa 72 (sabini na mbili) wakati wowote linapojitokeza jambo la dharura au la kushughulikiwa kwa haraka kuhusiana na uendeshaji na usimamizi wa Ligi Kuu.

(7) Makamishna kwenye michezo ya Ligi Kuu wataandaliwa na kupangwa na Idara ya Mashindano ya TFF kutokana na mchakato na Utaratibu utakaotolewa na TFF. Katika Mazingira Maalum, TFF inaweza kuteua Kamishna wa mchezo wa Ligi Kuu itavyoona inafaa.

(8) Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi inaweza kufuta adhabu ya kadi yoyote iliyotolewa uwanjani na mwamuzi, na kuondoa adhabu inayoambatana na kadi hiyo endapo inathibitika bila mashaka kuwa mtuhumiwa hakustahili kadi hiyo.

(9) Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi ya TPLB itachukua hatua moja kwa moja kwa vitendo vyovyote vya uvunjifu wa Kanuni vilivyo na ushahidi usio na mashaka vilivyotokea katika mchezo wa Ligi Kuu au kuhusiana moja kwa moja na mchezo ya Ligi Kuu bila ya kujali mahitaji ya kupelekwa kwenye vyombo vingine vya TFF.

(10) Katika Mazingira maalum ya Majanga kiasi cha kusababisha Ligi Kuu kushindwa kuendelea kwa muda unaoathiri Kalenda ya msimu katika hali ya kutorekebishika wakati ikiwa imekwishachezwa michezo zaidi ya nusu kwa msimu husika, TFF itathibitisha Msimamo wa Ligi Kuu kwa wakati husika kuwa ndio Msimamo wa Mwisho na Utatumika kama Msimamo rasmi utakaotambulika kwa timu kutumikia hali ya nafasi zilipo kwenye Msimamo. Katika Mazingira ya Hali ya majanga wakati Ligi Kuu ikiwa bado haijafikia nusu ya michezo yake kwa msimu husika, TFF itafuta Ligi Kuu kwa msimu husika na Hali itasalia kama ilivyomalizika Msimu uliotangulia.

## Kanuni : 13 Uthibitisho wa Ushiriki

(1) Timu itawajibika kutoa taarifa ya maandishi kwa TPLB endapo haitashiriki Ligi Kuu msimu husika katika kipindi cha Maombi ya Leseni ya Klabu.

(2) Ada ya ushiriki wa Ligi Kuu itakuwa shilingi milioni moja (1,000,000/-) ambazo zitalipwa katika kipindi cha uthibitisho wa ushiriki baada ya klabu husika kupata leseni.

(3) Klabu itawajibika kutoa taarifa zake nyingine muhimu kwa TPLB baada ya kupatiwa Leseni ya kushiriki Ligi Kuu. Mabadiliko yoyote ya taarifa zinazotolewa na klabu yataarifiwe kwa TPLB wakati wowote wa mabadiliko hayo.

## Kanuni : 14 Leseni ya Klabu

(1) Klabu ya Ligi Kuu inawajibika na kutakiwa kuwasilisha kwa TFF maombi ya kupatiwa Leseni ya Klabu katika muda utakaotangazwa na Kamati ya Leseni za Klabu ya TFF na kuhakikisha inakidhi masharti na vigezo vyote vya msingi vya kupatiwa leseni ili kushiriki Ligi Kuu. Klabu itakayoshindwa kukidhi masharti ya kupatiwa Leseni haitashiriki Ligi Kuu kwa msimu husika.

(2) Klabu ya Ligi Kuu iliyopata nafasi ya Kushiriki Mashindano Kimataifa, itawajibika kukidhi Masharti ya Leseni ya Klabu (Club Licencing) kwa kiwango cha Masharti hayo Kimataifa ili iweze kuwa na sifa za kushiriki Mashindano husika. Kushindwa kutimiza masharti husika ipasavyo kutapelekea Klabu husika kupoteza nafasi yake ya ushiriki kwa msimu husika.

## Kanuni : 15 Msimu na Ratiba

(1) Kamati ya Utendaji ya TFF itatangaza kuanza na kumalizika Msimu wa Ligi Kuu.

(2) Timu zinawajibika kufuata utaalamu wa kiufundi katika kuzingatia matumizi sahihi ya vipindi vya mapumziko katika msimu *(off season)*, kipindi cha matayarisho *(preseason)* na kipindi cha kucheza Ligi.

(3) Ratiba ya Ligi Kuu itapangwa na TPLB kwa kushirikiana na TFF na itatolewa angalau wiki nne (4) kabla ya Ligi kuanza isipokuwa katika mazingira maalum.
Ratiba ikishatolewa haitabadilishwa isipokuwa tu kwa dharura au sababu nzito na za msingi.

## Kanuni : 16 Udhamini

(1) TFF/TPLB itatoa maelekezo na mwongozo kuhusu masharti na makubaliano ya msingi kimkataba na Mdhamini ambapo Klabu, timu, wachezaji na wadau wengine watawajibika kuheshimu na kutekeleza.

1.1 Nembo ya Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu itawekwa kwa rangi zake halisi katika mkono wa kulia kwenye sare za timu za kuchezea, na timu zitalazimika kufanya hivyo kwa michezo yake yote ya Ligi Kuu.

1.2 Timu zinazoshiriki Ligi Kuu na waamuzi wanatakiwa wahakikishe wanavaa vifaa vilivyotolewa na Mdhamini wa Ligi Kuu *(endapo vimetolewa)* katika michezo wanayoshiriki ya Ligi Kuu.

1.3 Timu zitalazimika kuweka nembo ya mdhamini kwenye vifaa vyake vya kuchezea kama inavyoelekezwa na Kanuni hizi au kwa Maelekezo Maalum ya TFF.

1.4 Hairuhusiwi kuweka matangazo ya kampuni ambayo ina ushindani wa moja kwa moja wa kibiashara na Mdhamini wa Ligi Kuu.

1.5 Matangazo au mabango ya mdhamini/wadhamini wa Klabu yasiyozidi kumi *(katika vipimo vya 600cm x 90cm kwa kila bango)* yatawekwa katika mchezo wa klabu husika kwenye uwanja wake wa nyumbani tu akiwa ni timu mwenyeji. Klabu ngeni italazimika kuwa na makubaliano maalum na timu mwenyeji wake wa mchezo endapo itahitaji kuweka matangazo ya mdhamini/wadhamini wake binafsi uwanjani katika mechi yake ya ugenini.

1.6 Matangazo yasiyokuwa ya wadhamini Ligi Kuu au klabu au yasiyoidhinishwa na TFF hayatoruhusiwa kwenye maeneo ya uwanja wakati wa michezo na shughuli zinazohusiana na Ligi Kuu.

1.7 Klabu inawajibika kuheshimu masharti ya udhamini wa Ligi Kuu kimkataba kwenye michezo yake kama inavyoelekezwa na TFF/TPLB, timu itakayokiuka itatozwa faini ya shilingi milioni kumi (10,000,000/-) kwa kila mchezo itakaokiuka na inaweza kuchukuliwa hatua zaidi ikiwemo kushushwa daraja na/au kufungiwa.

1.8 Klabu itakayofanya jambo lolote *(ambalo halihusiani na*

*mchezo wake)* la kukiuka masharti ya mikataba ya wadhamini kama ilivyoelekezwa na TFF/TPLB itatozwa faini ya shilingi milioni tatu *(3,000,000/-)* na endapo itakaidi zaidi inaweza kuchukuliwa hatua zaidi ikiwemo kuondolewa kwenye Ligi Kuu.

1.9 Mwamuzi anawajibika kuvaa sare zinazotolewa na mdhamini wa Ligi Kuu kwenye michezo atakayoshiriki na kwa makusudio mengine yaliyowekwa.

1.10 Klabu yoyote inayotaka kuingia mkataba na mdhamini binafsi inalazimika kuwasilisha rasimu ya mkataba huo kwa TFF kabla ya kutia saini kuingia mkataba huo, na baada ya kuingia mkataba klabu inawajibika kutambulisha mdhamini wake kwa TFF/TPLB ikiambatanisha na nakala ya mkataba wa udhamini huo.

1.11 Hairuhusiwi kwa klabu/mchezaji/kiongozi wa klabu/mwamuzi kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na mdhamini wa Ligi bila ruhusa ya TFF kuhusu masuala yanayohusu mkataba wa udhamini. Yeyote atakayekiuka atafungiwa kipindi kati ya miezi mitatu (3) na kumi na miwili (12) au faini isiyopungua shilingi milioni kumi (10,000,000/-).

1.12 Hairuhusiwi kwa mchezaji kuingia mkataba binafsi wa udhamini na mshindani wa kibiashara wa Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu, atakayekiuka atafungiwa kwa kipindi cha kati ya mwezi mmoja (1) na mitatu (3).

(2) Klabu za Ligi Kuu zitakuwa na haki ya kulipwa stahili zao zote zinazotokana na udhamini wa ligi kama ilivyokubalika bila kukosa na kuchelewa zikiwemo zawadi na tuzo kwa wanaostahili.

(3) Ligi Kuu ya Tanzania Bara inaweza kubadilishwa jina na kutajwa kwa jina la Mdhamini Mkuu/Mdhamini wa Jina la Ligi Kuu wake katika kukidhi masharti ya mkataba wa udhamini.

(4) Haki zote za Matangazo ya Televisheni na Redio *(Tv & Radio Rights)*, za habari za machapisho *(print)* na za habari za kielektroniki *(electronic)* kuhusiana na Ligi Kuu ni mali ya TFF.

(5) Haki zote za matangazo kwenye viwanja inapochezwa michezo ya Ligi Kuu ni mali ya TFF. TFF itaweka mazingatio kwa matangazo ya Wadhamini wa Ligi Kuu na Wadhamini binafsi wa klabu za Ligi Kuu waliotambuliwa na TFF.

(6) Hairuhusiwi kwenye Uwanja wowote unaochezwa mchezo wa Ligi Kuu kuwekwa matangazo ya aina yoyote wakati wa mchezo wa Ligi Kuu bila kibali cha TFF. Timu mwenyeji itawajibika kwa ukiukwaji wowote wa sharti hili na kuvutia adhabu dhidi yake.

(7) Klabu za Ligi Kuu zinawajibika/zinatakiwa kuwa na mdhamini/wadhamini binafsi kwa mazingatio ya Kanuni ya

16:1(1.10) ili kukidhi gharama za uendeshaji wa timu na maendeleo ya klabu kwa ujumla.

# SURA: V

## MCHEZO



| SURA : V | MCHEZO |
|---|---|
| Kanuni : 17 | Taratibu za Mchezo |

(1) Michezo yote ya Ligi Kuu itachezwa kwa kufuata sheria kumi na saba za mpira wa miguu za FIFA *(17 Laws of the Game)*.

(2) Kutakuwa na mkutano wa kitaalamu wa Maandalizi na Uratibu wa mchezo (MCM) utakaofanyika kabla ya mchezo, saa 4:00 (nne) asubuhi siku ya mchezo. Kwa sababu maalum, mkutano huu unaweza kupangiwa muda, siku na mahali pengine kama itakavyopendekezwa na FA(M) na kuidhinishwa na Kamishna wa mchezo au GC wa mchezo (kama ameteuliwa).

2.1 Wanaotakiwa kuhudhuria kikao cha MCM ni:
- 2.1.1 Wawakilishi wa Timu kwa mchezo husika *(Mkuu wa Msafara, Meneja, Daktari, Afisa Vifaa, Afisa Usalama)*
- 2.1.2 Kamishina wa Mchezo *(atakuwa Mwenyekiti wa Kikao)*
- 2.1.3 Mratibu wa mchezo (GC)
- 2.1.4 Waamuzi wa mchezo *(wanaweza wasiwepo endapo kuna Mtathimini wa waamuzi)*
- 2.1.5 Mamlaka ya Uwanja
- 2.1.6 Msimamizi wa Vijana wa Mipira (ball kids)
- 2.1.7 Huduma ya Kwanza
- 2.1.8 Afisa Usalama wa TFF/Kituo
- 2.1.9 Mamlaka ya Polisi ya eneo husika
- 2.1.10 Mamlaka ya Zimamoto
- 2.1.11 Daktari wa Mchezo
- 2.1.12 Mwakilishi wa Mdhamini mwenye haki za matangazo ya runinga

2.2 Timu inawajibika kufika kwenye kikao cha kitaalamu cha maandalizi ya mchezo bila kukosa kwa wakati ikiwakilishwa na viongozi waliotajwa (kanuni 17:2(2.1) wakiwa kamili na vifaa tajwa (kanuni 17:2(2.3) kwa idadi na nafasi na si mwingine yeyote asiyetajwa.

2.3 Kila timu inatakiwa kufika na vifaa vyake, jezi, bukta na soksi watakavyotumia kwa mchezo husika kwa mpangilio ufuatao:

- 2.3.1 Sare ya Vifaa kwa Wachezaji wa Ndani (Field players)
- 2.3.2 Sare ya Vifaa kwa Walinda Mlango (Goalkeepers)
- 2.3.3 Timu Ngeni ifike na Sare za Nyumbani na Ugenini/ya ziada
- 2.3.4 Sare ya Vifaa vya Mazoezi mchezoni (warming Up kit)
- 2.3.5 Kitambaa cha Alama ya Nahodha (Captain Armband)
- 2.3.6 Sare ya Maofisa wa Benchi la Ufundi (Technical Officials)
- 2.3.7 Msimamizi ahusike na Sare za Vijana wa mipira (Ball Kids)

2.4 Ni sare zilizoamuliwa kwenye MCM tu kwa wachezaji na viongozi ndizo zitakazoruhusiwa kuvaliwa wakati wa mchezo.

2.5 Kila jezi inatakiwa kuwa na namba kubwa zinazosomeka

vizuri zilizo kati ya namba 1 (moja) hadi 70 (sabini).

2.6 Endapo rangi katika sare za timu mbili zitafanana, timu ngeni italazimika kubadili sare yake na endapo moja ya timu sare zake zitafanana na sare za waamuzi, waamuzi watalazimika kubadili. Taratibu za mabadiliko lazima zijulikane kwenye kikao cha MCM.

2.7 Sare ya mlinda mlango isifanane rangi na sare *(jezi)* za wachezaji wa ndani na mlinda mlango wa timu pinzani.

2.8 Kikao cha maandalizi ya mchezo (MCM) kinaweza kufanyika kwa njia ya mtandao kwa mazingatio ya Kanuni 17:2.

2.9 Timu mwenyeji kwa kushirikiana na Msimamizi wa Kituo ina jukumu la kuandaa ukumbi kwa ajili ya Kikao cha Maandalizi ya Mchezo (MCM) wenye sifa na vigezo kama itakavyoelekezwa na TPLB/TFF.

2.10 Maafisa wote wa bechi la ufundi wanapaswa kuvaa sare zenye vifupisho vya majina yao katika kila mchezo wa Ligi Kuu.

(3) Endapo kutatokea kufanana sare za timu wakati wa ukaguzi kabla ya mchezo kuanza, timu ambayo haikufika kwenye MCM itawajibika kubadili sare zake.

(4) Kamishna atahakikisha timu zinatumia sare kwa mujibu wa rangi za nyumbani, ugenini na ziada kama zilivyoandikishwa na klabu kwa TPLB.

(5) Timu zitaheshimu uchaguzi wao wa rangi za sare zao kwa michezo ya nyumbani na ugenini/ya ziada *(katika mazingira ya mgongano wa rangi)*, na endapo itatokea timu ya nyumbani kukosa uzingativu wa kuwasilisha rangi sahihi kwa sare zake kwa mechi za nyumbani katika kikao kitangulizi cha MCM timu ngeni itakuwa na haki ya kwanza ya kuchagua rangi ya sare katika mchezo husika.

(6) Timu zinazocheza mchezo husika zinatakiwa kuwasilisha kwa Kamishna/Mratibu (GC) wa mchezo Orodha ya Viongozi wasiozidi tisa (9) na wasiopungua saba (7) kwa nafasi zilizoainishwa kwenye Kanuni ya 76.2 ya Ligi Kuu na wachezaji wasiozidi ishirini na mmoja (21) kwa mchezo husika saa tatu (3) kabla ya muda wa kuanza mchezo (kick off) kwa kutumia fomu maalumu iliyojazwa kwa unadhifu na ukamilifu ikiwa imesainiwa na kila mmoja.

6.1 Fomu maalum ni lazima iwe na mfumo (formation) wa uchezaji.

6.2 Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kujumuisha wachezaji wasiopungua wawili (2) kutoka katika timu zake za vijana kwenye orodha ya wachezaji 21 kwa ajili ya kila mchezo wa Ligi Kuu na angalau mmoja apate nafasi ya kucheza kwa angalau asilimia kumi

(10%) ya muda wote wa mchezo husika.

(7) Kila klabu ya Ligi Kuu ina wajibu wa kuhakikisha linakuwepo Gari la wagonjwa *(ambulance)*, watoa huduma ya kwanza, walinzi wa uwanjani (stewards) na vijana waokota mipira *(ball kids)* uwanjani katika kila mchezo wake wa nyumbani timu yake inapocheza. Iwapo huduma hizo hazitakuwepo, Kamishna atazuia mchezo kuchezwa, na timu mwenyeji itapoteza mchezo huo. Klabu itawajibika na kuadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi kwa vitendo vyovyote visivyo vya kiuanamichezo au vinavyovunja taratibu za mchezo vitakavyofanywa na watoa huduma ya kwanza, walinzi wa uwanjani, watoto waokota mipira na watoa huduma wengine wanaoletwa na klabu.

(8) Kocha Mkuu na Viongozi wa Benchi la Ufundi wanawajibika kuvaa sare maalum za timu yao kwa Benchi la Ufundi. Endapo Kocha Mkuu atahitaji kuvaa mavazi tofauti, anawajibika kuwa katika Mavazi Rasmi ambayo ni ya Heshima na Nadhifu. Uvaaji wa Kaptula ya aina yoyote hauruhusiwi kwa Kocha Mkuu. Ukiukwaji wowote utavutia adhabu kwa muhusika na/au kwa timu husika.

(9) Mchezaji anayeruhusiwa kucheza ni yule tu aliye kwenye orodha ya timu iliyowasilishwa kwa Kamishna na kukaguliwa kabla ya kuanza mechi. Mchezaji ambaye hakukaguliwa atahesabika kuwa batili (*non-qualified*).

(10) Michezo yote ya ligi itachezwa kwa vipindi viwili vya jumla ya dakika 90 (tisini) kila kipindi kikiwa na dakika 45 (arobaini na tano) na mapumziko ya dakika zisizopungua 5 (tano) na zisizozidi 15 (kumi na tano) kati ya vipindi hivyo. Mwamuzi wa mchezo ndio mtunza muda.

(11) Mchezaji atakayevaa jezi isiyokuwa na nambari mgongoni ama itakayobandikwa kwa plasta au katika utaratibu wowote ule usiokubalika hataruhusiwa kucheza.

(12) Manahodha wa timu zinazoshindana wanatakiwa kuvaa vitambulisho *(armband)* vya rangi tofauti na jezi zao kwenye mikono ya jezi zao.

(13) Kila mchezaji ni lazima avae kilinda ugoko *(shinguard)* kwenye miguu yote miwili, mchezaji asiyevaa hataruhusiwa kucheza mpaka avae.

(14) Wachezaji/viongozi wa kiufundi hawaruhusiwi kushangilia goli kwa kufanya ishara yoyote isiyokuwa ya kiuanamichezo au ya kashfa au matusi kwa timu pinzani au watazamaji.

(15) Timu zinatakiwa kufika uwanjani si chini ya dakika 90 (tisini) kabla ya muda wa kuanza mchezo na kulazimika kufuata ratiba ya matukio ya mchezo (count down) kama itakavyotolewa na mratibu wa mchezo. Baada ya kuwasili uwanjani katika muda wa kikanuni, wachezaji na maofisa wa benchi la ufundi wa timu wanaruhusiwa kuzuru kiwanja kwa muda usiozidi dakika kumi (10).

(16) Muda wa kuanza mchezo (kickoff) utapangwa katika mazingira ya kawaida na kwa mazingatio maalum ya hali kwa michezo inayoonyeshwa kwenye televisheni, viwanja na sababu nyingine yoyote muhimu. Mabadiliko yoyote ya muda wa kuanza mchezo yatajulishwa ipasavyo kwa pande zote husika za mchezo angalau saa ishirini na nne (24) kabla ya muda wa awali uliopangwa. TPLB/TFF inaweza kubadili muda wa kuanza mchezo (kickoff) kwa mazingatio maalum katika mazingira ya dharura na/au yaliyo nje ya uwezo wa pande zote kwa maana ya TPLB/TFF na Klabu husika.

(17) Ni marufuku kwa viongozi kuingia kiwanjani (pitch) bila sababu za msingi kinyume na taratibu za mchezo kabla, wakati au baada ya mchezo.

(18) Ni marufuku kwa mashabiki kuingia kiwanjani (pitch) kabla, wakati au baada ya mchezo.

(19) Timu zinapokaguliwa au kupeana mikono zenyewe na waamuzi zitalazimika

(20) Baada ya kuwasili Uwanjani katika muda rasmi na muda wote kabla ya kuanza kwa mchezo na wakati wa mapumziko, timu zitalazimika kupumzika kwenye vyumba vyao vya kuvalia kwa kutumia milango rasmi kwa ajili hiyo na si vinginevyo.

20.1 Maofisa watakaokagua chumba cha kuvalia ili kuhakiki usalama wake kiafya na kama kuna changamoto yoyote kutoa taarifa TPLB ni wafuatao;

20.1.1 Daktari wa Uwanja (Venue Doctor)
20.1.2 Madaktari wa timu zote mbili
20.1.3 Mratibu wa Mchezo (GC)
20.1.4 Kamishna wa Mchezo
20.1.5 Ofisa Usalama wa Mchezo, na
20.1.6 Msimamizi wa Kituo

(21) Timu yoyote hairuhusiwi kuruka ukuta wa nje ili kuingia uwanjani *(Stadium)* ama kuruka uzio wa ndani unaotenga watazamaji na kiwanja *(pitch)*, ama kupita katika mlango wowote usio rasmi kwa kuingizia timu.

(22) Wachezaji wote watatambulika kwa kutumia Leseni zao zitakazotolewa na kuidhinishwa na TFF. Mchezaji yeyote ambaye hatakuwa na leseni hatoruhusiwa kucheza katika mchezo husika.

(23) Katika mazingira maalum ya kukosekana Leseni ya mchezaji, TFF inaweza kutoa utambulisho wa dharura/muda ili kukidhi mahitaji ya kikanuni kwa mchezaji kucheza mchezo husika.

(24) Iwapo itathibitika bila kujali kukatwa au kutokatwa Rufaa, kupitia taarifa za mchezo za Kamishna ama kwa njia yoyote kuwa timu imechezesha mchezaji ambaye usajili wake haujathibitishwa na TFF hivyo kuwa batili kiusajili *(non-qualified)* timu hiyo itapoteza mchezo na ushindi kupewa timu pinzani.

(25) Iwapo itathibitika bila kujali kukatwa au kutokatwa Rufaa, kupitia taarifa za mchezo za Kamishna ama kwa njia yoyote kuwa timu imechezesha mchezaji ambaye hajaorodheshwa kwenye fomu

maalum ya Orodha ya wachezaji na viongozi kama mchezaji wa siku hiyo kwa mchezo husika na hivyo kushindwa kupitia mchakato wa ukaguzi wa wachezaji kabla ya mchezo timu hiyo itapoteza mchezo na ushindi kupewa timu pinzani.

(26) Wanaoruhusiwa kukaa kwenye benchi la ufundi wakati wa mchezo ni wachezaji kumi (10) wa akiba na viongozi tisa (9) ambao ni Mwalimu Mkuu *(head coach)* Walimu Wasaidizi *(assistant coaches)* wasiozidi wanne (4), Daktari, Mtaalamu wa tiba ya viungo, Meneja wa Timu na Afisa Vifaa wa Timu.

(27) Endapo timu iliyokiuka maelekezo ya Kanuni (17:26) itakataa kutii maelekezo ya mwamuzi ya kuwaondoa wasiohusika kwenye benchi la ufundi, mwamuzi anaweza kuomba msaada kwa GC/Kamishna/Msimamizi.

(28) Mwamuzi ataanzisha mchezo iwapo tu kuna mipira isiyopungua mitatu (3) yenye sifa zinazokubalika kisheria. Msimamizi wa Kituo/FA(M) watapeleka uwanjani mipira hiyo.

(29) Ni marufuku kwa timu yoyote kukataa kuchezea mpira wowote uliochaguliwa na mwamuzi. Endapo timu yoyote itakataa kuchezea mpira wowote uliochaguliwa na mwamuzi na kusababisha mchezo kuvunjika, au kuchelewa kuanza na kusababisha kuvunjika kwa sababu ya giza, timu hiyo itapoteza mchezo huo na kutozwa faini na timu pinzani itapata ushindi.

(30) Mwamuzi ataanzisha mchezo katika mazingira ya kuanza (kick off) au kuendelea na mchezo iwapo kila timu ina wachezaji 11 (kumi na mmoja) uwanjani. Endapo timu yoyote haitimizi wachezaji 11 (kumi na mmoja) mchezo unaweza kuanzishwa ikiwa tu wachezaji wa kila timu hawapungui 7 (saba) mmoja wao akiwa mlinda mlango.

(31) Endapo timu itakuwa na wachezaji pungufu ya 7 (saba) kabla ya mchezo kuanza au itabakiwa na wachezaji pungufu ya 7 (saba) uwanjani kutokana na wachezaji wake kutoka katika mazingira yasiyoruhusu kuingia mchezaji badala, timu hiyo itakuwa imesababisha mchezo huo kuvunjwa na mwamuzi na hivyo timu pinzani itapewa ushindi na endapo itabainika kuwa hali hiyo imefikia kutokana na udanganyifu au hila yoyote ya kuvuruga mchezo huo, basi hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa kanuni katika sura ya 4 (nne) na/au sura ya 6 (sita) ya Kanuni hizi.

(32) Timu inaruhusiwa kubadilisha wachezaji watano (5) tu katika awamu zisizozidi tatu (3) kwenye mchezo mmoja, wanaoingia badala ambao lazima watokane na orodha ya wachezaji wa akiba wasiozidi tisa (9) walioorodheshwa kwenye fomu ya Orodha ya Timu kwa mchezo husika. Timu itakayobadilisha zaidi ya wachezaji watano (5) itapoteza mchezo husika na kutozwa faini na timu itakayobadili wachezaji wasiozidi watano (5) ila kinyume na utaratibu wa awamu tatu uliowekwa, itatozwa faini. Mabadiliko wakati wa mapumziko hayatahesabika kama awamu.

(33) Timu itakayochelewa kuingia kiwanjani kuanza mchezo au kuchelewa kurejea kiwanjani baada ya muda wa mapumziko kumalizika na kushindwa kutii wito wa mwamuzi itatozwa faini.

(34) Hairuhusiwi kwa wachezaji wa ndani *(field players)* wa timu moja kuvaa jezi zinazotofautiana kwenye mchezo mmoja.

(35) TFF/TPLB inawajibika kufanyia kazi/uchunguzi na kutolea uamuzi tukio lolote la mchezo wa hatari au lisilo la kawaida, la kudhalilisha au la kibaguzi au lililo na mahitaji ya kufanyiwa maamuzi lililotokea wakati wa mchezo au katika shughuli za mchezo wa Ligi Kuu kutokana na taarifa kutoka vyanzo mbalimbali au taarifa ya mchezo ya Kamishna kwa Mazingatio na/au bila kujali hatua zilizochukuliwa na mwamuzi uwanjani.

(36) Kwenye kila mchezo wa Ligi Kuu inawajibika kuwepo kibao maalum cha kubadilishia wachezaji (substitution board) na ubao maalum wa kuonyesha magoli (scoreboard).

(37) Timu zinaruhusiwa kutumia vyumba vya kuvalia *(dressing rooms)* saa 8 (nane) kabla ya mchezo kuanza. Klabu ambayo itakwamisha kwa namna yoyote utekelezaji wa kanuni hii itaadhibiwa kwa kufungiwa kutumia uwanja wake wa nyumbani kwa michezo isiyopungua mitatu (3)

(38) Mchezo wa Ligi Kuu unaweza kuchezwa kwa kuchezeshwa na waamuzi wasiopungua wanne, endapo watakuwa pungufu mchezo huo hautachezwa. Katika Mazingira maalum, mchezo wa Ligi Kuu unaweza kuchezeshwa na Waamuzi sita (6) na kutumika kwa mfumo wowote wa kiteknolojia unaoaminika na uliothibitishwa na TFF.

(39) Endapo itatokea hali ya uwanja kuharibika kutokana na hali ya hewa au matokeo ya hali ya hewa mbaya ambayo haiwezi kurekebishika kwa muda mfupi mchezo unatakiwa kuahirishwa mapema kabla ya saa sita mchana. Katika mazingira maalum ya dharura mchezo unaweza kuahirishwa kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa pande zote zilizothibitishwa na TFF/TPLB.

(40) Mwamuzi wa mchezo ndiye pekee mwenye mamlaka ya kuamua kuhusu uwanja wa kuchezea *(pitch)* kama unafaa na kukidhi vigezo kuchezewa katika hali ya kawaida na dharura ya mvua au madhara katika uwanja yaliyosababishwa na mvua au sababu nyingine.

(41) Hairuhusiwi kwa timu/mchezaji/mwamuzi kuonyesha, kutumia au kuvaa tangazo lolote la biashara *(bila kujali kama lina mgongano na wadhamini wa ligi au la)* au lenye madhumuni maalum kwenye michezo ya Ligi Kuu ambalo halitambuliwi na halijaidhinishwa na TFF/TPLB.

(42) Mchezo unaweza kuchelewa kuanza *(kick off)* kwa mpaka dakika 30 *(thelathini)* endapo itatokea timu kuchelewa kufika uwanjani au kuna taratibu za msingi za mchezo kuchezwa hazijatimizwa na mojawapo ya timu au kwa sababu nyingine zinazokubalika, baada

ya muda huo mchezo utavunjwa. Endapo ni timu imeshindwa kufika itatafsiriwa kushindwa kucheza mchezo wa Ratiba ya Ligi Kuu, na endapo imeshindikana kutatuliwa mapungufu yaliyochelewesha mchezo kuchezwa, timu hiyo itapoteza mchezo husika na kuadhibiwa kwa mazingatio ya Kanuni ya 31.

(43) Mchezaji akifunga magoli matatu katika mchezo mmoja atazawadiwa mpira mmoja miongoni mwa mipira iliyochezewa mchezo huo.

(44) Timu yoyote itakayopewa ushindi katika mchezo wowote wa Ligi Kuu kutokana na makosa ya kikanuni yaliyofanywa na timu pinzani katika mchezo husika yanayosababisha timu kunyang'anywa ushindi au timu pinzani kupewa ushindi, itatunukiwa pointi tatu (3) na magoli matatu (3).

(45) Benchi la wachezaji wa akiba na viongozi zitapangwa kwa kuzingatia timu ya nyumbani kuwa upande wa kushoto na timu ngeni upande wa kulia mwa mwamuzi wa akiba *(4th Official)*. Vyumba vya kubadilishia *(changing rooms)* na sehemu ya kufanyia mazoezi mepesi *(warming up)* vitakuwa upande uleule wa mabenchi kwa timu husika.

(46) Hairuhusiwi kwa Mchezaji, mwamuzi au kiongozi wa timu kuonesha kwa njia yoyote tangazo au ujumbe unaohusiana na dini yoyote au ulio na madhumuni maalum bila idhini ya TFF/TPLB.

(47) Mchezo wowote wa Ligi Kuu lazima uandaliwe kwa ukamilifu wa huduma muhimu za msingi za mchezo kuchezwa kama usalama, huduma ya kwanza, daktari, gari la wagonjwa, waokota mipira na uwanja *(pitch)* uliotayarishwa kwa kufuata sheria za uwanja wa kuchezea.

47.1 Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kwa shughuli zote za maandalizi ya mchezo ikiwemo uuzaji wa tiketi za kuingilia uwanjani kwa njia ya Elektroniki kupitia kwa mzabuni wa klabu aliyeidhinishwa na TFF/TPLB.

47.2 Muongozo wa uuzaji tiketi utatolewa na TFF/TPLB ambapo klabu itawajibika kutafuta mzabuni wake na kuwasilisha taarifa zake kwa TFF/TPLB.

47.3 Maandalizi na ugawaji wa vitambulisho vya msimu, mialiko ya watu maalum (VVIP) na mpangilio wa jukwaa la watu maalum, yatakuwa chini ya mamlaka ya TFF/TPLB.

47.4 Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kuutangaza kila mchezo wake wa Ligi kwa njia mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari.

47.5 Klabu mwenyeji inapaswa kuhakikisha kunakuwa na mfumo wa sauti uwanjani kwa ajili ya kutoa

matangazo muhimu na burudani kwa watazamaji.

(48) Katika mchezo wowote wa Ligi Kuu wakati mchezo ukiwa unachezwa hairuhusiwi kufanyika shughuli nyingine yoyote katika uwanja wa kuchezea na eneo la uwanja la ndani ya uzio wa ndani wa uwanja kama vile muziki, ujenzi na kuendeshwa kwa vyombo vya moto na visivyo vya moto pamoja na kuonekana kwa silaha za moto au nyinginezo katika meneo hayo.

(49) Hairuhusiwi kwa viongozi wa klabu, mashabiki na mtu yeyote asiyekuwa na kazi maalum kuhusiana na mchezo katika eneo la kiwanja *(pitch)* kuwepo eneo la uwanjani ndani kuzunguka kiwanja cha kuchezea *(pitch)*.

(50) Hairuhusiwi kwenye kiwanja au eneo la ndani linalozunguka kiwanja (pitch area) chochote kinachotumika kwa michezo ya Ligi Kuu uwepo wa Matangazo ya Biashara (au mengineyo), Dini, Siasa au yenye madhumuni maalum wakati wa mchezo ambayo hayajaruhusiwa na TFF/TPLB. Timu mwenyeji itawajibika kwa uvunjifu huu kwenye uwanja wake wa nyumbani katika mchezo wake husika.

(51) Hairuhusiwi kwa kocha/kiongozi yeyote wa timu aliyetolewa mchezoni na mwamuzi kujihusisha/kuendelea na kazi zake kwenye mchezo huo kwa siku hiyo na wakati wote wa adhabu dhidi yake kwa mujibu wa kanuni hizi.

(52) Mchezo wowote wa Ligi Kuu unatakiwa kuanza (kickoff) kati ya saa 8.00 (nane) mchana na saa 4.00 (nne) usiku. Katika Mazingira maalum, mchezo unaweza kupangiwa muda mwingine na TPLB kwa Mazingatio ya mashauriano na Kamishna au Msimamizi wa Kituo.

(53) Mchezo unaweza kusitishwa kwa muda na kisha kuendelea endapo kumetokea jambo lisilo la kawaida au mabadiliko makubwa ya hali ya hewa yanayoweza kuathiri usalama/afya za watu au kuathiri mchezo wenyewe.

(54) Klabu zinaweza kujulishwa kuhusu michezo yao itakayoonyeshwa moja kwa moja kwenye televisheni (live tv broadcasting). Klabu zitawajibika kukidhi mahitaji yote ya taratibu za kufanikisha maandalizi na mchezo husika.

(55) Klabu ya Ligi Kuu italazimika kuteua na kuitangaza angalau siku moja (1) ndani ya kipindi cha miezi miwili (2), ambayo itakuwa maalum kwa ajili ya wanahabari kufanya mahojiano na wachezaji, maafisa wa ufundi na viongozi wa klabu hiyo kwa lengo la kuitangaza klabu na Ligi kwa ujumla.

(56) Kutakuwa na siku maalum ya mdhamini mwenye haki ya matangazo ya runinga kutangaza matukio ya klabu moja ya Ligi Kuu kuanzia maandalizi ya mwisho ya mchezo (mazoezi), chakula cha mchana, kuwasili uwanjani pamoja na baadhi ya matukio ya chumba cha kuvalia kwa lengo la kuitangaza klabu na Ligi

kwa ujumla. Klabu husika itajulishwa kuhusu siku hiyo.

(57) Kutakuwa na mkutano wa waandishi wa Habari siku moja kabla ya mchezo ambapo Kocha Mkuu na Nahodha au mchezaji mwenye Ushawishi ndani ya Timu yake watazungumza katika mkutano huo.

(58) Klabu ina wajibu wa kushirikiana na mdhamini wa matangazo ya televisheni na TPLB, ikiwemo kupata picha za wachezaji na benchi la ufundi kwa ajili ya maandalizi ya mechi zao.

(59) Endapo Klabu yoyote ya Ligi Kuu inahitaji kuchukua Kumbukumbu za kurekodi video na Picha kuhusiana na mechi yake yoyote ya Ligi Kuu au inayohusiana na uwepo wake kwenye Ligi Kuu inaruhusiwa kufanya hivyo kwa kutoa Taarifa na Kukubaliwa na TPLB/TFF ambapo kumbukumbu hizo hazitaruhusiwa kutumika au kuhusika/kuhusishwa kibiashara kwa namna yoyote na klabu husika au mshirika wake.

(60) TFF/TPLB inaweza kutoa maelekezo ya mchezo wowote wa Ligi Kuu kurekodiwa au kuoneshwa moja kwa moja (live) na televisheni katika utaratibu na mazingira itakavyoona inafaa kwa maslahi ya mpira wa miguu.

(61) TPLB itachukua hatua kwa ukiukwaji wowote wa Taratibu za Mchezo kama zilivyoainishwa kwenye kanuni ya 17 kwa kutoa Onyo kali au karipio au kutoza faini kuanzia shilingi milioni tano (5,000,000/-) mpaka shilingi milioni kumi (10,000,000/-) na/au kufungia michezo isiyozidi mitatu (3) au kipindi kisichozidi miezi mitatu (3). Faini kwa makosa yanayojirudia itatozwa kati ya shilingi milioni kumi na moja (11,000,000/-) na shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa mchezaji, kiongozi au timu.

(62) TPLB itachukua hatua kwa ukiukwaji wowote wa taratibu za mchezo kama zilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 17 kwa kutoa onyo kali au karipio au kutoza faini kuanzia shilingi milioni kumi (10,000,000/-) na/au kufungia michezo isiyozidi mitatu (3) au kipindi kisichozidi miezi mitatu (3). Faini kwa makosa yanayojirudia itatozwa kati ya shilingi milioni kumi na moja (11,000,000/-) na shilingi milioni arobaini (40,000,000/-) kwa mchezaji, kiongozi au klabu.

## Kanuni : 18 Michezo ya Kirafiki

(1) Timu ya Ligi Kuu inayotaka kucheza mchezo wa kirafiki katika kipindi ligi ikiendelea itawajibika kuitaarifu TFF angalau saa arobaini na nane (48) kuhusu mchezo huo kabla ya kuchezwa.

(2) Hairuhusiwi kuchezwa mchezo wowote wa kirafiki utakaohusisha klabu nyingine ya Ligi Kuu katika siku ambayo kuna mchezo wa Ligi Kuu katika kituo/Mkoa husika bila kupata idhini ya TFF/TPLB.

(3) Mchezo wowote wa kirafiki utakaohusisha timu ya Ligi Kuu ni

lazima utolewe taarifa kwa TFF/TPLB au/na FA(M), itakayofanya maandalizi yote muhimu kwa mchezo kuchezwa na kufuatwa kwa taratibu zote kwa kiwango cha mchezo wa Ligi Kuu.

(4) Makubaliano yoyote kuhusiana na mchezo wa kirafiki unaohusisha timu ya Ligi Kuu lazima yafanywe kwa maandishi na mwandaaji wa mchezo huo. (TFF/FA(M) TFF/TPLB au/na FA(M) itasimamia makubaliano hayo.

(5) Masharti yoyote mengine kuhusiana na mchezo wa kirafiki unaohusisha timu ya Ligi Kuu ni lazima yaidhinishwe na TFF kwa michezo inayohusisha timu kutoka nje ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kupitia maombi yote ya mchezo husika.

(6) Timu yoyote ya Ligi Kuu inapotaka kucheza au kwenda nje ya Tanzania kwa shughuli za mpira wa miguu itawajibika kuomba kibali kwa TFF, maombi ya kibali hicho yatumwe siku kumi na nne (14) kabla ya siku ya kuondoka.

(7) Timu yoyote ya Ligi Kuu hairuhusiwi kucheza mchezo wowote wa kirafiki na timu kutoka nje ya Tanzania bila kuwa na kibali cha TFF.

(8) Mwanachama wa TFF au Wakala wa Mechi wa FIFA anayetaka kuandaa mchezo wowote ukihusisha timu za kimataifa na timu za Ligi Kuu anawajibika kutuma maombi kwa TFF siku kumi na nne (14) kabla ya siku ya tukio yakianisha madhumuni ya mchezo huo. TFF itafanya uamuzi juu ya maombi hayo.

(9) Taratibu za Jumla kuhusu Michezo ya Kirafiki ni kama zitavyosomeka kwenye Kanuni za TFF kuhusu Mashindano Maalum/Wadau.

## Kanuni : 19 Ngao ya Jamii

(1) Kutakuwa na shindano la Ngao ya Jamii kama Tukio la Ufunguzi wa Msimu wa Mashindano wa TFF kabla ya kuanza kwa ratiba ya Ligi Kuu na Mashindano mengine kwa kila msimu kwa madhumuni ya kuutumia mchezo wa mpira wa miguu kupitia Mashindano ya Mpira wa Miguu na wadau wake kuchangia shughuli za kibinadamu kusaidia jamii. Shindano hili msingi wake mkuu ni kurejesha kwa jamii kwa uchangiaji hivyo kila mdau mhusika anawajibika kujielekeza kuchangia.

(2) Shindano maalum la ufunguzi wa Ligi (Ngao ya Jamii) litashirikisha timu zilizoshika nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa Ligi na Timu Bingwa wa Kombe la Shirikisho. Endapo Bingwa wa Kombe la Shirikisho atakuwa miongoni mwa washindi wa nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, timu iliyoshika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi itashiriki shindano hilo.

2.1 Shindano la Ngao ya Jamii litachezwa katika uwanja/viwanja vitakavyotangazwa na TFF kwa hatua mbili za Nusu Fainali na Fainali.

2.2 Hatua ya Nusu Fainali itakuwa na michezo miwili, mchezo wa kwanza utakaoshirikisha bingwa wa Ligi Kuu dhidi ya timu iliyoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu na mchezo wa pili utashirikisha timu iliyoshika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu dhidi ya bingwa wa Kombe la Shirikisho/timu iliyoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

2.3 Timu zitakazopata ushindi kwenye hatua ya Nusu Fainali zitacheza mchezo wa Fainali, timu zitakazopoteza michezo ya Nusu Fainali zitacheza mchezo maalum wa kutafuta mshindi wa tatu na wa nne.

2.4 Timu shiriki katika Shindano la Ngao ya Jamii inatakiwa kutumia wachezaji wake wa kikosi cha kwanza (timu A).

(3) Katika mazingira ya ratiba za FIFA, CAF na CECAFA kubana kalenda ya matukio ya TFF, TFF itaandaa mchezo wa Ngao ya Jamii (badala ya Shindano la Ngao ya Jamii), kama tukio la ufunguzi wa msimu wa mashindano ya TFF kabla ya kuanza kwa ratiba ya Ligi Kuu na mashindano mengine kwa kila msimu kwa madhumuni ya kuutumia mchezo wa mpira wa miguu kupitia mashindano ya mpira wa miguu na wadau wake kuchangia shughuli za kibinadamu kusaidia jamii. Mchezo huu msingi wake mkuu ni kurejesha kwa jamii kwa uchangiaji hivyo kila mdau mhusika anawajibika kujielekeza kuchangia.

3.1 Mchezo maalum wa ufunguzi wa Ligi (Ngao ya Jamii) utahusisha Timu Bingwa wa Ligi Kuu na timu bingwa wa Kombe la Shirikisho. Endapo Bingwa wa Kombe la Shirikisho atakuwa bingwa wa Ligi Kuu, timu iliyoshika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu itashiriki mchezo huo.

3.2 mchezo wa Ngao ya Jamii utachezwa katika uwanja utakaotangazwa na TFF.

(4) Mshindi katika mchezo wa Shindano la Ngao ya Jamii itakuwa ni timu itakayopata goli/magoli zaidi ya timu mpinzani wake katika muda wa dakika tisini (90) za mchezo, endapo hatopatikana mshindi katika muda huo sheria ya penalti itatumika kumpata Mshindi wa mchezo wa Shindano la Ngao ya Jamii.

(5) Mgawanyo wa mapato katika mchezo wa Ngao ya Jamii utazingatia kwanza kutolewa asilimia kumi na nane za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT 18%), asilimia tatu (3%) Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na gharama za tiketi ambapo Baki ya pato itagawanywa asilimia thelathini (30%) Mfuko wa Jamii, asilimia kumi na tano (15%) Uwanja, asilimia kumi na tano (15%) kila klabu iliyoshiriki, asilimia sita (6%) TFF, asilimia saba (7%) gharama za mchezo, asilimia tano (5%) TPLB, asilimia tano (5%) Mfuko wa Maendeleo ya Mpira wa Miguu (FDF), FA(M) asilimia mbili (2%)

(6) Mapato mengine yanayotokana na mchezo wa Ngao ya Jamii

yataamuliwa na TFF kutegemea msingi wa Mapato husika na Madhumuni yaliyokusudiwa.

(7) Walengwa Wanufaika wa mapato ya Mfuko wa Jamii watatambulishwa mapema kabla ya shindano la Ngao ya Jamii kuchezwa.

(8) TFF itaamua na kupanga Uwanja, tarehe na muda kwa mchezo wa Shindano la Ngao ya Jamii na taratibu nyingine kwa msimu husika.

(9) Vitendo vya utovu wa nidhamu na ukiukwaji mwingine wa taratibu za mchezo katika mchezo wa Ngao ya Jamii utachukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni hizi ambapo uamuzi wowote dhidi yake utakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Ligi Kuu, na mechi za ligi zinazohusisha timu husika.

## Kanuni : 20 Matumizi ya Teknolojia ya Video Support System (VS)

(1) Katika kuondoa utata wa maamuzi kutakuwa na matumizi ya teknolojia ya Video Support System (VS) ambayo itatumiwa na mwamuzi wa mchezo ili kujiridhisha na tukio ambalo maamuzi yake yatakuwa yamelalamikiwa na timu wakati wa mchezo husika.

(2) Maamuzi ambayo yatahitaji matumizi ya VS ni yenye utata juu ya maamuzi yafuatayo: goli au siyo goli, penati au siyo penati, kosa linastahili kadi nyekundu ya moja kwa moja au kadi ya pili ya njano, kumtaambua mchezaji mwenye hatia ya kosa endapo kuwakuwa na malalamiko kuwa mwamuzi amemwadhibu mchezaji asiye na hatia.

(3) Matumizi ya VS yatafanywa na mwamuzi pale tu ambapo timu inayodhani itathirika na maamuzi hayo itaomba mwamuzi ajiridhishe kuhusu kufanyika kwa tukio husika kwa kurejea picha za tukio hilo kwenye VS.

(4) Kocha mkuu wa timu au kiongozi mwingine wa juu kwenye benchi la ufundi la timu inayolalamika ndio watakaokuwa na haki ya kuwasilisha maombi ya marejeo ya picha katika VS kwa kuwasiliana na mwamuzi wa akiba (fourth official).

4.1 Iwapo mchezaji atakuwa na mtazamo kuwa tukio linahitaji marejeo katika VS, mchezaji atawajibika kuwasiliana kwa ishara na Kocha Mkuu au kiongozi mwingine wa benchi la ufundi ili Kocha au kiongozi huyo aweze kuwasilisha lalamiko hilo kwa mwamuzi wa akiba.

4.2 Itakuwa ni marufuku kwa mchezaji yeyote kumkabili mwamuzi kwa nia ya kuomba au kushinikiza marejeo ya tukio kwenye VS. Mchezaji atakayekiuka masharti ya kifungu hiki ataadhibiwa kwa mujibu wa kanuni ya 17:62.

(5) Malalamiko na maombi ya marejeo (VS review) lazima yafanywe haraka iwezekanavyo ndani ya dakika moja tangu tukio hilo litokee au kabla mwamuzi hajaruhusu mchezo kuendelea baada

ya tukio husika kufanyika. Malalamiko yakichelewa kuwasilishwa, mwamuzi msaidizi hatawasilisha lalamiko kwa mwamuzi wa mchezo. Mwamuzi wa mchezo atakuwa na wajibu wa kupuuza wasilisho la malalamiko yaliyowasilishwa nje ya muda na mwamuzi hatasimamisha mchezo au kubadili maamuzi ya awali kwa namna yoyote.

(6) Iwapo katika mazingira yoyote mwamuzi atakuwa na mashaka na tukio lolote ambalo halijalalamikiwa, anaweza kurejea tukio hilo kwenye VS ili kujiridhisha ufanyikaji wa tukio ili achukue hatua stahiki kuhusu tukio hilo.

(7) Baada ya kupokea malalamiko, mwamuzi msaidizi atawasiliana na mwamuzi wa mchezo (main referee). Iwapo mchezo ulikuwa unaendelea baada ya tukio linalolalamikiwa, mwamuzi atasimamisha mchezo na kwenda kujiridhisha katika VS juu ya uhalali/ukweli wa maamuzi ya tukio husika katika eneo uliposimikwa mtambo wa VS.

(8) Wakati wa marejeo ya tukio katika VS, mwamuzi atasaidiwa na mafisa wa mfumo (floor manager wa mrusha matangazo akishirikiana na afisa wa TFF/TPLB watakaokuwepo uwanjani kumsaidia mwamuzi kurejesha nyuma picha za tukio hilo (replay) kwa muonekano wa pande mbalimbali (different camera angles) kwa kadri inavyowezekana kwa wakati huo.

(9) Maamuzi ya awali ya mwamuzi hayatabadilika mpaka pale ambapo itathibitika wazi na pasipokuwa na utata wowote kuwa maamuzi ya awali yalikuwa na makosa. Iwapo marejeo ya picha kwenye VS bado yanaacha utata kuhusu uhakika na uhalisia wa tukio linalolalamikiwa, maamuzi ya awali yatabaki kama yalivyo.

(10) Ili kuondoa utata wa uhalali wa goli lililofungwa, kila baada ya goli kufungwa, mwamuzi wa akiba (fourth official) atafanya rejea (review) ya tukio hilo kwenye VS na kuwasiliana na mwamuzi wa mchezo endapo kuna kosa lilitendeka kabla ya goli kufungwa. Iwapo kutakuwa na mgongano wa misimamo kati ya alichokiona mwamuzi na taarifa ya mwamuzi msaidizi, mwamuzi wa mchezo ataondoa utata kwa kufanya marejeo yeye mwenyewe ili kujiridhisha na maamuzi yake yatakuwa ya mwisho.

(11) Iwapo mfumo wa VS utakuwa na hitilafu, mchezo utaendelea bila uwepo na matumizi ya VS. Makocha na manahodha wa timu husika watajulishwa kuhusiana na hitilafu hiyo kabla ya kuanza kwa mchezo au baada ya kutokea kwa hitilafu.

# SURA: VI

## TIBA NA BIMA



## SURA : VI TIBA NA BIMA

### Kanuni : 21 Huduma ya Kwanza

(1) Klabu Mwenyeji/FA(M)/Msimamizi wa Kituo ni lazima wahakikishe kuwa katika mchezo wowote wa Ligi Kuu panakuwepo huduma ya kwanza maalum na yenye vifaa na sare, gari la wagonjwa *(Ambulance)* lililo na vifaa tiba stahili na Daktari kamili mwenye ujuzi.

(2) Huduma ya Gari la Wagonjwa *(Ambulance)*, huduma ya kwanza na Daktari zinahitajika uwanjani tangu muda wa kufungua mageti kuingiza watazamaji uwanjani mpaka saa moja baada ya mchezo kumalizika.

(3) Kila uwanja kunapochezwa michezo ya Ligi Kuu kunahitajika chumba maalum kwa ajili ya huduma za tiba na matibabu.


(4) Ikitokea mchezo umeshindwa kuchezwa kutokana na sababu ya kutotimiza idadi ya wachezaji wanaohitajika kikanuni kutokana na sababu za kiafya zilizosababishwa na magonjwa ya mlipuko, timu husika itakuwa imepoteza mchezo na timu shindani itapewa ushindi wa pointi tatu (3) na mabao matatu (3).

### Kanuni : 22 Bima

Kila klabu ina wajibu wa kuwawekea wachezaji wake na maofisa wa benchi la ufundi bima ya matibabu na fidia kutokana na ajali michezoni, na muda wa bima usipungue kipindi cha mwaka mmoja. Klabu itakayokiuka kanuni hii itakuwa imepoteza sifa ya kuwa klabu ya Ligi Kuu na usajili wa wachezaji wa timu yake hautathibitishwa na haitashirikishwa katika Ligi Kuu. Klabu zinaelekezwa kuwasilisha Hati ya Bima (Cover Note) kwa ajili ya uhakiki katika Mamlaka husika.

# SURA: VII

## MALALAMIKO NA RUFAA



## SURA : VII MALALAMIKO NA RUFAA

### Kanuni : 23 Malalamiko

(1) Katika mchezo wowote wa Ligi Kuu inapotokea klabu kutoridhika au kuwa na mahitaji ya kupinga jambo lolote inawajibika kuwasilisha malalamiko kwa Bodi ya Ligi Kuu (TPLB) itakayosikiliza na kuyatolea maamuzi au kupelekwa kwenye Kamati nyingine husika ya TFF kwa maamuzi.

(2) Upande wowote ambao haujaridhika na maamuzi juu ya malalamiko yaliyotolewa unaweza kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyo na mamlaka kutegemea chombo kilichofanya maamuzi ya awali na kanuni zinahusu maamuzi hayo.

(3) TFF/TPLB inaweza kupeleka jambo lolote kuhusiana na Ligi Kuu kwenye chombo husika kujadiliwa na kuamuliwa bila ya kujali kulalamikiwa au la.

(4) Wahusika katika shauri lolote litakalosikilizwa na Kamati yoyote ya maamuzi wanaohitajika kuhudhuria kikao hicho watawajibika kujulishwa na TFF kuhusu mahali, siku na muda wa kikao hicho katika kipindi kisichopungua siku tano (5) kabla ya kikao hicho. Yeyote atakayeitwa atahudhuria kwa gharama zake mwenyewe.

### Kanuni : 24 Utaratibu wa Malalamiko

(1) Malalamiko yoyote kuhusiana na mchezo yawasilishwe kwa maandishi kwa Kamishna wa mchezo au ofisi ya Bodi ya Ligi Kuu sio zaidi ya saa 72 *(sabini na mbili)* baada ya mchezo kumalizika.

(2) Kamishna wa mchezo atawasilisha kwa Bodi ya Ligi Kuu sio zaidi ya saa ishirini na nne (24) tangu kupokea malalamiko hayo.

(3) Malalamiko yoyote yatakayowasilishwa yatashughulikiwa ndani ya siku 14 *(kumi na nne)* tangu kuwasilishwa, katika hali ya upekee malalamiko yanaweza kusikilizwa katika muda mfupi zaidi au mrefu zaidi.

(4) Malalamiko yatakayowasilishwa baada ya muda uliowekwa hayatasikilizwa. Endapo mlalamikaji atawasilisha malalamiko yatakayobainika kutokuwa na msingi atatozwa faini.

### Kanuni : 25 Pingamizi katika Mchezo

(1) Malalamiko yoyote kabla au wakati wa mchezo *(pingamizi)* yatolewe kwa maandishi yakiainisha tuhuma na msingi wake na yawasilishwe kwa Kamishna mara baada ya ukaguzi wa wachezaji mpaka kabla ya mchezo kumalizika. Pingamizi katika Mchezo litapokelewa na Kamishina wa Mchezo na Kusainiwa na Meneja au Kocha wa Timu iliyolalamikiwa na Mwamuzi wa Mchezo husika

(2) Endapo malalamiko yanahusisha uhalali wa mchezaji kucheza mchezo husika, timu inayolalamikiwa inaweza kumuondoa kwenye orodha yake ya wachezaji wa siku hiyo mchezaji aliyewekewa pingamizi kabla ya mchezo kuanza ikiwa inakubaliana/kuheshimu pingamizi hilo. Timu itakayomuondoa mchezaji katika hali hii itatozwa faini ya shilingi laki tano (500,000/-).

(3) Malalamiko yatasikilizwa na kutolewa majibu ndani ya siku kumi na nne (14).

## Kanuni : 26 Rufaa

(1) Upande wowote unaopinga maamuzi ya malalamiko au mengine yaliyofanywa na chombo husika unaweza kukata rufaa kwa kamati ya rufaa husika endapo utaratibu wa chombo na kanuni zilizofanya maamuzi hayo vinaruhusu kufanya hivyo.

(2) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya TFF ndio chombo cha juu kwa TFF cha kusikiliza Rufaa zinazotokana na maamuzi ya Kamati ya Nidhamu ya TFF.

(3) Maamuzi ya Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya TFF yatakuwa ya mwisho. Endapo mrufani au mrufaniwa hakuridhika na maamuzi ya Kamati hii apeleke shauri lake Mahakama ya Usuluhishi wa Mashauri ya Michezo Ulimwenguni (CAS).

(4) Ni marufuku kupeleka malalamiko yoyote dhidi ya TFF/TPLB kuhusiana na uendeshaji wa Ligi Kuu katika mahakama za kawaida za sheria. Klabu, mdau au mtu yeyote atakayepeleka malalamiko yake katika mahakama za sheria atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa Kanuni za Maadili za TFF.

(5) Malalamiko au jambo lolote litakaloamuliwa na Kamati nyingine za TFF, Rufaa dhidi yake itafuata utaratibu wa kamati hizo kwa mujibu wa utaratibu wa TFF na uamuzi wake utakuwa wa mwisho endapo tu jambo lililoamuliwa linaweza kukatiwa rufaa kwa mujibu wa kanuni hizi na za vyombo hivyo.

(6) Kamati ya Rufaa ya TFF itasikiliza rufaa kupinga maamuzi yoyote ya Kamati ya Nidhamu ya TFF au Maamuzi ya Vyombo vya Bodi ya Ligi Kuu ambayo yanaweza kukatiwa rufaa.

(7) Wahusika wote wanaohitajika kwenye shauri la rufaa watajulishwa na TFF siku, mahali na muda angalau siku tano (5) kabla ya siku ya shauri na watahudhuria kwa gharama zao wenyewe.

(8) Rufaa itasikilizwa ndani ya siku saba (7) tangu ilipowasilishwa.

## Kanuni : 27 Utaratibu wa Rufaa

(1) Rufaa ya kupinga maamuzi ya Kamati ya Nidhamu iwasilishwe kwa maandishi kwenye ofisi za TFF sio zaidi ya siku tano (5) za kazi baada ya kupata maamuzi ya Kamati ya Nidhamu na iwe imeambatanishwa na ada ya rufaa pamoja na vielelezo vyote vya shauri hilo.

(2) Mrufani anaweza kuomba kwa TFF uwasilishwaji wa vielelezo kwenye Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ambavyo hana uwezo wa kuwa navyo na anaweza pia kuwasilisha vielelezo vya ziada kukazia malalamiko yake wakati shauri lake linasikilizwa.

(3) Mrufaniwa anayo haki ya kupata nakala ya rufaa dhidi yake baada tu ya rufani kuwasilishwa TFF.

(4) Rufaa yoyote itakayowasilishwa bila ya vielelezo au ambayo haijalipiwa ada haitasikilizwa.

(5) Rufaa yoyote itakayowasilishwa baada ya muda uliowekwa chini ya kanuni hii, haitasikilizwa na ada ya rufaa haitarudishwa kwa mrufani.

(6) Ada ya rufaa kwa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ni shilingi milioni moja (1,000,000/-)

## Kanuni : 28 Vyombo vya Maamuzi

(1) Vyombo vya Maamuzi vya TFF na TPLB vitashughulikia masuala na mashauri mbalimbali kuhusiana na Ligi Kuu na kufanya maamuzi kwa misingi ya kanuni na mwongozo wa Katiba ya TFF. Vyombo vya maamuzi vitatumia kanuni hizi za Ligi Kuu, Kanuni nyingine za TFF, CAF na FIFA katika kufanya maamuzi yake.

(2) Mhusika yeyote wa shauri linalosikilizwa na kuamuliwa na miongoni mwa vyombo vya maamuzi vya TFF atawajibika kufuata taratibu za vyombo hivyo bila ya kuathiri masharti ya kanuni hizi inayoongoza usikilizwaji na maamuzi ya shauri husika.

(3) Shauri lolote linalosikilizwa na chombo cha haki cha TFF ni lazima liwekewe utaratibu wa mashtaka katika mfumo wa kimahakama katika kuzingatia haki za mlalamikaji na mlalamikiwa.

(4) Shauri lolote linalosikilizwa na kuamuliwa na chombo cha TFF kilicho na mamlaka ya mwisho wa usikilizaji na maamuzi ya shauri hilo linaweza kuombewa marejeo (review) ya kusikilizwa endapo kuna upande wowote haujaridhika na maamuzi. Uamuzi wa marejeo hayo utakuwa wa mwisho. Ada ya marejeo (review) ni shilingi milioni mbili (2,000,000/-).

(5) TFF inaweza kuelekeza chombo chake chochote cha maamuzi kushughulikia jambo kuhusiana na Ligi Kuu kutokana na mahitaji au dharura kuhusiana na jambo husika.

(6) Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ligi ya TPLB itashughulikia na kufanya maamuzi kwa masuala yote ya kiuendeshaji ambayo maamuzi yake hayatakatiwa rufaa kwenye chombo kingine cha maamuzi cha TFF kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu.

(7) TFF/TPLB inaweza kutoa adhabu zaidi kwa kutoza faini zaidi au adhabu nyingine yoyote zaidi, au kuongeza adhabu yoyote iliyotolewa kwa mchezaji, kiongozi, mwamuzi au timu kutokana na kuthibitika ukiukwaji zaidi wa taratibu au makosa

yanayojirudia katika msimu mmoja au

kutegemea uzito na mazingira ya ufanyaji kosa au mwendelezo wa kutenda kosa.

(8) TFF/TPLB itatoza faini kwa ukiukwaji mwingine wowote wa kanuni na taratibu ambao haujaainishwa wazi katika kanuni hizi ulio na mahitaji ya adhabu ya faini kwa kati ya shilingi laki mbili (200,000 /-) na shilingi milioni tano (5,000,000/-).

# SURA: VIII

## MAPATO NA GHARAMA



## SURA : VIII MAPATO NA GHARAMA

### Kanuni : 29 Mgawanyo wa Mapato

(1) Mgawanyo wa mapato ya mlangoni *(gate collection)* utafanywa kwa kuzingatia kwanza kutoa asilimia kumi na nane ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (18% VAT), Baraza la Michezo la Taifa (BMT) asilimia tatu (3%) (kutoka baki ya pato) na gharama za tiketi kwa mchezo husika. Baki ya pato itagawanywa kwa Timu mwenyeji asilimia sitini (60%), TPLB asilimia nane (8%), gharama za mchezo asilimia saba (7%), mamlaka ya Uwanja asilimia kumi na tano (15%), TFF asilimia nne (4%) na FA(M) mwenyeji asilimia sita (6%) Mgawanyo wa Mapato utafanywa kwenye Fomu Maalum itakayotolewa na TFF kwa Madhumuni hayo.

(2) Endapo itatokea kuwa Gawio la Gharama ya Uwanja litakuwa ni kwa maelewano maalum na si kwa asilimia, Timu mwenyeji itawajibika kutimiza matakwa ya Masharti ya uwanja ili uweze kuchezewa na sehemu ya mgao wa Uwanja ya asilimia 15 itachukuliwa na timu mwenyeji.

(3) Endapo timu itahamia uwanja wa Mkoa mwingine kama uwanja wake wa nyumbani mgao wa mapato ya FA(M) ya asilimia sita (6%) itagawanywa kwa FA(M) inapotoka timu kupata (nusu) asilimia tatu (3%) na FA(M) unapochezwa mchezo pia (nusu) asilimia tatu (3%).

(4) Msimamizi wa Kituo atawasilisha taarifa ya mapato na fedha za mchezo husika kwa TFF na TPLB katika muda usiozidi saa 48 (arobaini na nane). Kiongozi au msimamizi atakayeshindwa kuwasilisha atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Kanuni za TFF.

(5) TFF/TPLB ndiyo itakayosimamia na kuratibu zoezi la kumpata mzabuni wa kuuza tiketi kwa ajili ya mashindano yote yaliyo chini yake.

### Kanuni : 30 Gharama za Mchezo

(1) Asilimia saba (7%) ya Gharama za Mchezo itatumika kulipia gharama mbalimbali za huduma zitakazoalikwa na kutolewa kufanikisha mchezo husika. Gharama za Mchezo zigawanywe kutumia Fomu Maalum inayotolewa na TPLB.

(2) TPLB/TFF itatoa waraka mwanzoni mwa msimu utakaofafanua viwango vya malipo ya maafisa wa mchezo na Utaratibu wa Malipo.

(3) Gharama zote za Msimamizi wa Kituo, Kamishna, Mratibu wa Mchezo (GC), Mtathimini Waamuzi na Waamuzi zitalipwa na TPLB. Gharama za usafiri ni kwa usafiri wa treni daraja la pili, basi au meli.

(4) Iwapo gharama halisi ni pungufu ya asilimia saba (7%) zilizokatwa kama Gharama za Mchezo, fedha zitakazobaki zitagawanywa

asilimia hamsini (50%) Bodi ya Ligi Kuu na klabu mwenyeji asilimia hamsini (50%) nyingine.

(5) Msimamizi wa Kituo atawajibika na usimamizi wa Gharama za Mchezo, atathibitisha uhalali na usahihi wa Malipo kwa kutumia Fomu Maalum ya TPLB kwa ajili ya Gharama za Mchezo na kusaini kwa niaba ya TPLB na Mwakilishi wa Klabu Mwenyeji atathibitisha na kusaini kwa upande wa klabu.

(6) Malipo yatalipwa kwa mifumo ya kibenki kama kanuni za Fedha zinavyoelekeza na/au vinginevyo katika mazingira maalum kama itakavyoelekezwa na TPLB.

# SURA: IX
## YASIYOTARAJIWA



## SURA : IX YASIYOTARAJIWA

### Kanuni : 31 Kujitoa

(1) Endapo Klabu yoyote ina nia ya kujitoa katika Ligi kwa sababu zozote zile za msingi ni lazima itoe taarifa ya maandishi kwa TFF ikieleza sababu zinazoilazimisha kujitoa siku 30 (thelathini) kabla ya Ligi kuanza.

(2) Endapo TFF imekubali kujitoa kwa klabu iliyoomba, klabu nyingine ambayo awali ilikuwemo katika daraja hilo lakini ilishuka kwa mujibu wa msimamo wa Ligi, itarudishwa kuziba pengo hilo. Klabu hiyo ni ile iliyo katika nafasi ya juu kuliko klabu nyingine zote zilizoshuka daraja katika msimu huo.

(3) Endapo klabu iliyojitoa ni miongoni mwa klabu zilizopanda daraja, klabu nyingine iliyokuwa kwenye nafasi inayofuatia kwa klabu zilizopanda/iliyopanda daraja itapandishwa kuchukua nafasi hiyo.

(4) Klabu yoyote itakayojitoa/itakayoondolewa kwenye Ligi Kuu baada ya Ligi kuanza au kushindwa kucheza mchezo mmoja wa ratiba ya Ligi Kuu katika msimu itakabiliwa na adhabu zifuatazo:

4.1 Itashushwa daraja na kufungiwa kucheza Ligi kwa misimu miwili (2). TPLB/TFF pia inaweza kuichukulia hatua zaidi klabu hiyo/viongozi au wachezaji iwapo itathibitika kuwa imejitoa kwa madhumuni ya kuhujumu msimamo wa Ligi au hujuma nyingine yoyote.

4.2 Iwapo zitajitoa, kuondolewa au kushindwa kumaliza Ligi kwa sababu yoyote ile timu zaidi ya idadi ya timu za kushuka daraja kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu timu zote hizo zitashuka daraja (kanuni 30:4.1) na timu zaidi zitapanda kutoka Ligi Daraja la Kwanza (Championship) ili kujaza nafasi na idadi ya timu za Ligi Kuu kuendelea kuwa ilivyokusudiwa.

4.3 Matokeo ya michezo yote iliyowahi kuchezwa yatafutwa endapo idadi ya michezo hiyo kwa timu husika haijafikia zaidi ya nusu ya michezo yake katika Ligi Kuu na endapo itakuwa zaidi ya nusu, timu ambazo hazijacheza na timu iliyojitoa au kuondolewa zitapewa ushindi kwa michezo hiyo. Timu husika itaendelea kusalia kwenye Msimamo wa Ligi katika mazigira yoyote bila ya kuathiri adhabu zaidi kwa timu husika kwa mujibu wa kanuni hizi.

4.4 Magoli yaliyofungwa na wachezaji wa timu iliyojitoa katika Ligi yatafutwa na hivyo wachezaji wake hawataweza kushindana katika ufungaji bora hata kama walifunga magoli mengi. Lakini magoli yaliyofungwa na wachezaji wa timu pinzani dhidi ya timu iliyojitoa kwenye ligi hayatafutwa, yataendelea kuonekana katika idadi ya magoli yaliyofungwa na wachezaji hao lakini hayataonekana katika idadi ya magoli yaliyofungwa na klabu zao.

4.5 Itapoteza haki zake zote stahili kwa timu za Ligi Kuu na itawajibika kurejesha stahili yoyote iliyokwishachukua kabla ya kujitoa endapo itaamriwa kufanya hivyo kutokana na mazingira ya kujitoa kwake

## Kanuni : 32 Kutofika Uwanjani

(1) Timu yoyote itakayokosa kufika uwanjani bila ya sababu za msingi zinazokubalika kwa TPLB na/au kusababisha mchezo usifanyike itakabiliwa na adhabu zifuatazo:

1.1 Itapoteza mchezo huo na timu pinzani itapewa ushindi wa pointi tatu (3) na magoli matatu (3).

1.2 Kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000/-) ambapo 50% ya faini itachukuliwa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania na 50% italipwa kwa timu pinzani.

1.3 Kulipa fidia ya maandalizi/uharibifu wowote unaoweza kujitokeza.

1.4 Kupokwa alama 3 (tatu) katika msimamo wa Ligi na Mwenyekiti au Rais wa Klabu kufungiwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja (1) hadi mitano (5).

1.4.1 Endapo timu itakuwa na alama pungufu ya tatu (3), itakuwa na alama hasi kwa kiasi kinachopungua kwenye msimamo wa Ligi.

1.4.2 Endapo timu itamaliza msimu wa Ligi ikiwa na alama hasi, itaanza na alama hizo hasi katika msimamo wa Ligi kwenye msimu unaofuata wa Ligi ya hadhi yake.

1.5 Kwa michezo ya hatua ya mtoano, timu iliyokosa kufika uwanjani katika mchezo wa mkondo mmoja, itakuwa imepoteza hadhi ya kuingia hatua inayofuata bila kujali matokeo ya mchezo wa mkondo mwingine.

1.6 Itapoteza haki ya kuchukua gawio lake la mapato ya mchezo huo.

1.7 Kiongozi mwingine yeyote atakayebainika kuwa alishiriki, alishawishi au alikuwa chanzo au sababu ya timu kutotokea uwanjani bila ya sababu za msingi atafungiwa kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12).

1.8 Inaweza kukabiliwa na adhabu zaidi kama ambavyo TFF/TPLB itahitaji kuchukua hatua zaidi kadiri itavyoona inafaa.

1.9 Timu ya Ligi Kuu itakayoshindwa kufika kituoni katika michezo mitatu (3) ya Ligi bila sababu za msingi zinazokubalika na TFF/TPLB itakuwa imejiondoa kushiriki Ligi hiyo.

1.10 Timu yoyote iliyopewa adhabu ya faini chini ya kanuni 31:1(1.1, 1.2 na 1.3) haitaruhusiwa kucheza hadi itakapotekeleza adhabu hiyo kwa daraja ambalo itakuwa ipo.

## Kanuni : 33 Kuvuruga Mchezo

(1) Timu itakayosababisha mchezo kuvurugika na hatimaye kuvunjwa, itapoteza mchezo huo hata kama ilikuwa inaongoza kwa magoli na timu pinzani itapewa ushindi na pointi tatu (3) na magoli matatu (3), iwapo timu pinzani inaongoza kwa magoli zaidi ya matatu itabakia na idadi ya magoli hayo iliyokwishafunga.

(2) Goli lililofungwa katika mchezo wowote uliovurugika na kuvunjika litaendelea kuhesabiwa kwenye magoli ya mfungaji endapo mfungaji ni kutoka timu iliyoshinda shauri na halitahesabiwa kwenye magoli ya timu husika mpaka endapo tu goli hilo ni miongoni mwa magoli katika mchezo uliovurugika hali ikiwa timu isiyosababisha kuvurugika mchezo huo ilishafunga zaidi ya magoli matatu ya ushindi wa kikanuni. Kadi zote zitakazotolewa katika mchezo huo zitaendelea kuhesabika kwa wahusika.

(3) Magoli yaliyofungwa na timu iliyosababisha mchezo kuvunjika yatafutwa lakini magoli yaliyofungwa na timu pinzani yataendelea kuonekana katika idadi ya magoli yaliyofungwa na wachezaji wa timu hiyo wakati wa kutafuta mfungaji bora.

(4) Endapo itatokea vurugu ya aina yoyote ile na kusababisha mchezo kusimama katika mazingira ya kuhatarisha mchezo huo kuendelea, mwamuzi atasubiri kwa dakika zisizozidi kumi na tano (15) na endapo hali ya vurugu bado inaendelea mwamuzi atavunja mchezo huo.

(5) Endapo timu itagomea kuendelea na mchezo kwa sababu zozote zile na kusababisha mchezo huo kuvunjika au kuvunjwa na mwamuzi timu hiyo itapoteza mchezo huo na timu pinzani itapewa ushindi. Timu iliyogomea itatozwa faini ya shilingi milioni tatu (3,000,000/-).

(6) Faini iliyotajwa (kanuni 32:5) italipwa kabla ya mchezo unaofuata wa timu husika baada ya kuamriwa kulipa.

(7) Mchezaji na kiongozi watakaobainika kugomea au kusababisha vurugu zilizopelekea mchezo kuvunjika watafungiwa kujihusisha na masuala yote ya mpira wa miguu kwa kipindi kati ya miezi sita mpaka miaka mitano.

(8) Endapo uvunjikaji wa mchezo utabainika kuwa wa utata au sababu nyingine au kukosekana uzingativu wa kutosha wa kanuni 32:4, mchezo huo utarudiwa katika tarehe nyingine, waamuzi wengine na uwanja utakaoamuliwa na TPLB.

(9) Timu itakayoleta/itakayofanya vurugu za aina yoyote au kupinga, kuzuia au kugomea mchezo kuoneshwa kwenye televisheni au kutangazwa kwenye redio kinyume na ilivyoelekezwa na TFF/TPLB itatozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000/-). Endapo timu hiyo itarudia kosa hilo itachukuliwa hatua zaidi ikiwemo kushushwa Daraja.

(10) Endapo vurugu zitatokea uwanjani mara tu baada ya mchezo kumalizika, viongozi au wachezaji husika watakaobainika kusababisha na/au kufanya vurugu hizo watakabiliwa na adhabu ya kufungiwa kwa kipindi cha miezi mitatu mpaka kumi na miwili (12) na kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja (1,000,000/-) kwa timu husika.

(11) Endapo itathibitika timu yoyote imefanyiwa fujo na/au vurugu kabla, wakati au baada ya mchezo na washabiki wa timu pinzani, timu pinzani itakabiliwa na adhabu ya faini kati ya shilingi milioni moja (1,000,000/-) hadi shilingi milioni kumi (10,000,000/-) au/na kusimamishwa kwa michezo ya timu husika katika Kituo/Uwanja wake husika au timu hiyo italazimika kucheza michezo isiyopungua mitatu ya nyumbani kwenye uwanja wake bila ya kuwa na mashabiki na kulazimika kuilipa fidia timu pinzani kama itakavyoamuliwa na TPLB. Sambamba na adhabu hizo, klabu italazimika kulipa fidia kwa uharibifu wowote wa mali uliofanywa na mashabiki wake.

## Kanuni : 34 Kupanga Matokeo

(1) Endapo timu zozote zitabainika kuwa zimepanga kwa namna yoyote ile matokeo ya mchezo wowote waliocheza kwa madhumuni yoyote yale zitachukuliwa hatua zifuatazo:

1.1 Mtu yeyote aliyekula njama na kushawishi upangaji matokeo ataadhibiwa kwa kusimamishwa mechi na kufungiwa kushiriki katika shughuli yoyote ya mpira wa miguu kwa kipindi kisichopungua miaka 10 (kumi) na faini isiyopungua shilingi milioni kumi (10,000,000/-*)*. Katika shauri linalovuruga/kushusha hadhi ya mpira wa miguu, mhusika atafungiwa maisha kutojishughulisha na mpira wa miguu.

1.2 Ikiwa mchezaji au kiongozi atajishughulisha katika kushawishi upangaji matokeo kama ilivyo katika kanuni ya 33 (1.1), klabu au mkoa ambao mchezaji au kiongozi anatoka utapigwa faini. Katika makosa mazito itaadhibiwa kwa kuondolewa kwenye Ligi, kushushwa daraja, kupunguziwa pointi na kurudisha zawadi.

## Kanuni : 35 Kuahirisha Mchezo

(1) Mchezo unaweza kuahirishwa kutokana na sababu yoyote kati ya zifuatazo:

1.1 Endapo timu ya Taifa ina mchezo.

1.2 Endapo timu inashiriki katika mashindano ya Kimataifa na ina muda usiozidi siku tatu (3) kufikia mchezo wa Kimataifa.

1.3 Sababu ya dharura au/na yenye msingi itakayokubaliwa na TPLB.

1.4 Endapo itatokea matukio yalio nje ya uwezo wa binadamu *(force majure)* yasiyotarajiwa wala kusababishwa na timu husika.

1.5 Endapo wachezaji wasiopungua watatu (3) wa klabu moja wataitwa kushiriki mchezo wa timu ya Taifa.

(2) Mchezo wowote ulioahirishwa chini ya kanuni 34(1.1 – 1.3) utapangwa tena katika tarehe itakayoamuliwa na TPLB isipokuwa kama utaahirishwa chini ya kanuni 34(1.4) utachezwa siku inayofuata au muda mwingine wa karibu zaidi kadiri ratiba inavyoruhusu.

(3) Iwapo mchezo ulishaanza na kuvunjika kwa sababu ya matukio ya dharura yasiyotarajiwa wala kusababishwa na timu husika, utapangwa kuchezwa

kwa muda uliosalia kuanzia dakika na tukio ulipovunjika ukiwa na wachezaji na waamuzi walewale. Mabao yaliyofungwa na kadi/adhabu walizoonyeshwa wachezaji katika mchezo uliovunjika zitaendelea kuhesabika. Muda wa kuanza mchezo huo na taratibu zitaamuliwa na TPLB.

(4) Taarifa ya maombi ya kawaida ya kuahirisha mchezo ni lazima itolewe kwa maandishi si chini ya siku kumi na nne (14) kabla ya siku ya mchezo, isipokuwa kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa binadamu au dharura kubwa.

(5) Ruhusa ya wachezaji wanaoteuliwa kuchezea timu za Taifa za nchi zao na kwa timu za Taifa za vijana chini ya miaka 23 (ishirini na tatu) na miaka 20 (ishirini) itatolewa kwa kufuata sheria za FIFA kwa muda kabla na baada ya mchezo husika.

# SURA: X

## USIMAMIZI WA MCHEZO



## SURA : X USIMAMIZI WA MCHEZO

### Kanuni : 36 Msimamizi wa Kituo

(1) Kila kituo cha michezo ya Ligi Kuu patakuwepo Msimamizi wa Kituo Mkaazi, ambaye atakuwa ni Katibu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa husika atakayeteuliwa na TFF kushirikiana na Klabu Mwenyeji kuhakikisha Maandalizi na Uendeshaji wa mchezo husika vinafanyika kwa mujibu wa Taratibu na Kanuni za Ligi Kuu ikiwemo miongozo inayotokana nazo kutoka TFF/TPLB na kuridhiwa, kuongozwa na kusimamiwa na Kamishna wa Mchezo.

(2) Mapendekezo yoyote ya Uteuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Kituo kutoka FA(M) ni lazima yathibitishwe kwanza na TFF katika kukamilisha Uteuzi huo. Msimamizi Msaidizi ambaye hajathibitishwa na TFF, hatatambuliwa.

(3) Katika Mazingira maalum TFF inaweza kuteua Msimamizi wa Kituo kutoka Nje ya FA(M) husika/Mkoa wa Kituo kwa sababu maalum na atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu kwa Kituo husika kwa tukio husika kwa Mazingatio ya Utendaji kwa kanuni ya 35.1 ya kanuni hizi.

(4) Msimamizi wa Kituo atawajibika kuhakikisha anatuma kwa TPLB taarifa za fedha za mauzo ya tiketi, fedha stahili kwa TFF/TPLB na fomu za malipo ya Maofisa wa mchezo katika kipindi cha saa 24 (ishirini na nne) baada ya mchezo kumalizika.

(5) Msimamizi wa Kituo atawajibika kuhakikisha kuwa huduma zote muhimu na vifaa kazi kuufanya mchezo kuchezwa na kufanikiwa vi/zinakuwepo.

(6) Msimamizi wa Kituo atawajibika kumpa ushirikiano Kamishna wa mchezo kiutaratibu na ikitokea mahitaji ya ziada ndani ya Utaratibu kwa Kamishna katika kutimiza majukumu yake. Kamishna wa Mchezo ndiye Mwakilishi Rasmi wa kwanza wa Muendeshaji kwa mchezo husika.

(7) Msimamizi wa Kituo atahakikisha kwamba michezo yote ya vijana kwa mujibu wa kanuni hizi inayotakiwa kufanyika katika kituo chake inaandaliwa na kuchezwa bila kukosa.

(8) Msimamizi wa Kituo atawajibika kufanya mawasiliano na kutoa taarifa za kituo chake/mchezo husika kwa TFF/TPLB wakati wowote inavyofaa au atakapohitajika kutokana na Matukio au Uendeshaji kwa Kituo husika.

(9) Msimamizi wa Kituo anawajibika kwa Kanuni hizi. Hatua zitachukuliwa ipasavyo kwa mujibu wa Kanuni hizi katika Mazingira ya Msimamizi wa Kituo kufanya Vitendo kinyume na Kanuni hizi.

(10) Msimamizi wa Kituo kwa kushirikiana na Afisa Habari wa Mchezo ataandaa Mahali, kuratibu na Uendeshaji kwa ajili ya Mkutano kwa Waandishi wa Habari wa kabla ya Mchezo (prematch press conference) utakaohusisha Makocha na Manahodha/mchezaji mwingine mwenye ushawishi kwenye timu husika katika muda na siku itakayopangwa kabla ya mchezo.

(11) Msimamizi wa Kituo kwa Kushirikiana na Timu Mwenyeji watahakikisha kutokuwepo kwa Matangazo yoyote mengine ya Biashara yasiyotambuliwa au kudhinishwa na TFF/TPLB kwenye eneo la ndani la Uwanja na kuzunguka kiwanja cha kuchezea (pitch) ikiwemo mazingatio ya matangazo yaliruhusiwa yanayohusu Wadhamini wa Ligi Kuu.

## Kanuni : 37 Kamishina

(6) Katika mchezo wowote wa Ligi Kuu atapangwa Kamishina wa Mchezo kuhakiki, kuongoza na kusimamia Taratibu mbalimbali za Uendeshaji wa Mchezo kwenye maeneo ya Utawala, Uendeshaji na Ufundi na kutoa taarifa ipasavyo kwa TPLB.

(7) Kamishina wa Mchezo ndiye mwakilishi Rasmi wa TPLB kwa mchezo husika aliyekasimiwa Mamlaka ya Muendeshaji wa Shindano kwa Mchezo husika ambaye Taarifa zake kwa mujibu wa Muongozo, Kanuni na Taratibu za Ligi Kuu ndio Taarifa Kuu za Mchezo kwa Muendeshaji.

(8) Kamishina wa Mchezo atatoa taarifa mbalimbali na za jumla za mchezo, kwa TPLB akitumia fomu mbalimbali maalum zilizoandaliwa kwa madhumuni husika na kwa mujibu wa muongozo wa Kamishina uliotolewa na TFF ambao unasomeka pamoja na Kanuni hizi.

(9) Kamishina wa Ligi Kuu watapangiwa utaratibu wa kupatikana kwao au/na kuteuliwa na TFF kupitia mchakato mahsusi kwa Kamishina na kupangwa katika michezo ya Ligi Kuu kutegemea kiwango cha kukidhi vigezo stahili, uwajibikaji na kuaminika kwake katika uwezo wa utekelezaji ipasavyo wa Muongozo wa Kamishina uliotolewa na TFF.

(10) Kamishina wa Ligi Kuu atatokana na aidha aliwahi kuwa au ni kiongozi wa mpira wa miguu wa ngazi fulani, Mwamuzi mstaafu, Kocha *(asiyefundisha timu katika Ligi Kuu/Mashindano ya TFF)* au Mchezaji wa zamani aliyepata sifa na kuheshimika au mwanafamilia mwingine wa mpira wa miguu anayeaminika.

(11) Kamishina atawajibika kushughulikia ipasavyo malalamiko *(pingamizi)* yanayotolewa kabla, baada au wakati wa mchezo pamoja na kukusanya ushahidi unaohitajika utakaosaidia vyombo husika kufanya maamuzi stahili.

(12) Kamishina wa Mchezo anaweza kuishauri TFF/TPLB kuzuia kuchezwa kwa Mchezo katika mazingira ya kabla ya mchezo kuanza endapo atajiridhisha kukosekana kwa usalama kwa timu na maofisa wa mchezo husika na baada ya jitihada zake za utatuzi wa hilo kushindikana. Endapo mchezo ulishaanza Maamuzi yatakuwa ya mwamuzi wa mchezo huo. Katika Mazingira maalum Kamishina anaweza kushauriana na Mwamuzi endapo hali ya usalama inatishia usalama wa timu na maafisa mchezo.

(13) TFF itatoa Muongozo kwa Kamishina utakaokuwa na maelekezo muhimu na ya lazima kwa Kamishina kutekeleza katika Majukumu yake ya Usimamizi wa Michezo mbalimbali atakayopangiwa.

## Kanuni : 38 Mratibu wa Mchezo

(1) Kutakuwa na Mratibu wa Mchezo (GC) ambaye ni Mtendaji mkuu wa shughuli za Uendeshaji mchezo akiwakilisha TPLB. Mratibu wa mchezo ndiye atakayekuwa Msaidizi wa kwanza wa Kamishina wa Mchezo akiratibu na kutekeleza majukumu ya uendeshaji ya kamishina wa mchezo ambapo Kamishina atabakia na jukumu Kuu la Usimamizi wa Jumla wa Mchezo akiendelea kuwa Mwakilishi Mkuu wa TPLB Kituoni na kwa mujibu wa Muongozo wa Kamishina.

(2) TPLB inaweza kuteua Mratibu wa Mchezo (GC) katika kuboresha na kuongeza kiwango cha Utendaji kwa mchezo husika ambapo Mratibu wa Mchezo atafanya kazi za Maandalizi na uendeshaji wa mchezo kwa Ushirikiano wa kiUtaratibu kutoka Kituoni, chini ya Usimamizi wa Kamishina wa mchezo.

(3) Mratibu wa Mchezo atawajibika kutuma Taarifa yake kwa kutumia Fomu Maalum kwa ajili hiyo itakayotolewa na TPLB katika muda usiozidi masaa ishirini na nne baada ya mchezo husika kumalizika.

(4) Mratibu wa Mchezo atashughulikia masuala yote mengine ya uandaaji na uendeshaji kwenye Mchezo katika maeneo ambayo hakuna Afisa aliyeteuliwa maalum kwa ajili hiyo.

(5) Mratibu wa Mchezo ataongoza timu na waamuzi kuingia kiwanjani (pitch) tayari kwa hatua za mwisho za kuanza mchezo.

(6) Mratibu wa Mchezo atafanya shughuli zake kwa Mazingatio ya Muongozo kwa Mratibu wa Mchezo uliotolewa na TFF/TPLB.

6.1 Mratibu wa Mchezo atakayeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo au kutekeleza bila kufuata Mazingatio ya Muongozo kwa Mratibu wa Mchezo uliotolewa na TFF/TPLB, ataadhibiwa kwa kuonywa, kuondolewa katika ratiba ya waratibu wa michezo kati ya mizunguko mitatu (3) mpaka mitano (5) au kufungiwa kati ya miezi mitatu (3) mpaka sita (6).

6.2 Kwa makosa yanayojirudia na kwa makosa ya rushwa atafungiwa kwa miaka mitatu (3) au/na kuondolewa au kufutwa kabisa katika orodha ya waratibu wa michezo wanaotambuliwa na TFF.

## Kanuni : 39 Mtathimini Waamuzi

(1) TFF inaweza kumpanga Mtathimini Waamuzi katika mchezo wowote wa Ligi Kuu endapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Mtathimini Waamuzi lazima awe ni mwamuzi mstaafu aliyefikia kiwango cha juu cha uchezeshaji wakati akichezesha kabla ya kustaafu na amepata mafunzo ya Ukufunzi wa waamuzi.

(3) Katika Mazingira ya uwepo wa Mtathimini wa Waamuzi *(referees' assessor)*, atawawakilisha Wamuzi katika majukumu yanayohusu shughuli za waamuzi kabla na baada ya mchezo akishirikiana na Mwamuzi wa akiba *(4th official)*.

## Kanuni : 40 Waamuzi

(1) Kutakuwa na waamuzi TEULE (select referees) ishirini na nne (24) na waamuzi wasaidizi arobaini (40) watakaoteuliwa na Kamati ya Waamuzi ya TFF mwanzoni mwa kila msimu maalum kwenye Orodha ya Waamuzi watakaopangwa kuchezesha michezo ya Ligi Kuu. Waamuzi TEULE hawa wanawajibika kuwa waaminifu, waadilifu na wenye nidhamu na tabia njema zisizotiliwa mashaka.

(2) Katika Orodha ya Waamuzi Teule wa Ligi Kuu kutakuwepo waamuzi wachache wa akiba kwa Ligi Kuu wanaoweza kujumuishwa kuchezesha michezo ya Ligi Kuu katika mazingira ya dharura au uwepo wa haja ya kufanya hivyo kwa sababu zinazoaminika. Katika Mazingira ya kawaida, Waamuzi wa Akiba katika Orodha ya Waamuzi teule wa Ligi Kuu watatumika kuchezesha Ligi ya Championship.

(3) Mwamuzi TEULE yeyote wa Ligi Kuu anaweza kuondolewa wakati wowote endapo TFF itajiridhisha au kubaini Mapungufu katika uwezo wake, Uadilifu au Uwajibikaji wake kwenye michezo na kuhusiana na Ligi Kuu na michezo mingine aliyopangiwa na wakati wowote TFF inaweza kufanya Uteuzi wa Mwamuzi TEULE wa Ligi Kuu kwa Mazingatio ya Sifa na Vigezo kwa Mujibu wa Kanuni hizi.

(4) Waamuzi TEULE watateuliwa wakijumuisha waamuzi na waamuzi wasaidizi walio na hadhi ya FIFA, pia kutoka miongoni mwa waamuzi wazoefu na vijana wanaofanya vizuri sana kwa kipindi husika walio na Hadhi ya Daraja la Kwanza *(Class I)*.

(5) Waamuzi TEULE watateuliwa kwa kukidhi vigezo na kuwa na sifa zifuatazo:

5.1 Umri wa miaka isiyopungua miaka 23 (ishirini na tatu) kwa mwanaume na 21 (ishirini na moja) kwa wanawake na wasiozidi miaka 45 (arobaini na tano) katika siku ya tarehe ya Uteuzi.

5.2 Uzoefu wa kuchezesha michezo ya Ligi Kuu au Ligi Daraja la Kwanza usiopungua misimu miwili (2). Mwamuzi kijana aliyetathiminiwa na kuonyesha kiwango bora katika msimu mmoja katika matukio ya michezo yanayoaminika kwa TFF au anayetokana na Programu za Maendeleo ya Uamuzi na Waamuzi za TFF anaweza kujumuishwa.

5.3 Awe amefaulu mtihani wa afya yake *(medical examination)*, amekidhi kiwango kwa jaribio la utimamu

wa mwili wake *(physical fitness test)* iliyoendeshwa na Mkufunzi maalum wa utimamu wa mwili *(referee physical fitness Instructor)* iliyosimamiwa na Kamati ya Waamuzi ya TFF (au Mamlaka za Kimataifa zinazokubalika) na kufaulu mtihani wa sheria za mpira wa miguu (Laws of the Game). Mwamuzi mwanamke anawajibika kufaulu katika viwango vya wanaume ili kuchezesha michezo ya wanaume.

(6) TFF itaandaa Jaribio la Utimamu wa mwili *(physical fitness test)* kwa waamuzi wa Ligi Kuu kulingana na mahitaji na utaratibu wake litakaloambatana na upimaji wa afya ya mwamuzi *(medical examination)* na mitihani ya sheria za mpira wa miguu *(Laws of the Game)*. Mwamuzi anawajibika wakati wote wa msimu kuwa tayari kiafya, kimwili na ufahamu wa sheria.

(7) Kamati ya Waamuzi ya TFF itapanga Waamuzi kwenye Michezo ya Ligi Kuu na ndiyo pekee yenye mamlaka ya kupanga, kubadilisha na kuondoa mwamuzi kwenye ratiba kwa Utaratibu na Mfumo uliowekwa *(kwa kushirikiana na Sekretarieti ya TFF)* kwa Mazingatio ya Kanuni hizi.

7.1 Kamati ya Waamuzi ya TFF inaweza kupanga mwamuzi/waamuzi kutoka nje ya Tanzania kwenye Michezo ya Ligi Kuu.

(8) Klabu au yeyote aliye na malalamiko au jambo kuhusu kupangwa au Uchezeshaji wa mwamuzi anawajibika kuwasilisha kwa Maandishi kwa TFF si chini ya siku tatu (3) katika mazingira ya wakati kabla ya Mchezo na/au wakati mwingine wowote baada ya Mchezo husika. Hairuhusiwi kwa klabu/Kiongozi/Kocha/Mchezaji kumkataa mwamuzi yeyote aliyepangwa wala kumjadili au kushutumu kwa namna yoyote au kwenye vyombo vya habari. TFF itachukua hatua katika mazingira ya uvunjifu wa sharti hili.

(9) Mwamuzi na mwamuzi msaidizi yeyote aliyepangwa kuchezesha mchezo wowote wa Ligi Kuu anawajibika kuzingatia yafuatayo:

9.1 Kutoa taarifa kwa TFF mara tu baada ya kupata taarifa ya Uteuzi wake juu ya uhusiano wowote kati yake na mhusika yoyote katika klabu au klabu alizopangiwa kuchezesha yanayoweza kusababisha mgongano wa kimaslahi *(conflict of interest)*.

9.2 Kutoa taarifa siku saba (7)/au muda wa karibu zaidi katika hali ya kawaida kabla ya mchezo aliopangiwa endapo hataweza kushiriki katika mchezo huo na kutoa sababu, na pia anaweza kutoa taarifa kwa dharura kutegemea dharura iliyojitokeza.

9.3 Kutoa taarifa ya safari yake kwa TFF na Msimamizi wa Kituo/Kamishina wa Mchezo husika aendako na matarajio ya kuwasili kwake.

9.4 Kufika kituo cha mchezo siku moja kabla na kuondoka si zaidi ya siku moja baada ya mchezo labda tu kwa dharura kubwa na za msingi. Mwamuzi atawajibika kutoa Taarifa rasmi kwa TFF katika mazingira ya tofauti na sharti hili.

9.5 Kuhudhuria kikao cha maandalizi ya mchezo (prematch meeting) kwa muda uliopangwa akiwa nadhifu, makini na kamili kwa wakati na bila kukosa wala kuchelewa *(wanaweza wasihudhurie endapo atateuliwa Mtathimini waamuzi)*.

9.6 Kuwasilisha kwa Kamishna wa Mchezo husika madai yake sahihi ya malipo anayostahili na gharama zinazostahili marejesho (*akiambatanisha stakabadhi au nyaraka za uthibitisho)* kwa umakini, unadhifu na bila udanganyifu.

9.7 Kufika Uwanjani katika muda uliokubalika kwenye kikao cha maandalizi ya mchezo akiwa makini, kamili, nadhifu na bila kuchelewa.

9.8 Kutekeleza wajibu wake kwa/kwenye nafasi yake kama mwamuzi kwa kuzingatia miiko na maadili ya uamuzi, Uwajibikaji unaotarajiwa na mazingatio yasiyo mashaka ya sheria kumi na saba za mpira wa miguu *(17 Laws of the Game)* bila hiyari.

9.9 Kuhakikisha amepata uthibitisho kutoka kwa ofisa mhusika kwenye Leseni yake ya Uamuzi *(referee LogBook)* bila kukosa.

9.10 Kutoa taarifa kwa TPLB/TFF kwa njia ya barua pepe (email) juu ya masuala yote yaliyo kwenye eneo lake pamoja na uchezeshaji na hali ya mchezo husika ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya mchezo kumalizika kwa kujaza fomu maalum ya Taarifa ya mwamuzi

kwa unadhifu, ukweli, umakini na mazingatio ya weledi wa kiuamuzi *(kwa mwamuzi wa kati)*. Mwamuzi atawajibika kutuma taarifa ya awali *(flash report)* na katika mazingira maalum au hitajika, mwamuzi anaweza kulazimika kutuma taarifa yake ya mchezo kwa njia ya elektroniki.

(10) Katika mchezo wowote wa Ligi Kuu, uamuzi wa Mwamuzi uwanjani ni wa mwisho. Klabu zinatakiwa kuchukua hatua zinazofaa katika kutaarifu mamlaka husika juu ya malalamiko yoyote yanayohusiana na uamuzi au mwamuzi uwanjani kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(11) Mwamuzi wa Ligi Kuu aliyepangwa kwenye mchezo husika hatakiwi kuwa na uhusiano unaosababisha mgongano wa kimaslahi baina yake binafsi katika au/na mojawapo au klabu zote anazozichezesha. Mwamuzi atahitajika kutoa taarifa kwa TFF endapo ana uhusiano unaoweza kusababisha mgongano wa kimaslahi kwa mchezo wowote aliopangiwa wa Ligi Kuu, TFF itachukua hatua zinazofaa katika mazingira hayo.

(12) Mwamuzi wa Ligi Kuu haruhusiwi kuchezesha mchezo wowote ulio na hadhi ya Kitaifa ndani na nje ya nchi usiotambuliwa na TFF, na vivyo hivyo katika Hadhi zilizo kwenye Mamlaka ya FA(M) na FA(W) wake/yake husika, mwamuzi atakayekiuka atakabiliwa na adhabu.

(13) Mwamuzi wa mchezo ndiye pekee mwenye mamlaka ya kuamua kuhusu hali ya uwanja wa kuchezea *(pitch)* na kuruhusu mchezo kuchezwa au vinginevyo kwa mazingatio ya mahitaji kisheria kwa uwanja wa kuchezea na Maamuzi yake ni ya mwisho.

(14) Mwamuzi na mwamuzi msaidizi yeyote aliyeteuliwa na kupangwa kuchezesha Ligi Kuu anawajibika kujiheshimu, kuwajibika, kufuata sheria kumi na saba za mchezo na kuzingatia nidhamu, maadili na sheria katika utekelezaji wa majukumu yake katika kiwango bora na kisichotia mashaka. Aidha mwamuzi anawajibika kuwa na haiba na mwenendo bora wa kitabia katika ushirikiano wake na wadau wengine wa mpira wa miguu.

# SURA: XI

## UDHIBITI NA ADHABU



| SURA : XI | UDHIBITI NA ADHABU |
|---|---|
| **Kanuni : 41** | **Udhibiti Kimashindano** |

(1) Adhabu yoyote kwa Wachezaji, Maafisa wa Ufundi na muhusika yoyote binafsi katika Ligi Kuu zitahusiana na kutekelezwa katika Mashindano yote Rasmi ya TFF ambapo muhusika atawajibika kutumikia adhabu husika katika mchezo au ushiriki wake mwingine kwenye michezo ya Mashindano yote ya TFF. Adhabu zilizo na malimbikizo *(cautions)* zitahesabiwa kwa kuhusisha Mashindano yote Rasmi ya TFF.

(2) Ni marufuku kwa Kocha/kiongozi wa Timu/Klabu, mchezaji au mdau mwingine yeyote wa mpira wa miguu wakiwemo maofisa habari wa klabu kushutumu au kutoa matamshi/maandiko/picha/video kwa lengo la kumkejeli au kumshutumu au kumkashifu au kumdhalilisha Mwamuzi yeyote wa mchezo/kiongozi yeyote wa klabu/kiongozi wa TFF/FA(M)/TPLB kwenye vyombo vya habari na mahali pengine popote. Kiongozi au mdau atakayekiuka atafungiwa idadi ya michezo isiyopungua mitatu (3) au kujihusisha na mpira wa miguu kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu (3) na kisichozidi miezi kumi na miwili (12) na/au faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-).

(3) Adhabu za kuondolewa kwa mwamuzi au Ofisa mwingine wa mchezo zitatumika kwa Mashindano yote ya TFF isipokuwa tu pale ambapo adhabu husika imetolewa maelekezo maalum na chombo husika.

(4) Pamoja na kutambua masharti yanayoainishwa kwenye kanuni ya 76 ya kanuni huzi, Tukio lolote la uvunjifu wa Kanuni mchezoni kama kupiga, kupigana, kutoa lugha za kashfa au matusi, kufanya vitendo vya kudhalilisha, vya kibaguzi na/au kuvunja hadhi lililo na Ushahidi usiotiliwa mashaka litaamuliwa moja kwa moja na Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji bila ya mahitaji ya kupelekwa kwenye vyombo vingine vya maamuzi. Kwa Matukio yanayohitaji Uchunguzi yatapelekwa kwenye Vyombo husika vya TFF.

(5) Kitendo chochote cha uvunjaji taratibu au ukiukaji mwingine wowote kanuni na taratibu kwa mujibu wa kanuni hizi ikiwemo taratibu za Usajili wa wachezaji au taratibu nyingine za uendeshaji Ligi Kuu ambao haukuainishwa waziwazi kwenye kanuni hizi bado utastahili adhabu kwa muhusika kwa kupewa Onyo Kali au Karipio na/au faini kati ya shilingi laki tatu (300,000/-) mpaka shilingi milioni tatu (3,000,000/-) na/au kufungiwa kwa kipindi kati ya miezi mitatu (3) mpaka miezi ishirini na nne (24) au michezo kati ya mitatu (3) mpaka kumi (10).

(6) Ni marufuku kwa kocha, mchezaji, kiongozi au ofisa wa mchezo kushiriki michezo ya kubashiri (betting). Kocha, mchezaji, kiongozi au ofisa wa mchezo atakayekiuka, atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

6.1. Zuio la kushiriki michezo ya kubashiri litajumuisha pia kutoa taarifa zozote kwa mtu mwingine (Third party) kuhusiana na mbinu za mchezo wa timu, benchi la ufundi au mchezaji. Hivyo

hairuhusiwi kutoa taarifa hizo iwe kwa ahadi ya zawadi,tuzo au msaada wa iana yoyote bila kujali mahusiano ya mtoaji na mpokea taarifa.

6.2. Viongozi wa klabu, wataalamu wa ufundi, wachezaji na waamuzi wanao wajibu wa kutoa taarifa juu ya mtu yeyote au kikundi cha watu wanaojihusisha na michezo ya kubashiri kinyume na kanuni hii au ana uhusiano wa karibu au ushirikiano na mtu anayeshiriki au taasisi inayoendesha michezo ya kubashiri.

6.3. TFF/TPLB watafuatilia matukio yote katika michezo ambayo yana viashiria vya kuhusishwa

6.4. na uhusika katika michezo ya kubashiri na pale itakapobainika, wahusika wataadhibiwa kwa mujibu wa kanuni.

6.6. Mchezaji, kiongozi wa klabu au ofisa mwingine yeyote wa klabu atakayekiuka kanuni hii,baada ya kusikilizwa na kuonekana ushahidi wake hauna mashiko ataadhibiwa kwa kupewa adhabu yoyote kati ya zifuatazo;-
a) Kutojihusisha na mpira wa miguu kwa maisha yake yote (life ban).
b) Kufungiwa kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au faini ya shilingi milioni thelathini (30,000,000) au vyote kwa pamoja.

(7) Adhabu za Kadi na nyinginezo zinazohusiana na mchezo zitatafsirika kwa alama kama inavyoonekana kwenye jedwali la viwango vya adhabu:

| Kiwango cha Adhabu | Alama |
|---|---|
| **WACHEZAJI** | |
| Kadi ya Njano | 1 |
| Kadi ya Pili ya Njano (Nyekundu) | 2 |
| Kadi Nyekundu (ya moja kwa moja) | 3 |
| Kadi Nyekundu (ya moja kwa moja kupiga/nyingine) | 5 |
| Adhabu bila ya kuonyeshwa kadi Uwanjani | 5 |
| **VIONGOZI WA UFUNDI** | |
| Kadi ya Njano | 1 |
| Kadi ya Pili ya Njano (Nyekundu) | 3 |
| Kadi Nyekundu (ya moja kwa moja) | 4 |
| Kadi Nyekundu (ya moja kwa moja kupiga/nyingine) | 6 |
| Adhabu bila ya kuonyeshwa kadi Uwanjani | 6 |

## Kanuni :42 Udhibiti kwa Wachezaji

(1) Wachezaji wa Ligi Kuu wanatakiwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa, wanatakiwa kudumisha Nidhamu ndani na nje ya uwanja. Mienendo ya wachezaji itadhibitiwa na Kanuni hizi.

(2) Mchezaji atakayeadhibiwa na Mwamuzi kwa kuonyeshwa kadi kutokana na makosa kuhusiana na Mchezo husika ataadhibiwa kwa Utaratibu ufuatao:

2.1 Mchezaji atakayetolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kadi mbili za njano *(second yellow card)* katika mchezo wa Ligi hataruhusiwa kucheza mchezo mmoja unaofuata wa timu yake.

2.2 Mchezaji atakayetolewa nje kwa kadi nyekundu ya moja kwa *moja (straight red)* atakosa michezo miwili inayofuata ya timu yake.

2.3 Mchezaji atakayeonywa kwa kadi ya njano katika michezo minne (4) hataruhusiwa kucheza mchezo mmoja unaofuata wa timu yake.

2.4 Mchezaji atakayepata kadi ya njano katika mchezo itakayotimiza idadi ya kadi nne (4) za njano zinazostahili adhabu na kisha kupata kadi nyekundu ya moja kwa moja *(straight red)* katika mchezo huo huo atafungiwa kucheza michezo mitatu (3) inayofuata ya timu yake.

2.5 Mchezaji atakayepata kadi ya njano katika mchezo itakayotimiza idadi ya kadi nne (4) za njano zinazostahili adhabu na kisha kupata kadi ya pili ya njano na hivyo kupewa kadi nyekundu *(second yellow)* katika mchezo huo huo atafungiwa kucheza michezo miwili (2) inayofuata ya timu yake.

2.6 Mchezaji atakayetolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kosa la kupiga/kupigana na mchezaji mwenziye katika mchezo husika atasimama kushiriki michezo mitatu (3) inayofuata ya klabu yake na atalipa faini ya shilingi milioni moja (1,000,000).

(3) Mchezaji yeyote atakayetakiwa kufanya vipimo vya dawa za kulevya au kuongeza nguvu, anawajibika kufanya hivyo, endapo atagundulika kutumia dawa za kulevya au kuongeza nguvu au atakataa kufanya vipimo hivyo atafungiwa kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12).

(4) Mchezaji yeyote atakayebainika kugomea mchezo, kufanya vurugu na/au kusababisha kuvurugika kwa mchezo mpaka mchezo huo kuvunjika atafungiwa kucheza na kujihusisha na mpira wa miguu kwa kipindi kati ya miezi sita (6) mpaka miaka mitano (5) na faini ya shilingi laki tano (500,000) mpaka shilingi milioni moja (1,000,000).

(5) Mchezaji atakayefanya jambo lolote kati ya yafuatayo atafungiwa michezo isiyopungua mitatu (3) na/au faini isiyopungua shilingi milioni tano (5,000,000/-).

5.1. Kutojiunga na Timu ya Taifa kwa sababu yoyote isiyo ya msingi.

5.2. Kupigana/kupiga kabla, wakati wa mchezo au mara tu baada ya mchezo kumalizika.

5.3. Kumshambulia mwamuzi, kiongozi, mtazamaji au mtu yoyote kwa namna yoyote ile, iwe kwa matusi au kwa vitendo.

5.4. Kufanya kitendo chochote cha aibu, kama vile kukojoa kiwanjani, kukataa kupeana mkono na mgeni rasmi, waamuzi na wachezaji wa timu pinzani, kutoa au kuonesha ishara inayoashiria matusi.

5.5. Kufanya vitendo vyenye kuonesha imani za ushirikina na uchawi hadharani au vitakavyobainishwa kwa ushahidi mwingineo.

5.6. Kufanya kitendo chochote kingine kitakachobainika kuwa ni kinyume cha maadili ya mchezo wa mpira wa miguu.

(6) Mchezaji atakayebainika kukutwa na makosa ya utovu wa nidhamu yanayojirudia au mara nyingi (sugu wa utovu wa nidhamu) atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(7) Mchezaji atakayeonyeshwa kadi nyekundu katika mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu au atakayemaliza msimu wa Ligi Kuu akiwa na adhabu ambayo haijaisha muda wake ataendelea kutumikia adhabu hiyo katika msimu unaofuata (katika timu au daraja lolote) isipokuwa adhabu inayotokana na kadi za njano (kanuni 41:2.3).

(8) Mchezaji atakayesababisha na/au kufanya vurugu za aina yoyote mara baada ya mchezo kumalizika atafungiwa kati ya michezo mitatu (3) mpaka sita (6) na/au faini isiyopungua shilingi milioni tano (5,000,000/-).

(9) Mchezaji atakayebainika kutoa taarifa za uongo kufanikisha kuthibitishwa kwa usajili wake na kushiriki kucheza Ligi Kuu atafungiwa kwa kipindi kisichozidi miaka miwili ( 2 ) na faini ya shilingi milioni moja (1,000,000/-) Matokeo ya michezo aliyocheza yatabaki kama yalivyotokea uwanjani.

(10) Mchezaji atakayebainika kushiriki kucheza mchezo wa Ligi Kuu hali akijua kuwa hajathibitishwa kiusajili atafungiwa kujihusisha na masuala ya mpira wa miguu kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12) na faini ya shilingi milioni moja (1,000,000/-). Timu iliyomchezesha itapoteza mchezo wowote alioshiriki na timu pinzani itapewa ushindi.

(11) Mchezaji atakayebainika kupanga matokeo ya mchezo kwa namna yoyote ile atafungiwa maisha kucheza mpira ndani na nje ya nchi.

(12) Mchezaji yeyote atakayebadili jina lake halisi kwa madhumuni ya

kudanganya ili asajiliwe kinyume cha masharti ya kanuni hizi atafungiwa kucheza mpira wa miguu ndani na nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe ya kubainika.

(13) Mchezaji atakayebainika kusaini mikataba na klabu zaidi ya moja kwa wakati mmoja na kuombewa usajili na klabu hizo katika kipindi cha msimu mmoja wa usajili atafungiwa kucheza mpira ndani na nje ya nchi kwa kipindi kati ya mwaka mmoja (1) na miaka mitatu (3).

(14) Mchezaji yeyote wa timu ya Ligi Kuu atakayekataa kuhojiwa na vyombo vya habari baada ya mchezo kumalizika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na maofisa wa mchezo atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(15) Mchezaji wa Klabu ya Ligi Kuu anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa kanuni hizi kutokana na makosa ya utovu wa nidhamu au ukiukaji wa maadili yaliyotokana na mchezo wa kirafiki na mashindano mengine yanayotambuliwa aliyoshiriki na timu yake.

(16) TFF/TPLB inaweza kuwatumia kwa pamoja wachezaji wasiopungua wanne katika shughuli ya kijamii kuhusiana na Ligi Kuu na Udhamini wa Ligi Kuu kupitia klabu yao. Wachezaji watakaokaidi/kushindwa bila sababu za msingi zinazokubalika kwa TFF/TPLB kila mmoja atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(17) Mchezaji aliyetozwa faini na kuamriwa kulipa kutokana na makosa aliyofanya hataruhusiwa kucheza mchezo unaofuata wa klabu yake mpaka faini hiyo iwe imelipwa, klabu itapoteza mchezo kwa kumchezesha mchezaji ambaye hajalipa faini bila ya kujali kumalizika kwa adhabu nyingine iliyoambatana na faini hiyo.

(18) Mchezaji atakayemaliza msimu wa ligi au kuhamia klabu nyingine akiwa anatumikia adhabu ataendelea kutumikia adhabu hiyo katika msimu unaofuata au katika klabu atakayohamia kwa daraja atakalokuwepo. Ukiukwaji wa sharti hili utavutia kufikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(19) Uvunjifu wowote wa Masharti ya Kimkataba yanayohusu Matumizi yoyote ya Mchezaji wa Klabu ya Ligi Kuu yasiyokuwa na ridhaa au idhini ya Klabu yake yataamuliwa na Klabu husika kwa Mazingatio ya Masharti stahili ya Mkataba wa Mchezaji na Klabu husika.

(20) Mchezaji yeyote atakayepatikana na hatia ya kufanya makosa makubwa ya kimaadili au kinidhamu, au ya kibaguzi au ya kidhalilishaji au yatakayotafsiriwa kuwa ni ukiukaji mkubwa wa taratibu za mchezo na ubinadamu atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(21) Mchezaji atakayethibitika na kupatikana na hatia ya kumpiga mchezaji mwenzake isivyo kawaida au kwa kutumia nguvu kubwa kuliko kawaida/kupigana au kumpiga mwamuzi, kijana wa mipira (ball kids), au ofisa/mhudumu mwingine wa mchezo atasimama kushiriki michezo isiyopungua mitatu (3), au kufungiwa kati ya miezi mitatu mpaka mwaka mmoja na faini isiyopungua shilingi milioni tatu

(3,000,000/-) bila ya kujali kutochukuliwa hatua au hatua yoyote iliyochukuliwa na mwamuzi uwanjani na kwa mazingatio ya kanuni ya (41.5.2 & 41.5.3).

## Kanuni : 43 Udhibiti kwa Waamuzi

(1) Mwamuzi yeyote atakayethibitika au kubainika kwa lolote miongoni mwa yafuatayo katika kanuni hii atapata adhabu ya kuonywa, kuondolewa katika ratiba ya waamuzi kati ya mizunguko mitatu (3) mpaka mitano (5), kufungiwa kati ya miezi mitatu (3) mpaka sita (6).
Kwa makosa yanayojirudia na kwa makosa ya Rushwa atafungiwa kwa miaka mitatu (3) au/na kushushwa daraja la uamuzi au/na kuondolewa au kufutwa kabisa katika orodha ya waamuzi wanaotambuliwa na TFF na kunyang'anywa leseni/hadhi ya uamuzi.

1.1 Akishindwa kumudu mchezo kwa uzembe, makusudi, woga au kutozingatia sheria ipasavyo kiasi cha kuvuruga mchezo, kuhatarisha amani au kutia aibu fani ya uamuzi na/au kushusha hadhi ya mpira wa miguu.

1.2 Akishindwa kufika kwenye kituo kwa wakati au kushindwa kufika kwenye mchezo au kuchelewa kwenye mchezo kiasi cha kusababisha mchezo kuanza ukiwa umechelewa au kutofanyika au kusababisha mchezo kuahirishwa au kurekebishwa kwa ratiba ya waamuzi.

1.3 Akifanya kitendo cha utovu wa nidhamu kama vile kutukana, kufanya fujo ya aina yoyote, kuanzisha ugomvi au kupigana kabla, wakati au baada ya kumaliza mchezo, kubainika kutumia kilevi cha aina yoyote wakati wa kikao cha maandalizi na wakati wa mchezo pamoja na kitendo kingine chochote kinyume na maadili ya uamuzi wa mpira wa miguu.

1.4 Akibainika kuandika taarifa yake kwa kusudio la kutoa taarifa ya uongo au kusudio lolote au kutoa taarifa itakayobainika kuwa sio sahihi au ya udanganyifu kwa sababu yoyote ile.

1.5 Akibainika kwa namna yoyote au kutoa visingizio visivyokuwa na msingi ili kukwepa mchezo aliopangiwa au atakayekuwa na uhusiano katika/na timu yoyote aliyopangiwa kuchezesha na kushindwa kutoa taarifa za uhusiano huo kwa wakati.

1.6 Atakayebainika kushindwa kuchukua hatua stahili kwa wachezaji na viongozi wa timu kwa vitendo vya utovu wa nidhamu au ukiukwaji wa taratibu kipindi kabla, wakati na baada tu ya mchezo kumalizika.

1.7 Atakayebainika kutovaa vifaa vya mdhamini alivyopewa kwa madhumuni yaliyokusudiwa na/au atakayefanya jambo lolote kumdhalilisha mdhamini wa Ligi Kuu au bidhaa au tangazo la mdhamini katika mchezo husika au kwa namna yoyote ile.

1.8 Atakayebainika kushindwa kutafsiri sheria za mpira wa miguu ipasavyo katika mchezo aliouchezesha na kupelekea kuwa na upungufu mwingi wa kiuchezeshaji na hata kusababisha kupata alama ndogo au kubainika kwa hali hiyo ya uchezeshaji kwa njia nyingine yoyote inayoaminika.

(2) Akibainika kuwa amedai Rushwa au amepokea/ametoa Rushwa au kuhusika na matendo yoyote yanayoashiria Rushwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kabisa kutoa taarifa ya Rushwa au kwa wakati, au kutoa taarifa ya mpango wa Rushwa inayotia mashaka au kushawishi kuteuliwa na/au kupangwa kwa njia yoyote atafungiwa kwa mwaka mmoja mpaka miaka mitatu (3) au maisha.

(3) Mwamuzi TEULE wa Ligi Kuu atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF kutokana na makosa yanayotokana na mchezo wa kirafiki na mashindano mengine yanayotambuliwa aliyochezesha yakihusisha timu ya/za Ligi Kuu au kwa kuchezesha mchezo wowote wa mpira wa miguu usiotambuliwa na TFF na FA(M) wake au FA(W) yake.

(4) Mwamuzi yeyote atakayebainika kuwa na upungufu au kushindwa kukidhi mahitaji ya vigezo na taratibu za kiuamuzi kama zinavyoainishwa kwenye kanuni ya 39:5(5.1 - 5.3) na 39:9(9.1 – 9.10) ya kanuni hizi ataadhibiwa kwa kuondolewa kwenye ratiba kwa mizunguko mitatu (3) mpaka mitano (5), kupewa Onyo Kali au Karipio, kushushwa daraja la Mashindano au Kufungiwa kipindi kuanzia mwezi mmoja (1) mpaka mwaka mmoja (1), kwa makosa ya Rushwa ataondolewa kwenye ratiba ya Ligi Kuu au/na kushushwa Daraja la Uamuzi na/au Kufutwa kwenye orodha ya waamuzi wanaotambuliwa na TFF na kunyanganywa leseni yake ya uamuzi.

## Kanuni : 44 Udhibiti kwa Kamishna

(1) Kamishna wa Ligi Kuu anawajibika kujiheshimu, kuwa makini na kushughulikia masuala yote ya mchezo ipasavyo na kuyatolea taarifa kwa kutumia fomu maalum kwa ukweli na umakini na si vinginevyo.

(2) Kamishna wa Ligi Kuu anaweza kuchukuliwa hatua stahili kwa makosa yoyote yaliyotokana na mchezo wa kirafiki aliosimamia uliohusisha timu ya/za Ligi Kuu au za Mashindano mengineyo.

(3) Kamishna Atakayebainika kuwa amedai Rushwa au amepokea/ametoa Rushwa au kuhusika na mpango/matendo yoyote yanayoashiria Rushwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kabisa kutoa taarifa ya Rushwa au kwa wakati, au kutoa taarifa ya mpango wa Rushwa inayotia mashaka atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(4) Kamishna anaweza kuadhibiwa kwa Onyo au Karipio au Kufungiwa kati ya miezi mitatu (3) mpaka miaka mitatu (3) au kuondolewa kwenye ratiba ya Ligi Kuu au kuondolewa kwenye Orodha ya Makamishna wanaotambuliwa na TFF endapo atabainika au kuthibitika kufanya katika yafuatayo:

(4.1) Kamishna atakayebainika kukataa kupokea Pingamizi la Mchezo au Malalamiko kwa sababu zisizokuwa za msingi/au atakayeshindwa kuchukua hatua stahili kuhusiana na Pingamizi katika mchezo.

(4.2) Akishindwa kutoa Taarifa Rasmi husika kama zinavyoelekezwa kwenye Muongozo wa Kamishna kwa Msimu husika au Taarifa ya mchezo ya Kamishna kwa usahihi na ukweli ikiwemo taarifa ya mchezaji bora wa mchezo husika na taarifa ya Mapato, au akishindwa kuwasilisha taarifa ya mchezo aliosimamia ndani ya saa 24 (*ishirini na nne*) baada ya mchezo kumalizika, au akibainika kushirikiana na mwamuzi kuandika taarifa ya mchezo kwenye maudhui ya taarifa *(ukiondoa ulinganisho wa usahihi wa kadi, magoli, mabadiliko ya wachezaji na muda)*, au akishindwa kutaarifu matukio mengine yaliyotokea kuhusiana na mchezo husika, au akitumia uongo au udanganyifu au taarifa yake isiyokuwa sahihi.

(4.3) Atakayebainika kuchelewa au kushindwa kufika kwenye kikao cha maandalizi ya mchezo au mchezoni, au kushindwa kufika kwenye mchezo kiasi cha kusababisha ratiba ya Makamishna kubadilishwa au mchezo kuchezwa bila Kamishna pasipo kutoa taarifa inayokubalika na kwa wakati, au atakayebainika kutumia kilevi cha aina yoyote wakati wa kikao cha maandalizi ya mchezo *(MCM)* au wakati wa mchezo au kuendesha kikao cha Maandalizi ya mchezo akiruhusu ushiriki wa maofisa wa timu na wengineo wasiohusika.

(4.4) Kamishna atakayebainika kuwa alitoa visingizio visivyokuwa na msingi kukwepa mchezo aliopangwa au kushawishi kuteuliwa na/au kupangwa kwa njia yoyote ile.

(4.5) Kamishna akishindwa kufanyia kazi pingamizi la mchezo lililowasilishwa kwake, kwa kutafuta ushahidi wa kusaidia maamuzi ya malalamiko husika.

(4.6) Kamishna atakayeondolewa au kufungiwa kwa kipindi zaidi ya miezi sita (6) hatajumuishwa kwenye orodha ya Makamishna wa Ligi Kuu msimu unafuata.

(4.7) Kamishna atakayeshindwa kutoa taarifa sahihi za matukio ya vurugu ikiwemo mwamuzi kushambuliwa na kupigwa, kwa kuainisha ipasavyo wahusika.

(4.8) Atakayeshindwa kushughulikia jambo jingine lolote lililo kwenye mamlaka yake au kushindwa kutekeleza ipasavyo maelekezo ya Utatuzi wa tatizo kutoka TPLB.

(4.9) Akishindwa kutekeleza ipasavyo Taratibu kama zinavyoelekezwa kwenye Muongozo wa kamishna kwa msimu husika.

## Kanuni : 45 Udhibiti kwa Mtathimini Waamuzi

(1) Mtathimini Waamuzi wa Ligi Kuu anawajibika kujiheshimu, kuwa makini na kushughulikia masuala yote ya mchezo ipasavyo na kuyatolea taarifa kwa kutumia fomu maalum kwa ukweli na umakini ili kusaidia Kuimarisha sekta ya Uamuzi na Waamuzi.

(2) Mtathimini wa waamuzi anapaswa kuwa mwanachama hai wa Chama cha Waamuzi (FRAT) Taifa.

(3) Mtathimini Waamuzi wa Ligi Kuu anaweza kufikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF kwa makosa yoyote yaliyotokana na mchezo wa kirafiki aliosimamia uliohusisha timu ya/za Ligi Kuu au za Mashindano mengineyo.

(4) Mtathimini Waamuzi Atakayebainika kuwa amedai Rushwa au amepokea/ametoa Rushwa au kuhusika na mpango/matendo yoyote yanayoashiria Rushwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kabisa kutoa taarifa ya Rushwa au kwa wakati, au kutoa taarifa ya mpango wa Rushwa inayotia mashaka atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(5) Mtathimini Waamuzi anaweza kuadhibiwa kwa Onyo au Karipio au Kufungiwa kati ya miezi mitatu mpaka miaka mitatu au kuondolewa kwenye ratiba ya Ligi Kuu au kuondolewa kwenye Orodha inayotambuliwa na TFF endapo atabainika au kuthibitika kufanya katika yafuatayo:

4.1 Akishindwa kuwasilisha Taarifa ya Mtathimini Waamuzi kwa usahihi na ukweli, au akishindwa kuwasilisha taarifa ya mchezo aliosimamia ndani ya saa 24 (ishirini na nne) baada ya mchezo kumalizika, au akibainika kushirikiana na mwamuzi kuandika taarifa ya mchezo kwenye maudhui ya taarifa *(ukiondoa ulinganisho wa usahihi wa kadi, magoli, mabadiliko ya wachezaji na muda)*, au akishindwa kutaarifu matukio mengine yaliyotokea kuhusiana na mchezo husika, au akitumia uongo au udanganyifu au taarifa zisizo sahihi kwenye taarifa yake.

4.2 Atayashindwa kutekeleza majukumu yanayowahusu Waamuzi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu.

4.3 Mtathimini Waamuzi atakayebainika kuwa alitoa visingizio visivyokuwa na msingi kukwepa mchezo aliopangwa au kushawishi kuteuliwa na/au kupangwa kwa njia yoyote ile.

4.4 Mtathimini Waamuzi atakayeondolewa au kufungiwa kwa kipindi zaidi ya miezi sita (6) hatajumuishwa kwenye orodha ya Watathimini Waamuzi wa Ligi Kuu msimu unafuata.

4.5 Mtathimini/Mkufunzi Waamuzi ambaye hajateuliwa kwa mchezo husika endapo ataingilia Utaratibu wa mchezo kwa namna yoyote au kushirikisha waamuzi katika mambo ambayo hayajapangwa kama sehemu ya mchezo husika

atachukuliwa hatua bila kujali kuwa sio afisa husika kwa mchezo husika.

## Kanuni : 46 Udhibiti kwa Makocha na Maofisa Wengine wa Ufundi

(1) Kocha (Coach) au ofisa mwingine wa ufundi wa Timu ya Ligi Kuu ataadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi kutokana na makosa atakayofanya kwenye michezo ya Ligi Kuu ya timu yake au Mchezo wa Kirafiki wa Timu yake au Mchezo wowote Unaotambuliwa timu yake ilioshiriki.

(2) Kocha *(coach)* yeyote au ofisa mwingine wa ufundi atakayefanya jambo lolote kati ya haya yafuatayo ataadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hii kama inavyoelekezwa ifuatavyo:

2.1 Akimshambulia mwamuzi, mchezaji au kiongozi yeyote, kwa maneno au vitendo, kabla, wakati au baada ya mchezo, atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano (500,000/-) mpaka milioni mbili (2,000,000) na/au kufungiwa michezo isiyopungua mitatu (3), bila ya kujali adhabu yoyote iliyotolewa na mwamuzi kiwanjani.

2.2 Akitoa kauli au ishara inayoashiria au kushawishi shari kabla, wakati au baada ya mchezo atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano (500,000/-) mpaka milioni moja (1,000,000) na/au kufungiwa michezo isiyopungua mitatu *(3)*.

2.3 Akibainika kuwa anadai Rushwa au amepokea/ametoa Rushwa au kuhusika na matendo yoyote yanayoashiria Rushwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kabisa kutoa taarifa ya mpango wa Rushwa kwa wakati au inayotia mashaka, au kutoa taarifa *(itakayohitajika)* ya mchezo isiyo sahihi kwa makusudi atafungiwa maisha.

2.4 Akijishirikisha na vitendo vyovyote vile vinavyoashiria imani za uchawi au ushirikina atatozwa faini kati ya shilingi milioni moja (1,000,000) na milioni kumi (10,000,000) na/au kufungiwa michezo isiyopungua mitatu (3).

2.5 Akifanya kitendo chochote ambacho ni kinyume cha maadili ya mpira wa miguu na/au taaluma ya ukocha wa mpira wa miguu kama vile kusimamia benchi la ufundi katika mchezo akiwa amelewa atafungiwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au/na faini ya shilingi milioni moja (1,000,000)

2.6 Akibainika kughushi saini ya mchezaji au kufanya tendo lolote kwa lengo la kukamilisha zoezi la usajili kwa udanganyifu atafutwa katika orodha ya waalimu, leseni yake itatwaliwa na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

2.7 Akibainika kusababisha timu kutofika uwanjani na kukosa mchezo, baada ya kuhudhuria kikao cha maandalizi, atatozwa faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* na

kufungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili *(12)*.

2.8 Akibainika kusababisha au kuhamasisha vurugu au kugomea mpaka kupelekea mchezo kuvunjika atafungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili na faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)*

2.9 Akithibitika kutoa shutuma, kejeli au kushambulia mwamuzi wa mchezo, msimamizi, TPLB au TFF kwenye vyombo vya habari

atafungiwa kushiriki mechi tatu mpaka sita na/au kutozwa faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* mpaka milioni mbili *(2,000,000)*.

2.10 Akithibitika kumchezesha mchezaji ambaye ni batili kiusajili au ambaye usajili wake haujathibitishwa na TFF atafungiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja na faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)*.

2.11 Kocha atakayetolewa kwa kadi nyekundu na mwamuzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu atafungiwa kuiongoza timu yake kwenye vyumba vya kuvalia na benchi la ufundi katika michezo mitatu (3) inayofuatia ya timu yake na kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja (1,000,000/-).

2.12 Kocha/Kiongozi wa Ufundi atakayeonywa kwa kadi ya njano na mwamuzi kwenye michezo miwili ya Ligi Kuu atafungiwa kuiongoza timu yake kwenye benchi la ufundi wakati wa mchezo katika mchezo mmoja unaofuatia wa timu yake.

2.13 Kocha atakayekataa kuhojiwa na vyombo vya habari kwenye mchezo wa Ligi Kuu baada ya kutakiwa kufanya hivyo na maofisa wa mchezo atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

2.14 Meneja wa timu na Kiongozi yeyote atakayebainika kushawishi, kuongoza au kushindwa kuzuia timu kutotumia chumba cha kubadilishia nguo atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja (1,000,000/-) na kufungiwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja.

## Kanuni : 47 Udhibiti kwa Viongozi

(1) Kanuni hizi za Ligi Kuu zitadhibiti mienendo ya Viongozi wa ngazi Mbalimbali kuhusiana na nafasi zao katika Uendeshaji wa Ligi Kuu kutokana na Uvunjifu wa Kanuni katika Utekelezaji wa Majukumu kwenye Ligi Kuu.

(2) Kiongozi akibainika kudai, kupokea/kutoa Rushwa au kuhusika na vitendo vinavyoashiria Rushwa ikiwa ni pamoja na kushawishi Rushwa kwa waamuzi au wachezaji wa timu yoyote au kuthibitika kuhusika na masuala ya Rushwa kwa namna yoyote atafikishwa

kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(3) Akimshambulia Mwamuzi, mchezaji au kiongozi mwingine yoyote, kwa maneno au vitendo, kabla, wakati au baada ya mchezo atafungiwa kwa kipindi kisichozidi miezi sita na faini ya shilingi laki tano *(500,000/-)* mpaka milioni mbili *(2,000,000)*.

(4) Akifanya kitendo chochote kinachoashiria imani ya uchawi/ushirikina atafungiwa kwa kipindi cha miezi sita na faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* mpaka milioni kumi *(10,000,000)*.

(5) Akifanya kitendo chochote ambacho ni kinyume cha maadili ya uongozi wa mpira wa miguu kama vile kuhudhuria kikao cha maandalizi ya awali ya mchezo husika/au kusimamia shughuli za mchezo husika akiwa amelewa atafungiwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili *(12)*.

(6) Akishindwa kutoa taarifa zinazohitajika TFF kwa mujibu wa maagizo husika atafungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu *(3)*.

(7) Akitoa taarifa isiyo sahihi kiasi cha kupotosha maamuzi ya TFF atafungiwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili *(12)*.

(8) Akitoa matamshi au ishara za matusi dhidi ya mashabiki, akitoa matamshi, ishara za matusi yenye nia ya kumdhalilisha kiongozi mbele ya jamii awe

wa TFF, Klabu au Taifa atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(9) Kiongozi atakayebainika kushindwa/kukaidi kutii maamuzi au maagizo ya TFF/TPLB atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(10) Ni marufuku kwa Kocha/kiongozi wa Timu/Klabu kushutumu au kutoa matamshi/maandiko/picha/video kwa lengo la kumkejeli au kumshutumu au kumkashifu au kumdhalilisha Mwamuzi yoyote wa mchezo/kiongozi wa TFF/FA (M)/TPLB kwenye vyombo vya habari na mahali pengine popote. Kiongozi atakayekiuka atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(11) Kiongozi akibainika kuhudhuria kikao cha maandalizi ya mchezo kwa kujisingizia cheo kisicho kuwa chake atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(12) Uongozi ukibainika kughushi saini ya mchezaji kwa lengo la kukamilisha zoezi la usajili kwa udanganyifu, atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(13) Kiongozi akibainika kutoa taarifa au nyaraka zisizo sahihi au za udanganyifu kwa TFF/TPLB kwa lengo la kufanikisha usajili wa mchezaji au jambo lolote lililo na masharti maalum atafikishwa

kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(14) Kiongozi atakayebainika kusababisha timu kutofika uwanjani na kukosa mchezo, baada ya kuhudhuria kikao cha maandalizi, atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(15) Akibainika kusababisha au kuhamasisha vurugu au kugomea mpaka kusababisha mchezo kuvunjika atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(16) Akibainika kushiriki mpango wa kupanga matokeo ya mchezo atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(17) Akibainika kushawishi, kupotosha au kuzuia maamuzi/utekelezaji wa maamuzi ya TFF/TPLB, atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(18) Kiongozi yeyote atakayeweka saini ya uongo kwa madhumuni yoyote yale au atakayetoa taarifa zisizo sahihi na kupotosha vyombo vingine katika maamuzi yake kuhusiana na usajili na uhamisho atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(19) Kiongozi atakayekataa au kukwepa bila sababu ya msingi kusaini fomu/mkataba ya/wa usajili kwa madhumuni ya uhamisho atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(20) Msimamizi wa kituo atakayeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwemo kushindwa kutuma fedha na taarifa za fedha za kituo chake kwa TFF/TPLB atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(21) Kiongozi yeyote mwingine wa Benchi la Ufundi la Timu ya Ligi Kuu tofauti na Kocha Mkuu atakayetolewa kwenye Benchi la Ufundi kwa Kadi nyekundu atafungiwa kuiongoza timu yake kwenye Benchi la Ufundi wakati wa mchezo kwenye mechi tatu zinazofuatia za timu yake na kutozwa faini isiyopungua shilingi laki tano *(500,000/-)*.

(22) Kiongozi yeyote mwingine wa Benchi la Ufundi la Timu ya Ligi Kuu tofauti na Kocha Mkuu atakayeonywa kwa kadi ya njano kwenye michezo miwili ya timu yake atafungiwa kuiongoza timu yake kwenye Benchi la Ufundi wakati wa mchezo kwenye mechi moja inayofuatia ya timu yake.

(23) Kiongozi yoyote atakayekiuka masharti ya msingi ya mkataba wa usajili wa mchezaji wa klabu nyingine, au masharti ya kanuni hizi kuhusu mchezaji wa klabu nyingine mwenye mkataba (kanuni 74:(9,10) atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* au/na kufungiwa kipindi kisichopungua miezi sita *(6)*.

## Kanuni : 48 Udhibiti kwa Klabu

(1) Klabu ina wajibu na jukumu la kuhakikisha kuwa wachezaji, viongozi, wanachama na wapenzi wake wanajiheshimu na hawajihusishi na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu kama vile matusi, vitisho, vurugu, vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina na vitendo vyovyote vingine visivyokuwa vya kimichezo kwenye viwanja vya michezo. Klabu ambayo mashabiki/wachezaji/viongozi wake watafanya vitendo hivyo itatozwa faini ya shilingi Milioni tano (5,000,000/-). Kwa makosa ya kujirudia, faini itatozwa kati ya shilingi milioni kumi (10,000,000) na milioni ishirini (20,000,000).

(2) Shabiki atakayekamatwa akitoa matusi, vitisho, vurugu, kuashiria imani za uchawi/ushirikina na vyovyote vingine visivyokuwa vya kimichezo atachukuliwa hatua za kisheria na atakayepatikana na hatia atafungiwa kuingia uwanjani kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu *(3)* na kisichozidi miezi kumi na miwili *(12)*.

(3) Klabu pia zitawajibika kulipa gharama za matibabu na kulipa gharama za mali zilizoharibika kwa waathirika wa vurugu za washabiki wake zitakazofanyika kabla, wakati au baada ya mchezo.

(4) Klabu itapoteza mchezo ambao utathibitika kuvunjika kutokana na vurugu za washabiki wake.

(5) Klabu zinatakiwa zihakikishe viongozi wa klabu zao husika waliosimamishwa na TFF kujishughulisha na uongozi wa klabu wanatii adhabu zao na kuzitekeleza. Klabu ambayo itaruhusu viongozi wake waliosimamishwa kujishughulisha na masuala ya uongozi ndani ya kipindi cha adhabu kuendelea na shughuli hizo, itafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(6) Klabu itakayoshindwa kupeleka timu uwanjani itaadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 31 kuhusu kutofika uwanjani. Kiongozi aliyeshiriki kutopeleka timu uwanjani atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(7) Iwapo klabu imeshindwa kulipa faini iliyotozwa, haitaruhusiwa kushiriki Ligi katika ngazi ilipo.

(8) Timu yoyote itakayomchezesha mchezaji aliye chini ya adhabu ya kufungiwa/kusimamishwa au ambaye ametakiwa kulipa faini kwa maelekezo maalum na hajalipa kwa mujibu wa Kanuni hii itapoteza mchezo huo na timu pinzani itapewa ushindi.

(9) Kila Klabu inalazimika kuheshimu Mikataba ya Udhamini inayowekwa na TFF, timu itakayoshindwa kutekeleza masharti ya mikataba ya wadhamini iliyoelekezwa ikiwemo kuvaa na kuheshimu matangazo ya udhamini itatozwa faini ya shilingi milioni tano *(5,000,000/-)* kwa kila mchezo itayokiuka na inaweza

kuchukuliwa hatua zaidi ikiwemo kupoteza sifa ya kushiriki Ligi Kuu na kufungiwa endapo itaendelea kukaidi.

(10) Timu ambayo wachezaji wake wataoneshwa kadi zaidi ya tano katika mchezo mmoja itatozwa faini ya shilingi laki tano *(500,000/-)*.

(11) Klabu itakayomchezesha mchezaji anayetumikia adhabu ya kuoneshwa kadi tatu *(3)* za njano au kadi nyekundu kwa mujibu wa kanuni ya 41:2(2.1 – 2.6) itapoteza mchezo na timu pinzani itapewa ushindi wa pointi tatu *(3)* na magoli matatu *(3)*, endapo klabu haina uhakika au inataka taarifa ya idadi ya kadi zake itaomba kwa maandishi toka TPLB.

(12) Endapo mchezaji ameshiriki kucheza mchezo wa Ligi Kuu na baadae kugundulika usajili wake ulikuwa na kasoro baada ya kuthibitishwa na TFF kwa taarifa ambazo TFF haikuzijua kabla na hakuwa amewekewa pingamizi la usajili, timu husika itatozwa faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* kwa kila mchezo aliocheza, matokeo ya uwanjani yatabaki kama yalivyo.

(13) Klabu inatakiwa kuhakikisha kuwa faini yoyote inayoihusu, kocha, kiongozi au mchezaji wa timu yake inalipwa kama ilivyohitajika na endapo haitalipwa kwa masharti yaliyowekwa ya kanuni hizi wahusika hawataruhusiwa kushiriki shughuli yoyote katika klabu na timu mpaka faini itakapolipwa.

(14) Timu haitaruhusiwa kucheza mchezo wake unaofuata endapo imeshindwa/inakaidi kulipa faini iliyotozwa ikiwa imekwishaamriwa kulipa faini hiyo, na endapo timu itazuiliwa kucheza mchezo husika itakuwa imekosa kucheza mchezo mmoja wa ratiba ya Ligi na hivyo itakabiliwa na adhabu kwa mujibu wa Kanuni ya 31:1(1.3) ya Ligi Kuu.

(15) Viongozi wa timu ya Ligi Kuu itakayocheza mchezo wa kirafiki ambao hautambuliwi na TFF/TPLB au FA(M) watafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(16) Viongozi wa timu itakayoshindwa bila sababu za msingi/itakayokaidi kushiriki mashindano baada ya kuteuliwa na TFF kutokana na nafasi yake kwenye Ligi Kuu au vinginevyo, watafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(17) Timu yoyote inaposhindwa, kukaidi au kuchelewa kulipa malipo inayoamriwa kulipa na TFF/TPLB inaweza kukatwa malipo hayo na

TFF/TPLB kutoka kwenye chanzo chake chochote cha fedha kilicho kwenye mamlaka ya TFF/TPLB.

(18) Viongozi wa klabu ambayo itashindwa au kukaidi kutii maagizo/maamuzi au utekelezaji wa maamuzi ya TFF/TPLB watafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

(19) Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayoanza msimu mpya na kucheza mchezo wa Ligi bila kuwa na kocha mwenye ujuzi kwa kanuni ya 77:(1,2,3) itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na kocha anayehitajika kikanuni, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja.

19:1 Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayopoteza kocha mwenye ujuzi kwa kanuni ya 77:(1,2,3) baada ya kuanza msimu itaruhusiwa kutumia kocha wa muda mwenye sifa za kuwa kocha msaidizi kwa mujibu wa kanuni, kwa michezo isiyozidi sita (6) ya Ligi Kuu.

19.2 Kama itakuwa haijapata kocha mkuu mwenye ujuzi hadi baada ya michezo hiyo sita (6), itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na kocha anayehitajika kikanuni, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja

(20) Timu itakayomchezesha mchezaji ambaye mkataba wake na klabu hiyo umekwisha *(na bila kuwasilisha nyongeza ya mkataba mpya)* au usajili wake haujathibitishwa na TFF kwa timu hiyo kwa/na msimu husika, Mchezaji huyo atahesabika kuwa batili kiusajili na timu hiyo itapoteza mchezo na timu pinzani kupewa pointi tatu (3) na magoli matatu (3).

(21) Timu yoyote itakayokiuka masharti ya msingi ya mkataba wa usajili wa mchezaji wa klabu nyingine, au masharti ya kanuni hizi kuhusu mchezaji wa klabu nyingine mwenye mkataba (kanuni 74(9,10) au itakayokutwa na makosa mengi na makubwa ya udanganyifu kuhusiana na usajili na uhamisho wa wachezaji itakabiliwa na adhabu ya faini na/au zuio la usajili kwa kipindi kimoja mpaka vitatu vya usajili.

(22) Timu iliyomchezesha mchezaji aliyethibitishwa usajili wake lakini aliyebainika kubadili jina kwa nia ya kudanganya au kubainika kutumika udanganyifu mwingine wowote kufanikisha kukamilisha usajili wake au mchezaji aliyebainika usajili wake kuwa na kasoro baada ya kuthibitishwa italipa faini kati ya shilingi laki tano *(500,000/-)* na shilingi milioni tatu *(3,000,000/-)* kwa kila mchezo aliocheza lakini matokeo ya uwanjani hayatobadilishwa.

(23) Timu itakayobainika kumchezesha mchezaji ambaye hajasajiliwa itapoteza mchezo wowote husika, italipa faini ya shilingi laki tano *(500,000/-)* na mchezaji husika atafungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili
*(12)* bila ya kujali kulalamikiwa au la.

(24) Klabu yoyote itakayowasilisha usajili wake ndani ya saa 48 (arobaini na nane) baada ya tarehe ya mwisho itakayotangazwa na TFF itatozwa faini ya shilingi laki tano *(500,000/-)* kwa uchelewaji huo, endapo pia itashindwa

kuwasilisha ndani ya saa hizo 48 (arobaini na nane) baada ya siku ya mwisho iliyotangazwa na TFF, usajili wake hautapokelewa na itapoteza sifa na kutafsiriwa kujiondoa yenyewe kwenye Ligi Kuu na itashushwa daraja.

(25) TFF inaweza kufanya uchunguzi na maamuzi juu ya fujo/vitendo vya mashabiki wa klabu vilivyokithiri au vilivyo na madhara zaidi na/au visivyozingatia utu na haki za binadamu na/au vya kibaguzi siku au wakati kabla ya mchezo, wakati wa mchezo na baada ya mchezo. Adhabu za faini kati ya shilingi milioni mbili *(2,000,000/-)* na shilingi milioni tano *(5,000,000/-)*, klabu kufungiwa kutumia uwanja wake wa nyumbani au adhabu nyingine stahili na aina ya tukio na wakati.

(26) Timu hairuhusiwi kumtumia katika mchezo wake wowote mchezaji ambaye anatumikia adhabu ya kusimamishwa/kufungiwa. Ukiukwaji wowote utasababisha timu kupoteza mchezo kwa manufaa ya athari inayostahili endapo timu ilikwishapoteza mchezo husika.

(27) Klabu ya Ligi Kuu itakayoshindwa kupeleka timu yake ya Vijana (U20/U17) kwenye Mchezo mmoja wa Mashindano ya Vijana kwa Mujibu wa Taratibu za TFF/TPLB itapigwa faini ya shilingi milioni mbili *(2,000,000/-)* na kupoteza mchezo husika. Endapo klabu hiyo itashindwa tena kupeleka timu yake ya vijana katika mchezo unaofuata, itapigwa tena faini ya shilingi milioni mbili *(2,000,000/-)* na kunyang'anywa pointi tatu za timu yake inayoshiriki katika Ligi ya Wakubwa (Ligi Kuu) na kwa timu yake ya vijana ya Shindano husika la Vijana.

(28) Klabu itakayocheza mchezo wake wa Nyumbani bila ya kuwa na Huduma za Mchezo kama Huduma ya Kwanza, Vijana waokota Mipira, walinzi wa uwanjani, watoa huduma ya kwanza na matayarisho sahihi kwa sehemu ya kuchezea (pitch) itatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano *(500,000/-)*. Endapo klabu kitakuwa na makosa mengi na/au yanayojirudia kuhusiana na Huduma za mchezo itapoteza Haki ya kutumia Uwanja wake wa Nyumbani na kupangiwa kucheza katika uwanja utakaoamuliwa na TPLB.

(29) Kamishna atazuia kuchezwa kwa mchezo mpaka ajiridhishe na uwepo wa Gari la Wagonjwa (Ambulance) uwanjani. Klabu itakayoshindwa kutayarisha na kuwepo kwa Gari la Wagonjwa (Ambulance) itakuwa imesababisha mchezo kutochezwa na hivyo itapoteza mchezo huo na Ushindi kupewa timu pinzani wake kwa mchezo husika.

(30) Timu ikifanya kitendo chochote kinachoashiria imani za kishirikina itatozwa faini ya kati ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* na milioni ishirini *(20,000,000/-)*.

(31) Klabu isiyo na benchi kamili la ufundi itapigwa faini ya shilingi milioni moja *(1,000,000/-)* kwa kila mechi bila kuathiri na kwa mazingatio ya kanuni ya 47:19.

(32) Klabu ya Ligi Kuu inatakiwa kuajiri watendaji kwa nafasi za Mtendaji Mkuu, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala, Mkurugenzi wa Ufundi, Afisa Habari, Afisa wa Usalama, Meneja Mkuu wa Timu, Daktari na watendaji wengine wenye sifa na vigezo kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Leseni za Klabu.

(33) Klabu ya Ligi Kuu itakayoshindwa kufuata na kutekeleza masharti yote yaliyoainishwa kwenye Kanuni ya Leseni za Klabu, itaadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(34) Klabu ambayo itashindwa au kukaidi kushiriki sherehe za kukabidhi kikombe cha ubingwa, medali au tuzo nyingine yoyote inayotolewa na TFF/TPLB kutokana na nafasi ya klabu husika kwenye Ligi au shindano ililoshiriki, itatozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000/-) na viongozi wake wakuu watafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu TFF.

(35) Klabu inatakiwa kufuata utaratibu wa timu kutumia chumba cha kuvalia kama ulivyoelekezwa kwenye kanuni 17.20. Timu haitoruhusiwa kutumia chumba kabla ya muda uliopangwa, kuingia kwenye chumba cha timu pinzani kwanamna yoyote au kuweka kitu chochote au kufanya mabadiliko ya chumba bila ruhusa ya wasimamizi wa mchezo. Klabu itakayokiuka itatozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000/-). Pia viongozi wakuu wa klabu husika watafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu TFF kwa hatua zaidi.

(36) Timu itakayotumia sehemu kama ndani ya gari, jukwaani, chini ya mti, eneo la benchi la ufundi, nje ya uwanja au eneo lingine lolote tofauti na vyumba rasmi vya kuvalia kama ilivyoelezwa kwenye kanuni 17.20 itatozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000/-) na kukatwa Pointi tano (5) kwenye msimamo wa Ligi. endapo kosa litakuwa la kujirudia TFF/TPLB itatoa adhabu zaidi kadiri itakavyoona inafaa kwa kuzingatia uzito na mazingira ya kosa na viongozi wa juu wa klabu watafikishwa Kamati ya Nidhamu kwa hatua zaidi.

(37) Timu itakayoingia uwanjani (Stadium) kwa kuruka ukuta ama kuruka uzio wa ndani unaotenga watazamaji na kiwanja (pitch) ama kupita mlango usio rasmi itatozwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000/-) na endapo kosa litakuwa la kujirudia timu husika itakatwa pointi 2 (mbili) na faini ya shilingi milioni mia moja (100,000,000/-).

## Kanuni : 49 Udhibiti kwa Maofisa Habari wa Klabu

1. Kanuni hii imeundwa kwa lengo la kulinda taswira ya mashindano yote yaliyo chini ya TFF, klabu, waamuzi, wachezaji, na viongozi dhidi ya habari za uzushi, uchochezi, na kauli zinazoweza kuleta mvurugano au kushusha hadhi ya mpira wa miguu nchini kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, na mitandao binafsi ya maofisa habari.
2. Ni marufuku kwa Ofisa Habari kutoa kauli zinazochochea vurugu kati ya mashabiki, klabu, au kashfa kulingana na ukabila, ukanda,

udini, au jinsia.

3. Ni marufuku kwa Ofisa Habari kutumia lugha ya matusi, kashfa, dhihaka, au udhalilishaji dhidi ya TFF/TPLB na viongozi wake, klabu, viongozi, wachezaji au wadhamini.

4. Hairuhusiwi kwa Ofisa Habari kumtuhumu mwamuzi au ofisa wa mchezo ama kumjadili kuhusu tuhuma za kupokea rushwa, kupanga matokeo, au kuwa na upendeleo wa makusudi bila kuwa na ushahidi wa kisheria uliothibitishwa na Kamati ya Maadili ya TFF au mamlaka za kisheria.

5. Ofisa Habari haruhusiwi kusambaza taarifa za uongo, uzushi, au tetesi zenye nia ya kuharibu taswira ya klabu, ligi au mpira wa miguu kwa ujumla.

6. Ofisa Habari atawajibika binafsi kwa taarifa zozote hasi anazozitoa kuhusu mpira wa miguu.

7. Kwa Ofisa Habari atakayekiuka Kanuni hii atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni kumi (10,000,000/-) au/ na kufungiwa kipindi kisichopungua miezi sita (6).

## Kanuni : 50 Adhabu za Klabu

(1) Klabu yoyote inaweza kutoa adhabu inayostahili na kwa mujibu wa utaratibu dhidi ya mchezaji wake yeyote itakayotumika ndani ya nchi tu. Klabu haina mamlaka ya kumfungia mchezaji wake nje ya nchi.

(2) Adhabu zote zitakazotolewa na klabu ni lazima zithibitishwe na TFF kabla hazijaanza kutekelezwa. TFF inaweza kufuta, kupunguza au kuongeza adhabu ikiwa ni pamoja na kumfungia mchezaji husika nje ya nchi.

(3) Klabu haitakuwa na mamlaka ya kumfungia mchezaji kwa kipindi kinachozidi msimu wa ligi husika au kwa mchezaji mwenye mkataba, zaidi ya kipindi cha mkataba wake na klabu hicho.

(4) Kabla klabu haijatoa adhabu yoyote ni lazima mchezaji anayehusika apewe nafasi ya kujitetea.

(5) Klabu itakayotoa adhabu kwa mchezaji wake na kutuma taarifa hiyo TFF ili adhabu hiyo ithibitishwe, italazimika kutuma vielelezo vyote vinavyohusika ikiwa ni pamoja na muhtasari wa kikao kilichotoa adhabu hiyo.

(6) Endapo mchezaji hajaridhika kutokana na adhabu aliyopewa na klabu yake anaweza kukata rufaa kwa TFF kabla adhabu yake haijathibitishwa na TFF.

(7) Adhabu yoyote ya klabu kwa Mchezaji ni lazima itolewe na Chombo cha Klabu kilicho na mamlaka ya kufanya hivyo.

**Kanuni : 51** **Dawa Haramu**

(1) Hairuhusiwi kwa mchezaji kutumia dawa zilizopigwa marufuku na Shirika la Kimataifa la Kupambana na Dawa Haramu michezoni (World Anti Doping Agency-WADA) wakati wote wa ushiriki wake katika mpira wa miguu.
Adhabu kwa ukiukwaji wowote zitatolewa kwa mujibu wa Kanuni za WADA.

(2) Mchezaji yeyote atakayetakiwa kufanya vipimo vya kubaini matumizi ya dawa za kulevya au kuongeza nguvu akiwa mchezoni anawajibika kufanya hivyo, endapo atagundulika kuwa anatumia dawa za kulevya au kuongeza nguvu au akikataa kufanya vipimo hivyo atafungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili (12).

(3) Kiongozi, afisa wa ufundi au mtumishi yeyote wa klabu atakayekutwa na dawa zisizoruhusiwa mchezoni au kifaa chochote kitakachobainika kusaidia matumizi ya dawa au atakayebainika kushawishi matumizi ya dawa hizo au atakayeficha ushahidi au kukataa kutoa ushirikiano juu ya uchunguzi au kumsaidia mshukiwa kukwamisha ushahidi atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili (2,000,000/-) na kufungiwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili (12) au vyote kwa pamoja.

(4) Kila klabu ina wajibu wa kuhakikisha kuwa wachezaji wake hawatumii dawa zisizoruhusiwa michezoni. Pia klabu itakuwa na wajibu wa kutoa taarifa kwa TFF/TPLB haraka iwezekanavyo wakati wowote itakapopata taarifa au kubaini uwepo wa viashiria vya matumizi ya dawa hizo kwa mchezaji au wachezaji wake.

# SURA: XII

## HADHI YA WACHEZAJI



## SURA : XII HADHI YA WACHEZAJI

### Kanuni : 52 Wachezaji wa Ridhaa na Kulipwa

(1) Wachezaji wanaoshiriki katika Ligi Kuu ni wachezaji wa ridhaa na/au wa kulipwa.

(2) Mchezaji wa kulipwa ni yule mwenye mkataba wa maandishi na klabu na analipwa zaidi ya gharama halisi anazoingia kutokana na shughuli zake za soka. Wachezaji wengine wote tofauti na hivyo, wanahesabiwa kuwa ni wa ridhaa.

### Kanuni : 53 Kupata Upya Hadhi ya Ridhaa

(1) Mchezaji aliyesajiliwa kama mchezaji wa kulipwa hawezi kusajiliwa tena kama mchezaji wa ridhaa mpaka zipite angalau siku thelathini (30) baada ya mchezo wa mwisho aliocheza kama mchezaji wa kulipwa.

(2) Hakuna fidia inayolipwa kwa kupata upya hadhi ya ridhaa. Iwapo mchezaji anasajiliwa upya kama wa kulipwa katika kipindi cha miezi thelathini (30) ya kurudishiwa hadhi ya ridhaa, klabu yake mpya italipa fidia ya mafunzo kwa mujibu wa ibara ya 20 ya kanuni za FIFA.

### Kanuni : 54 Kuacha Shughuli

(1) Wachezaji wa kulipwa wanaomaliza muda wao wa mkataba na wachezaji wa ridhaa wanaomaliza muda wao, watabaki kuwa wamesajiliwa TFF ambapo ndipo klabu yao waliyochezea mwisho kwa kipindi cha miezi thelathini (30).

(2) Kipindi hiki kinaanza siku ambayo mchezaji atachezea klabu mara ya mwisho katika mchezo rasmi.

### Kanuni : 55 Wachezaji Wasiosajiliwa

(1) Iwapo mchezaji asiyesajiliwa na TFF anacheza mechi ya mashindano, mchezaji huyo atahesabika kucheza kinyume cha sheria. Bila kuathiri hatua yoyote inayotakiwa kurekebisha athari inayosababishwa na kucheza huko, adhabu na vikwazo vitawekwa kwa mchezaji na/au klabu. Haki ya kutoa adhabu na kuweka vikwazo hivyo kimsingi iko mikononi mwa TFF.

(2) Mchezaji yoyote ambaye hakusajiliwa na klabu yake na ambaye hakuhamishwa kwenda klabu nyingine yoyote katika kipindi hicho cha Msimu cha Usajili atahesabika kuwa huru.

### Kanuni : 56 Kuachwa Huru

Kila klabu italazimika kuwasilisha TFF kwa maandishi, majina ya wachezaji inaowaacha huru au watakaositisha mikataba yao kuwa huru katika usajili wa msimu ujao wa Ligi Kuu unaoanza katika muda

utakaotangazwa na TFF, na klabu italazimika kumpa taarifa ya maandishi mchezaji/wachezaji husika

## Kanuni : 57 Wachezaji Waliopandishwa

(1) Klabu inawajibika kusajili wachezaji wasiopungua watatu (3) kutoka miongoni mwa wachezaji wake wa timu za Vijana (U20/U17) ambao walithibitishwa na TFF katika usajili wa klabu husika msimu uliopita kama wachezaji waliopandishwa. Klabu inaweza kusajili (kupandisha) wachezaji wasiozidi kumi (10) tu kwa msimu.

(2) Mchezaji yeyote wa timu ya vijana (U20/U17) ambaye hakusajiliwa na kuthibitishwa na TFF katika msimu uliopita kwa klabu husika hataruhusiwa kusajiliwa katika timu ya kwanza ya klabu kama mchezaji aliyepandishwa au huru.

## Kanuni : 58 Wachezaji Huru

(1) Mchezaji yeyote ambaye hakusajiliwa na klabu yoyote ya daraja lolote katika msimu uliopita atakuwa huru, hatahitaji uhamisho wala kulipiwa ada yoyote ya uhamisho.

(2) Mchezaji yeyote ambaye klabu yake imemuacha huru kwa mujibu wa Kanuni ya 54 au imesitisha mkataba wake au mkataba wake umemalizika atakuwa huru, hatalipiwa ada yoyote ya usajili.

(3) Mchezaji wa timu ya vijana ya klabu husika anapopandishwa timu ya kwanza ya klabu yake atakuwa huru hatahitaji uhamisho wala kulipiwa ada yoyote ya uhamisho.

## Kanuni : 59 Wakala wa Mchezaji

(1) Mchezaji yeyote wa Ligi Kuu anaweza kutambulisha mwakilishi (Wakala mwenye leseni ya FIFA) wake ambaye anaweza kushughulikia jambo lolote linalomhusu mchezaji husika aidha kwa kwenda au kwa uwakilishi. Mchezaji na Wakala watatakiwa kuwasilisha Mkataba wa makubaliano baina yao.

(2) Wakala wa Mchezaji anawajibika kuwa na Mkataba wa Makubaliano baina yake na mchezaji uliothibitishwa na TFF unaoainisha wajibu na haki za kila upande ambapo Wakala wa Mchezaji ni lazima awe mwenye leseni ya Uwakala aliyefuzu kwa mujibu wa taratibu za TFF na FIFA na anayehodhi Leseni ya Uwakala iliyo hai.

(3) Mchezaji atawajibika kumtambulisha Wakala wake kwa klabu yake wakati akiingia mkataba na klabu husika kabla ya utambulisho huo na nyaraka ambatanishwa kuwasilishwa TFF. TFF itathibitisha na kumsajili wakala huyo.

# SURA: XIII
# UHAMISHO WA WACHEZAJI



## SURA : XIII UHAMISHO WA WACHEZAJI

### Kanuni : 60 Wachezaji wa Kuhamishwa

(1) Mchezaji yeyote ambaye hajamaliza mkataba au mkataba wake haujasitishwa na klabu yake, au ambaye hajamaliza msimu atakaposajiliwa na klabu nyingine ni lazima ahamishwe kuanzia ngazi ya klabu.

(2) Mchezaji aliyerudi Tanzania baada ya kumaliza mkataba wake nje ya nchi hatakuwa huru mpaka atakapokamilisha taratibu za uhamisho wa kimataifa.

(3) Mchezaji kutoka Zanzibar lazima Uhamisho wake uthibitishwe na ZFF.

(4) Mchezaji wa klabu inayoshiriki ligi daraja la chini aliyemaliza msimu uliopita anaposajiliwa na klabu ya Ligi Kuu atafanyiwa uhamisho kuanzia ngazi ya klabu, wilaya, mkoa na TFF.

(5) Mchezaji wa timu za vijana (U20) anapohitajika kuhama anawajibika kufuata taratibu za uhamisho kwa mujibu wa kanuni hizi.

### Kanuni : 61 Uhamisho

(1) Mchezaji anaweza kuhama/kuhamishwa kutoka klabu moja hadi nyingine kwa madhumuni ya kusajiliwa baada ya ligi kumalizika na/au katika kipindi cha usajili wa katikati ya msimu.

(2) Klabu inayotaka kumsajili mchezaji aliyesajiliwa au aliye na mkataba uliobakisha muda zaidi ya miezi sita (6) na klabu nyingine, italazimika kuafikiana na klabu yake kuhusu uhamisho wake kabla ya kukubaliana na kumsajili mchezaji huyo. Klabu inawajibika kuheshimu masharti ya msingi ya mkataba wa mchezaji wa klabu nyingine.

(3) Mchezaji aliyesajiliwa au aliye na mkataba na klabu anaposajiliwa kuhamishwa kwenda klabu nyingine katika kipindi cha usajili wa katikati ya msimu, atajiunga na klabu yake mpya kwa uzingativu wa makubaliano ya maandishi baina ya klabu zinazohusika na uhamisho huo na hataruhusiwa kuchezea klabu yake mpya kwa michezo ya Ligi Kuu mpaka usajili wake umethibitishwa na TFF.

(4) Endapo kiongozi wa klabu anayohama mchezaji amekataa au amekwepa kuidhinisha uhamisho wa mchezaji wa daraja la chini (asiye na mkataba) anayetaka kuihama klabu yake kuhamia Ligi Kuu baada ya msimu wa ligi kwisha, katibu wa FA(W) husika ataidhinisha uhamisho huo baada ya mchezaji aliyeomba kuhama kumthibitishia kwa maandishi kuwa anakusudia kuhamia klabu hiyo mpya lakini katibu wa klabu yake ya sasa anakwepa/hataki kuidhinisha uhamisho wake.

(5) Nakala za barua ya uthibitisho wa mchezaji wa daraja la chini (asiye na mkataba) kwenda kwa Katibu wa FA(W) husika ni lazima

zitumwe pia kwa Katibu wa FA(M) husika na kwa Katibu Mkuu wa TFF.

(6) Pamoja na kupokea nakala ya barua ya uthibitisho kwa mujibu wa kanuni ya 59(4), TFF inaweza kumwita mchezaji huyo kwa mahojiano kuhusiana na uthibitisho alioutoa kabla ya kufikia maamuzi.

(7) Uhamisho na usajili wa wachezaji watoto na vijana walio na umri chini ya miaka kumi na nane (18) utazingatia kanuni za FIFA kwa wachezaji wa umri huo.

(8) Ada za uhamisho wa mchezaji aliyemaliza msimu na asiye na mkataba kutoka daraja lolote kwenda Ligi Kuu na mgawanyo wake kwa mamlaka zinazohusika zitakuwa kama inavyoonekana kwenye jedwali A la uhamisho.

**Jedwali A la Uhamisho.**

| Klabu | TFF | FA (M) | FA (W) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 500,000/- | 100,000/- | 100,000/- | 100,000/- | 800,000/- |

(9) Ada hizi za uhamisho ni kwa wachezaji wasio na mikataba. Kwa klabu yenye mkataba na mchezaji ina haki ya kudai malipo stahili zaidi kwa ajili ya uhamisho toka kwa klabu kinachomtaka mchezaji wake ambapo ada kwa Mamlaka nyingine zitabaki kama zilivyo.

(10) Mchezaji aliye na mkataba au aliyesajiliwa na klabu yoyote na hajamaliza msimu anapotakiwa kuhama, uhamisho wake ni lazima uidhinishwe na klabu yake kwanza kabla ya kupitishwa na FA(W), FA(M) na TFF. Mamlaka nyingine zozote hazitaweza kuidhinisha Uhamisho wa Mchezaji wa aina hii bila Ridhaa na Idhini ya Klabu yake.

(11) Ada za uhamisho kuhamia klabu ya Ligi Kuu kutoka daraja la chini kwa mchezaji mwenye mkataba au aliyesajiliwa na hajamaliza msimu ni kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali B la Uhamisho.

**Jedwali B la Uhamisho.**

| Klabu | TFF | FA (M) | FA (W) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Maelewano | 100,000/- | 100,000/- | 100,000/- | - |

## Kanuni : 62 Uhamisho Zanzibar

(1) Mchezaji wa Ligi Kuu anapotakiwa kuhamia klabu ya Zanzibar atawajibika kupata ruhusa kutoka klabu yake ikiambatana na kuthibitishwa na FA (W) na FA(M) kabla ya kuidhinishwa na TFF.

(2) Ada ya Uhamisho kwa klabu anachotoka mchezaji itatokana na maelewano baina ya klabu husika wakati ada za uhamisho kwa mamlaka nyingine ni kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali C la uhamisho.

(3) Endapo mchezaji anayehamia Zanzibar atakuwa amemaliza mkataba kama mchezaji wa Ligi Kuu na hajasajiliwa na klabu nyingine, uhamisho wake utaidhinishwa na TFF.

(4) Mchezaji kutoka Zanzibar aliyemaliza/kusitisha mkataba wake ambaye anarudi Zanzibar atakuwa huru hatahitaji taratibu yoyote ya uhamisho, TFF inaweza kuitaarifu ZFF juu ya hali ya sasa ya mchezaji huyo baada ya kupata uthibitisho kutoka klabu yake.

**Jedwali C la Uhamisho**

| Klabu | TFF | FA (M) | FA (W) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Maelewano | 100,000/- | 100,000/- | 100,000/- | - |

## Kanuni : 63 Uhamisho Nje

(1) Uhamisho wa kimataifa unaombwa na kutolewa kwa chama cha mpira wa miguu cha kitaifa pekee kw a niaba ya klabu, na si kwa mchezaji au kiongozi wa klabu. Taratibu za mawasiliano ya maombi na utoaji wa hati ya uhamisho wa kimataifa yanafanyika kiofisi kupitia mawasiliano yanayoaminika kiofisi.

(2) Mchezaji yeyote anaruhusiwa kuhamia klabu nyingine nje ya nchi baada ya kupata hati ya uhamisho ya kimataifa.

(3) Kabla TFF haijatoa kibali, mchezaji analazimika kupata idhini ya klabu yake ya hapa nchini baada ya TFF kufanya mawasiliano na klabu hiyo.

(4) Maombi ya kibali cha TFF na idhini yoyote itakayotolewa na klabu ni lazima vifanywe kwa maandishi.

(5) Klabu inayotaka kumhamisha mchezaji na klabu inayohusika na mchezaji huyo watakubaliana kuhusu ada/gharama za uhamisho.

(6) Endapo itatokea kutokubaliana kati ya pande mbili zinazohusika na uhamisho huo kutokana na sababu yoyote ile TFF itatoa uamuzi kwa kuzingatia sheria na kanuni za TFF, CAF na FIFA.

(7) TFF itatambua kumalizika au kuvunjika kwa mkataba wa mchezaji na klabu yake ya nje baada ya Uthibitisho wa Uhamisho katika Mfumo wa Usajili au kupata cheti cha uhamisho wa kimataifa kutoka kwa chama cha soka cha nchi alipokuwa akicheza.

## Kanuni : 64 Wachezaji wa Kigeni

(1) Klabu ya Ligi Kuu inaruhusiwa kusajili wachezaji kumi na wawili (12) wa kigeni kutoka sehemu yoyote duniani (mazingatio kwa kanuni ya 62:4 ya kanuni hizi).

1.1 Klabu inaweza kuwachezesha/ kuwatumia (kuwemo kwenye orodha ya wachezaji wa mchezo kwa siku husika) wachezaji wake wote kumi na wawili (12) wa kigeni katika mchezo mmoja wa Ligi Kuu au Kombe la Shirikisho.

1.2 Klabu hairuhusiwi kusajili zaidi ya golikipa mmoja wa kigeni kwa ajili mashindano yote yaliyo chini ya TFF.

(2) Mchezaji wa kigeni atathibitishwa usajili wake baada ya TFF kuhakiki usahihi wa taarifa zake na kukamilika kwa taratibu za Uhamisho wa

kimataifa na Mazingatio maalum kwa Utimizwaji wa Masharti ya Kisheria kwa wageni.

(3) Mchezaji wa kigeni wa ridhaa anayesajiliwa kwenye Ligi Kuu anaweza kuhamishwa kwa kufuata utaratibu wa uhamisho wa kimataifa kwa wachezaji wa ridhaa.

(4) Mchezaji wa kigeni anayeruhusiwa kusajiliwa kwenye Ligi Kuu ni yule anayecheza katika Timu ya Taifa ya nchi yake au Ligi Kuu au Ligi Daraja la Kwanza ya nchi husika. Mchezaji kutoka Amerika ya Kusini, Ulaya na Asia, lazima awe anacheza angalau kuanzia Ligi Daraja la Pili (kitaifa, kutegemea mfumo kwa nchi husika). Mazingatio ya Daraja mchezaji analocheza kabla ya usajili wake kwenye Ligi ni kwa wakati husika au kipindi kisichozidi miezi sita tokea ameachana na timu yake ya mwisho kwa mchezaji aliye huru.

(5) Mchezaji yeyote wa kigeni anayesajiliwa katika Ligi Kuu atalipiwa ada maalum ya shilingi milioni nane (8,000,000/-) kwa msimu ili usajili wake uweze kuthibitishwa na kuruhusiwa kucheza.

## Kanuni : 65 Hati ya Uhamisho Kimataifa

(1) Maombi ya Hati ya Uhamisho wa Kimataifa (ITC) kwa wachezaji wa kigeni wa kulipwa yatawasilishwa kupitia mtandao wa kompyuta kwa kutumia program maalum ya Mfumo wa Ulinganisho wa taarifa za uhamisho wa mchezaji (transfer matching system - TMS) au Mfumo mwingine wowote Maalum Uliotambulishwa na TFF baada ya klabu zinazohusika na uhamisho wa mchezaji husika kukubaliana nje ya mtandao.

(2) Maombi ya ITC kwa mchezaji wa ridhaa wa kigeni yatawasilishwa kwa barua TFF baada ya klabu zinazohusika na uhamisho wa mchezaji husika kukubaliana. Chama cha mpira wa miguu kinachotoa ITC kwa njia hii kitatuma uhamisho huo moja kwa moja kwa TFF kufuatia maombi ya kufanya hivyo na kupeleka nakala FIFA.

(3) Hati ya Uhamisho wa Kimataifa haihitajiki kwa mchezaji mwenye umri chini ya miaka kumi na mbili (12).

## Kanuni : 66 Uhamisho kwa Mkopo

(1) Mchezaji wa kulipwa anaweza kuhamishwa kwa mkopo kwa klabu nyingine kwa msingi wa makubaliano ya maandishi kati yake na

klabu zinazohusika. Uhamisho huo wa mkopo utafuata sheria zilezile zinazotumika katika uhamisho wa wachezaji, yakiwemo masharti ya fidia ya mafunzo na utaratibu wa mshikamano.

(2) Klabu itakayompokea mchezaji kwa uhamisho wa mkopo haina haki ya kumhamisha mchezaji huyo katika klabu nyingine bila idhini ya maandishi ya klabu iliyomwachia mchezaji kwa mkopo na ya mchezaji husika.


(3) Mchezaji wa Ligi Kuu anaweza kuazimwa kwa mkopo kwa klabu za Ligi Kuu na Championship tu, kipindi cha chini cha kusajili mchezaji anayehamishwa kwa mkopo kitakuwa muda kati ya kipindi kikubwa cha usajili na kipindi cha usajili wa katikati ya msimu.

(4) Klabu isipokee/kutoa zaidi ya wachezaji watano kutoka timu moja. Inaweza kutoa/kupokea idadi yoyote ile ya wachezaji wa mkopo.

(5) Klabu inayomchukua mchezaji kwa mkopo itawajibika kuheshimu makubaliano kati yao.

# SURA: XIV

## USAJILI



## SURA : XIV USAJILI

### Kanuni : 67 Usajili

(1) Mchezaji lazima asajiliwe na Shirikisho la Mpira wa Miguu ili kuchezea klabu kama mchezaji wa kulipwa au wa ridhaa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za FIFA. Ni wachezaji waliosajiliwa tu ndio wanaostahili kushiriki katika soka rasmi. Kwa kujisajili, ina maana mchezaji anakubali kufuata sheria na kanuni za FIFA, TFF, mashirikisho na vyama vya mpira wa miguu.

1.1 Nyaraka za utambulisho zitakazokubaliwa na TFF ili kuthibitisha usajili wa mchezaji wa Ligi Kuu ni pasi ya kusafiria au kitambulisho cha taifa (kwa mchezaji mzawa).

(2) Mchezaji atasajiliwa katika klabu moja tu kwa wakati mmoja lakini anaweza kusajiliwa katika klabu hadi tatu kwa kipindi kati ya tarehe 01 Julai hadi 30 Juni mwaka unaofuata ambapo mchezaji atastahili kuchezea mechi rasmi katika klabu mbili tu.

(3) Klabu zinawajibika kutumia mikataba elekezi iliyotayarishwa na TFF kuhamisha, na kusajili wachezaji wake, mikataba mingine yote haitatambulika.

(4) Usajili wa wachezaji ni suala la kiufundi kama ilivyo kanuni ya 77:4. Kocha Mkuu wa timu atawajibika kutambua wachezaji wanaotakiwa kusajiliwa wakati ambapo Uongozi wa Klabu utafanya kazi ya kukamilisha zoezi la usajili wa wachezaji na kuwasilisha mikataba na nyaraka nyingine TFF kwa wakati uliowekwa. Ni Katibu Mkuu wa Klabu tu atakayetambulika na TFF kwa mawasiliano yote kuhusu usajili.

(5) Klabu ndiyo inawajibika kutangaza wachezaji wanaoachwa, wachezaji wanaohamia na wanaohama pamoja na usajili kamili wa timu yake katika kipindi cha kukamilika kwa usajili wa timu yake.

(6) Kila timu ya Ligi Kuu inatakiwa kusajili wachezaji wasiopungua watatu kutoka miongoni mwa wachezaji wa timu yake ya vijana (U20 au U17) waliothibitishwa Usajili wao na TFF kwa msimu uliomalizika ili usajili wake uweze Kuthibitishwa.

(7) Kutakuwa na Leseni maalum ya usajili wa mchezaji itakayotolewa na TFF ikiwa na taarifa zote muhimu za mchezaji husika. Mchezaji atatumia leseni hiyo kwa utambulisho wakati wa mchezo, mchezaji asiye na leseni au ambaye leseni yake imechafuka, kukunjwa au kufutwafutwa kiasi cha kuathiri uhalisia wake hataruhusiwa kucheza mchezo wa Ligi Kuu.

(8) TFF itatoa maelekezo au mafundisho juu ya mfumo wa kieletroniki utakaotumika kwa ajili ya uhamisho na usajili wa wachezaji kabla ya msimu kuanza na wakati wowote itakapohitajika.

(9) Mchezaji ana uhuru wa kujisajili na Klabu nyingine katika msimu mmoja iwapo kutakuwa na maelewano kati ya Klabu yake na kile kinachotaka kumsajili au atakuwa amemaliza mkataba na klabu yake.

(10) Klabu na Mchezaji wanalazimika kuingia mkataba utakaothibitishwa na TFF pamoja na kutimiza masharti mengine ya usajili na ndipo TFF inaweza kumuidhinisha mchezaji husika kucheza Ligi Kuu.

(11) Katika dirisha dogo la usajili, klabu ambayo ilikamilisha idadi ya wachezaji arobaini (40) katika dirisha kubwa, itaruhusiwa kuondoa na kusajili wachezaji wasiozidi saba (7). Kwa klabu ambayo haikutimiza idadi ya wachezaji arobaini (40) wakati wa dirisha kubwa itaruhusiwa kusajili wachezaji wanaotimiza idadi ya wachezaji arobaini (40) na itaruhusiwa kuondoa na kusajili wachezaji wasiozidi saba (7).

(12) Kila mchezaji wa Ligi Kuu atatakiwa kuwa na namba yake ya kudumu ya jezi ya kuchezea iliyosajiliwa na klabu yake wakati wa maombi ya usajili wa wachezaji. Mchezaji atatakiwa kutumia namba hiyo tu wakati wote katika Ligi Kuu na mashindano mengine rasmi yanayotambuliwa na TFF.

(13) Ukiukaji wowote wa masharti ya usajili ambao haujaainishwa ipasavyo kwenye kanuni hizi bado utastahili vikwazo vinavyofaa au kutozwa kwa faini kati ya shilingi laki tano *(500,000/-)* na shilingi milioni tano *(5,000,000/-),* au/na Zuio la kucheza kwa Mchezaji mpaka Masharti ya msingi kiutaratibu yawe yametimizwa au/na adhabu ya faini/kufungiwa kwa muhusika yoyote endapo kuna makosa binafsi ya kiUtendaji na fidia kwa athari zilizosababishwa na ukiukwaji au/na mapungufu hayo makubwa ya Taratibu za usajili yaliyo na athari.

(14) Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF ndio chombo chenye mamlaka ya kushughulikia masuala ya usajili, kuthibitisha au kutengua usajili wa mchezaji.

(15) TFF inaweza kutoa leseni ya dharura ya mchezaji kabla ya uthibitisho wa usajili wa wachezaji kuwezesha klabu inayowakilisha nchi katika mashindano mengine ya kimataifa kukidhi mahitaji ya usajili wa wachezaji katika mashindano maalum ya kimataifa yaliyo na masharti hayo endapo kuna ulazima wa kufanya hivyo. Leseni hiyo itatolewa kwa kuzingatia uthibitisho wa maelewano ya klabu zinazohusika na uhamisho wa mchezaji husika.

(16) TFF inaweza kuidhinisha/kuthibitisha usajili wa mchezaji wa kigeni wa ridhaa anayekidhi vigezo vya kusajiliwa kucheza Ligi Kuu kwa kutumia utaratibu wa uhamisho wa kimataifa kwa wachezaji wa ridhaa. Uthibitisho huo hauna dhamana yoyote kwa mchezaji husika kwa taratibu nyingine za usajili za mashindano ya ngazi ya klabu ya CAF.

(17) TFF inaweza kutoa waraka maalum kuhusiana na usajili wa watoto na vijana utakaosomeka pamoja na kanuni hizi utakaozingatia kanuni za FIFA kwa usajili na matunzo ya wachezaji walio chini ya miaka kumi na minane (18).

## Kanuni : 68 Vipindi vya Usajili

(1) Wachezaji wanaweza kusajiliwa katika moja ya vipindi vya usajili vya msimu vilivyopangwa na TFF. Kipindi cha kwanza cha usajili kitakuwa wakati wa kuanza msimu, kunaweza kuwa na kipindi cha pili siku chache baada ya Ligi kuanza na kipindi cha tatu kitakuwa katikati ya msimu. TFF itatangaza kuanza na kwisha kwa vipindi vya usajili.

(2) Mchezaji wa kulipwa ambaye mkataba wake umekwisha kabla ya kipindi cha usajili anaweza kusajiliwa nje ya kipindi cha usajili, TFF itahitaji kujiridhisha juu ya kuaminika kwa hali nzima ya kumalizika huko kwa

mkataba na maombi mapya ya usajili yanayokusudiwa, hali hii haitamhusu mchezaji ambaye mkataba wake umesitishwa au umevunjwa.

(3) Mchezaji wa kulipwa wa Ligi Kuu anaweza kusajiliwa tu katika hali ya upekee iwapo maombi ya usajili ya klabu yake yatawasilishwa kwa TFF wakati wa kipindi cha usajili kilichotangazwa na TFF.

## Kanuni : 69 Pasi ya Mchezaji

(1) Klabu inawajibika kuwa na historia ya uchezaji ya mchezaji tangu alipoandikishwa kwa mara ya kwanza kwa kila mchezaji inayemsajili ambayo itaiwasilisha kwa TFF katika kipindi cha maombi ya usajili wa mchezaji. TFF itaitumia au kuitoa historia hiyo yatakapokuwepo mahitaji ya kufanya hivyo kwa mamlaka husika.

(2) Klabu inawajibika kulipa fidia za mafunzo ya malezi ya mchezaji kwa mujibu wa historia ya uchezaji wa mchezaji kwa kufuata kanuni za FIFA.

## Kanuni : 70 Majina na Idadi

(1) Katika Mkataba, fomu, nyaraka na taarifa yoyote kuhusiana na usajili na uhamisho inalazimika kujazwa majina matatu (3) ya mchezaji.

(2) Klabu ya Ligi Kuu inaruhusiwa kusajili kwa kikosi chake cha kwanza wachezaji wasiozidi arobaini (40) na wasiopungua ishirini (20), na kwa timu zake za vijana (u20/u17) wachezaji wasiozidi thelathini (30) na wasiopungua kumi na nane (18) kwa kila timu.

(3) Klabu ambayo itawasilisha maombi yake ya usajili wa wachezaji wake ikiwa na pungufu ya wachezaji ishirini (20) kwa timu yake au itakayopata uthibitisho wa wachezaji pungufu ya wachezaji kumi nane (18) kwa timu zake za vijana itakuwa imepoteza sifa za kuwa klabu ya Ligi Kuu

**Kanuni : 71** **Maombi ya Usajili**

(1) Maombi ya usajili wa mchezaji wa Ligi Kuu yatawasilishwa kwa njia Maalum za Mfumo wa kielektroniki kwa mazingatio ya masharti ya usajili yaliyoainishwa ipasavyo kwa mfumo husika. Klabu inawajibika kufuata taratibu zote hitajika kukamilisha Maombi ya usajili wa Mchezaji wa Ligi Kuu kwa wakati husika. Klabu ya Ligi Kuu itawajibika pia kutimiza Masharti mengine na Maelekezo kuhusu Usajili wa wachezaji wa Ligi Kuu yaliyo nje ya mfumo kama yatakavyohitajika na TFF.

(2) Mchezaji yeyote wa Ligi Kuu anapaswa kuwa mwanachama wa Chama cha Wachezaji wa Mpira wa Miguu Tanzania (SPATA) kabla ya kukamilisha usajili wake kwenye klabu ya Ligi Kuu.

(3) Uwasilishaji wa Maombi ya Usajili wa Mchezaji kwa mifumo yote utahusisha fomu ya orodha ya wachezaji wote (fomu mama), na utazingatia viambatanisho kadhaa ikiwemo:

3.1 Nakala tatu za mkataba wa mchezaji zilizosainiwa na pande zote.
3.2 Cheti cha utimamu wa afya.
3.3 Hati ya uthibitisho kwa Bima kwa mchezaji.
3.4 Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Taifa, au pasi ya kusafiria.
3.5 Picha moja ukubwa wa picha ya pasipoti *(passport size)*.
3.6 Uthibitisho wa uanachama wa SPATA.
3.7 Hati ya uhamisho iliyo kamili *(Release letter)*.
3.8 Uthibitisho wa usajili uliopita (kwa mchezaji anayepandishwa).
3.9 Historia ya mchezaji ya uchezaji wa mpira wa miguu baada ya kutimiza miaka kumi na miwili (12) - *(players' passport)*.
3.10 ITC, kibali cha kuishi na kibali cha kazi kwa wachezaji wa kigeni.
3.11 Kwa wachezaji wa Ligi za Vijana kitaambatanishwa kitambulisho cha Taifa au cheti cha kuzaliwa au pasi ya kusafiria.

(4) Kwa mchezaji anayeendelea na mkataba na klabu yake maombi ya usajili wake yatawasilishwa yakijumuisha fomu ya usajili, cheti cha utimamu wa afya na hati ya uthibitisho wa bima tu. *(klabu inaweza kuambatanisha nyaraka nyingine za awali)*.

(5) Maombi ya usajili wa wachezaji wa timu ya kwanza ni lazima yawasilishwe kwa pamoja na maombi ya usajili kwa wachezaji wa timu ya vijana (U20).

(6) Maombi ya usajili kwa wachezaji wa timu ya vijana lazima yazingatie masharti ya maombi ya usajili wa wachezaji yalivyoainishwa kwenye kanuni 69:2(2.1 – 2.10).

(7) Pamoja na Mazingatio ya Kanuni 69:2(2.1 – 2.10), Maombi ya Usajili kwa mchezaji wa timu za Vijana kwa Klabu za Ligi Kuu lazima yaambatanishwe na Nyaraka zifuatazo za Mchezaji:

7.1 Cheti Halisi cha Kuzaliwa
7.2 Cheti cha Kumaliza Elimu ya Msingi
7.3 Tamko la Mzazi/Mlezi kuthibitisha Umri wa mchezaji

(8) Maombi ya usajili wa wachezaji wa Ligi Kuu yanaweza kufanywa kwa mfumo wa kielektroniki kwa kutumia mtandao katika kompyuta na mwombaji atawajibika kufuata taratibu na mahitaji yote ya mfumo huo kama yatakavyoelekezwa na TFF. Pamoja na uwasilishaji wa Maombi ya Usajili kwa njia hii, TFF inaweza kuhitaji nyaraka zote muhimu zilizotumika na zilizoambatanishwa kwa hatua zake zaidi.

## Kanuni : 72 Pingamizi la Usajili

(1) Klabu yoyote, FA(W), FA(M) na mamlaka nyingine wanaweza kuweka pingamizi kupinga usajili wa mchezaji yeyote kwenye kipindi cha Pingamizi kitachowekwa na kutangazwa na TFF.

(2) Pingamizi ni lazima liwekwe katika kipindi maalum cha Pingamizi na lazima liwe kwa maandishi kwa TFF, mwekaji akiainisha sababu pamoja na kuambatanisha vielelezo husika.

(3) Klabu itapewa taarifa juu ya pingamizi ililowekewa na itatakiwa kujibu au kumaliza dosari zilizosababisha pingamizi kwa wakati kabla Kamati husika haijathibitisha usajili wa wachezaji.

(4) Mchezaji ambaye dosari zake za usajili zilizobainishwa hazitakuwa zimemalizwa na klabu yake katika muda uliowekwa/uliotolewa usajili wake hautathibitishwa.

## Kanuni : 73 Katazo

(1) Haitaruhusiwa kwa mchezaji yeyote kutia saini mikataba ya klabu zaidi ya moja kwa wakati mmoja. Mchezaji atakayesaini mikataba ya klabu mbili (2) tofauti kwa wakati mmoja atafungiwa kucheza mpira wa miguu kwa mashindano yoyote rasmi kwa kipindi cha mwaka mmoja (1).

**(2)** Ni marufuku kwa mchezaji yoyote kutoa Taarifa za Udanganyifu au zisizo sahihi kuhusiana na usajili wake kwa klabu yoyote. Mchezaji atayebainika kutoa taarifa za Udanganyifu kwa lengo la kufanikisha usajili wake au jingine la aina hiyo atakabiliwa na adhabu kwa mujibu wa kanuni hizi na nyingine za kimataifa.

**(3)** Ni marufuku kwa Kiongozi yoyote kutumia taarifa za uongo, udanganyifu au zisizo sahihi kufanikisha usajili wa mchezaji yoyote kwa timu yake au kufanikisha kwa namna yoyote kwa timu nyingine. Adhabu zitatolewa kwa mujibu wa kanuni.

## Kanuni : 74 Uthibitisho wa Usajili

(1) Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF ndio chombo chenye mamlaka ya kushughulikia masuala ya usajili wa wachezaji, kitathibitisha usajili kwa wachezaji wote wa timu za kwanza (wakubwa) na timu za vijana (U20/U17) wa klabu za Ligi Kuu.

(2) TFF itathibitisha usajili wa timu zote tatu (3), timu ya kwanza (wakubwa) na vijana (U20/U17) kwa wakati mmoja, klabu zinatakiwa kukamilisha na kuwasilisha usajili wa timu zake zote tatu (3) kwa pamoja.

(3) Mchezaji yeyote hataruhusiwa kuchezea klabu yoyote katika michezo ya Ligi Kuu mpaka tu usajili wake umethibitishwa na TFF.

(4) TFF itatoa kati ya siku tatu (3) na kumi na nne (14) kupokea pingamizi la usajili wa wachezaji kimaandishi juu ya usajili wa wachezaji tangu kutangazwa majina ya wachezaji wanaoombewa kusajiliwa na klabu husika.

(5) TFF itatoa muda maalum kabla ya kufanya uthibitisho wa usajili wa wachezaji kwa klabu kumaliza dosari za usajili zilizogunduliwa au zinazotokana na pingamizi la usajili na kubainishwa, mchezaji ambaye dosari juu ya usajili wake hazitamalizwa katika muda huo usajili wake hautathibitishwa.

(6) TFF haitotoa manufaa kwa mlalamikaji kwa malalamiko yoyote kuhusu usajili kwa mchezaji ambaye usajili wake umethibitishwa na TFF akiwa hakuwekewa pingamizi la usajili au ambaye Pingamizi dhidi yake lilitatuliwa na Kamati.

(7) Endapo kumefanyika udanganyifu wowote kufanikisha usajili wa mchezaji yeyote wahusika wataadhibiwa kwa mujibu wa kanuni hizi.

(8) Mchezaji ambaye usajili wake utakuwa hauna dosari na umepita (approved) kwenye mfumo wa Usajili Unaotumika kwa TFF kwa ajili ya Ligi Kuu atapewa leseni na kuitumikia moja kwa moja timu yake mpya.

## Kanuni : 75 Kutengua Usajili

Usajili wa mchezaji yeyote wa Ligi Kuu uliothibitishwa unaweza kutenguliwa na TFF endapo itathibitika kuwa usajili huo umekiuka masharti ya kanuni hizi kwa taarifa zilizothibitika ambazo hazikujulikana kabla ya kuthibitishwa usajili wa mchezaji husika, bila ya kujali kuwa aliwekewa pingamizi la usajili au la.

## Kanuni : 76 Mikataba

(1) Klabu ya Ligi Kuu ni lazima iwe na mkataba na mchezaji wake kwa timu ya kwanza (senior) na timu za vijana (U20/U17) ili aweze

kuidhinishwa kucheza katika michezo ya Ligi Kuu na mashindano yoyote mengine rasmi yanayotambuliwa na TFF, mkataba huo utawasilishwa TFF wakati wa maombi ya usajili wa mchezaji husika.

(2) Iwapo wakala anahusika katika makubaliano ya mkataba, naye atatajwa katika mkataba.

(3) Muda wa chini wa mkataba utakuwa kati ya dirisha moja hadi lingine la usajili, wakati muda wa juu wa mkataba utakuwa miaka mitano (5). Mikataba ya muda mwingine wowote zaidi ya miaka mitano itakubaliwa tu kama inakubalika kutokana na sheria za nchi.

(4) Wachezaji chini ya umri wa miaka kumi na minane (18) hawaruhusiwi kuingia mikataba ya mchezaji wa kulipwa kwa kipindi kinachozidi miaka mitatu (3).

(5) Mchezaji wa kulipwa atakuwa huru kama mkataba na klabu yake umekwisha. Mchezaji wa kulipwa mwenye mkataba atakuwa huru kuingia mkataba na klabu nyingine iwapo mkataba wake na klabu yake ya sasa utakwisha ndani ya miezi sita (6). Klabu inayotaka kuingia naye mkataba haina budi kuiarifu klabu yake ya sasa kwa maandishi kabla ya kufanya makubaliano yoyote na mchezaji huyo. Uvunjaji wowote wa sharti hili utastahili vikwazo vinavyofaa.

(6) Uhalali wa mkataba wa mchezaji hautahesabiwa mpaka kuwe na matokeo mazuri ya upimaji afya na kutolewa kwa kibali cha kufanya kazi (kwa wachezaji wa kigeni).

(7) Iwapo mchezaji wa kulipwa ataingia mkataba zaidi ya mmoja unaohusu kipindi kimoja, masharti yaliyowekwa katika sura ya IV ya kanuni za FIFA yatatumika.

(8) Mikataba yote ya wachezaji wa Ligi Kuu lazima isajiliwe na kuthibitishwa na TFF. Mkataba wa mchezaji ambao haujasajiliwa na kuthibitishwa na TFF hautatambuliwa. Mkataba wa Nyongeza *(extension of contract)* Utasajiliwa TFF kwa sharti la Uthibitisho wa pande zote husika za mkataba.

(9) Mchezaji aliye na mkataba wa zaidi ya miezi sita (6) hatoruhusiwa kujisajili na klabu nyingine kabla ya klabu yake mpya kuafikiana na klabu yake ya zamani.

(10) Mchezaji yoyote aliye na mkataba ulio na pungufu ya miezi sita (6) kumalizika anaruhusiwa kufanya mazungumzo ya usajili na klabu kingine kwa sharti la lazima la kujulishwa kwanza klabu yake aliyo na mkataba nayo. Ukiukwaji wa sharti hili utavutia adhabu kwa Klabu au Kiongozi husika.

(11) TFF itakuwa na ridhaa ya kuzingatia marekebisho au nyongeza yoyote katika mikataba ambayo haikuwasilishwa ipasavyo awali.

(12) Usitishwaji wowote wa mkataba upande wowote ni lazima ufanywe kwa maandishi.

(13) Mikataba au mfumo wowote wa utunzaji wachezaji watoto *(walio na umri mpaka miaka kumi na sita)* kwa klabu za Ligi Kuu ni lazima uandikishwe TFF kwa kufuata kanuni za FIFA.

(14) Mkataba wa usajili wa mchezaji na klabu utahesabika kuvunjika au kusitishwa mpaka tu taratibu za msingi za uvunjwaji au usitishaji zimefuatwa na kukamilishwa na chombo husika bila ya kujali upungufu wowote katika utekelezaji wa mkataba huo kwa upande wowote miongoni mwa pande husika za mkataba. Chombo husika kitatatua hitilafu au upungufu wowote wa utekelezaji wa mkataba bila kuathiri/kuingilia nafasi/hali ya sasa ya mkataba husika.

(15) Endapo kutatokea mvutano/kutokuelewana miongoni mwa pande husika za mkataba wa usajili wa mchezaji, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF ndio chombo pekee chenye mamlaka ya utatuzi wa mgogoro wowote wa kimkataba. Ada ya kufungulia maombi itakuwa shilingi elfu hamsini (50,000/-). Upande wowote husika katika shauri unaweza kuomba marejeo (review) ya usikilizwaji wa shauri lao endapo haujaridhika na uamuzi wa awali. Ada ya maombi ya marejeo itakuwa shilingi milioni mbili (2,000,000/-). Hatua ya mwisho ya rufaa ni Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS) ya Lausanne, Uswisi.

(16) SPATA na TAFCA vinaweza kuwawakilisha wanachama wao katika utatuzi wa mgogoro wa kimkataba kwa ridhaa/maombi ya mwanachama husika.

(17) Kila upande unaohusika na mkataba wowote wa usajili na uhamisho wa mchezaji unawajibika kutekeleza bila kukosa wajibu wake kimkataba na kuheshimu masharti yote ya mkataba husika. Kila upande unaohusika na Mkataba utawajibika kuwa na nakala halisi (original) ya mkataba miongoni mwa nakala zilizosajiliwa na TFF.

## Kanuni : 77 Vijana na Watoto

(1) Kila klabu inatakiwa kusajili na kudumisha timu za vijana chini ya miaka ishirini (U20) na miaka kumi na saba (U17) na kuzichezesha katika michezo ya utangulizi ya Ligi Kuu wakati timu ya kwanza ikicheza nyumbani na kushiriki katika mashindano ya vijana yanayoandaliwa na TFF ikiwa ni sharti

la kushiriki Ligi Kuu na kwa manufaa ya klabu na kwa maendeleo ya mchezo wa mpira wa miguu kwa jumla.

(2) Klabu itaruhusiwa kusajili wachezaji wa timu ya vijana (U20) wasiopungua kumi na wanane (18) na wasiozidi thelathini (30) wenye umri usiozidi miaka Ishirini (20).

(3) Klabu za Ligi Kuu zinaweza kusajili mchezaji wa kigeni kwa timu yake ya vijana (U20) atakayehesabika kuwa sehemu ya wachezaji wa kigeni wanaoombewa usajili na klabu husika kwa uzingativu wa masharti ya kanuni ya 62 ya kanuni hizi.

(4) Klabu zinatakiwa ziwe zimekamilisha usajili wa timu za vijana (U20 na u17) katika kipindi cha usajili sambamba na timu ya kwanza ya klabu husika.

(5) Wachezaji mpaka watano (5) tu kutoka orodha ya wachezaji waliosajiliwa wa timu ya vijana (U20) ndio watakaoruhusiwa kuchezea timu ya kwanza ya klabu yao katika mchezo mmoja wa Ligi Kuu.

(6) Usajili na Uhamisho kwa wachezaji wa timu za vijana (U20 na u17) za Ligi Kuu utazingatia kanuni za usajili na uhamisho za kanuni za Ligi Kuu.

(7) Waraka maalum unaweza kutolewa kila mwanzo wa msimu na wakati mwingine kuhusiana na usajili wa wachezaji wa timu za vijana (U20) ambao utasomeka pamoja na kanuni hizi.

(8) Mchezaji wa timu ya vijana (U20) anapopandishwa timu ya kwanza ya klabu yake kwa madhumuni ya kusajiliwa katika kipindi cha usajili atakuwa huru, hatahitaji uhamisho.

(9) Timu za vijana za Ligi Kuu zinaweza kushiriki ligi daraja la chini kuanzia ngazi za mikoa ya klabu zao na zinaweza kupanda daraja mpaka daraja la kwanza (Championship) endapo timu yake ya kwanza bado ipo Ligi Kuu.

(10) Timu za vijana za Ligi Kuu zinazoshiriki ligi ya daraja la chini hazitaruhusiwa kuwa katika daraja moja la ligi na timu yao ya kwanza, endapo itatokea mojawapo kupanda daraja na nyingine kushuka daraja kadiri misimu itakavyokuwa inaendelea. Endapo hali hiyo itatokea timu ya vijana italazimika kushushwa daraja la chini yake.

(11) Mchezaji wa timu ya vijana (U20) anayeshiriki ligi daraja la chini anaweza kuichezea timu ya kwanza ya klabu yake kwenye michezo ya Ligi Kuu na ile ya daraja la chini kadiri atakavyopangiwa na klabu yake.

(12) Mchezaji wa timu ya kwanza ya klabu ya Ligi Kuu hataruhusiwa kwa namna yoyote kucheza kwenye timu ya vijana ya klabu yake inayoshiriki ligi daraja la chini.

(13) Timu ya vijana ya klabu ya Ligi Kuu inayoshiriki ligi ya daraja la chini haitalazimika kucheza mchezo wa utangulizi wa timu yake ya kwanza kwa mujibu wa ratiba ya ligi kuu kwa michezo ya nyumbani endapo kutatokea mgongano wowote wa ratiba, lakini italazimika kucheza Mashindano ya Vijana ya Umri husika.

(14) Timu za Ligi Kuu zinawajibika kuwa na timu za vijana na watoto katika umri tofauti na mipango ya uendelezaji na mafunzo stahili kwa wachezaji wa

timu hizo, usajili na mikataba ya wachezaji hao lazima kutambuliwa na TFF.

(15) Wachezaji saba (7) wa timu ya vijana (U17) wanaruhusiwa kuchezea timu ya vijana (U20) ya klabu yao kwenye mashindano na michezo yoyote inayohusiana na timu za vijana (U20) za Ligi Kuu. Ruhusa hii ni kwa wachezaji wa timu ya vijana (U17) waliosajiliwa TFF na klabu husika katika kipindi cha usajili kwa msimu husika.

(16) Mashindano kwa Timu za Vijana za Ligi Kuu kwa mazingatio ya Vipengele vya Kanuni hizi kuhusiana na timu za Vijana za Klabu za Ligi Kuu Yataendeshwa kwa Matumizi ya Kanuni ndogo kwa Mashindano hayo ambazo zitasomeka pamoja na Kanuni hizi. Masuala yote kuhusiana na Uchezwaji wa Mashindano ya Vijana yataelekezwa katika Kanuni hizo ambapo pia masuala ya jumla yanayohusu Klabu yataamuliwa na kuhusiana moja kwa moja na Kanuni hizi za Ligi Kuu.

# SURA: XV

## DAWATI LA UFUNDI



| SURA : XV | DAWATI LA UFUNDI |
|---|---|
| Kanuni : 78 | Viongozi wa Ufundi |

(1) TFF/TPLB inaweza kufanya uchunguzi na ufuatiliaji kuhakiki utekelezaji na uzingativu wa kikanuni uliokusudiwa kuhusiana na viongozi wa dawati la ufundi kwa mujibu wa kanuni hizi na ikibidi kutoa adhabu za faini na nyinginezo katika kuhakikisha kuwa kila klabu inakuwa na wataalamu wenye sifa zinazohitajika katika kiwango cha Ligi Kuu na wanaotekeleza majukumu yao ipasavyo.

(2) Katika mazingira ya kawaida kila Timu ya Ligi Kuu inawajibika kuwa na wataalamu wa Ufundi (Technical Officials) wasiopungua saba (7) wakijumuisha Kocha Mkuu, Kocha Msaidizi, Kocha wa Magolikipa, Afisa wa Vifaa, Daktari, Mtaalamu wa Viungo na Meneja. Klabu inaweza kuwa na Maafisa zaidi kama Mtathimini mchezo (Perfomance analysts), Mtaalamu wa sayansi ya michezo (Sports scientist), Mchambuzi wa Video (Video analyst) na wengineo kwa Mazingatio ya sifa na mahitaji kwa kila nafasi.

(3) Maafisa wengine wa Ufundi wa Klabu wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kupata adhabu kutokana na makosa wanayofanya uwanjani kama ilivyo kwa Makocha.

| Kanuni : 79 | Makocha |
|---|---|

(1) Kila klabu inapaswa kuajiri Kocha Mkuu na wasaidizi wenye sifa na ujuzi kwa timu ya kwanza (wakubwa) na za vijana (U20 na U17) wanaokubalika kwa mujibu wa taratibu za TFF na mikataba yao kusajiliwa TFF.

(2) Kocha toka nje ya nchi atathibitishwa kwanza na TFF kwa kuzingatiwa pia kupatikana kwa kibali stahili cha kuishi na kufanya kazi nchini kabla ya kuingia mkataba na klabu.

(3) Kocha Mkuu anatakiwa kuwa na angalau Diploma A ya CAF au inayolingana na hiyo iliyotolewa na Mashirikisho ya mabara mengine yanayotambuliwa na FIFA. Kocha Msaidizi anatakiwa kuwa na angalau Diploma B ya CAF au inayolingana na hiyo iliyotolewa na Mashirikisho ya mabara mengine yanayotambuliwa na FIFA.

3.1 Kocha mkuu wa klabu ya Ligi Kuu kutoka nje ya bara la Afrika anatakiwa kuwa na angalau Pro Diploma au inayolingana nayo.

3.2 Kocha msaidizi wa klabu ya Ligi Kuu kutoka nje ya bara la Afrika anatakiwa kuwa na angalau A Diploma au inayolingana nayo.

3.3 Kocha wa timu ya Ligi Kuu kutoka nje ya Tanzania ni lazima awe amefundisha klabu ya Ligi Kuu au

timu ya Taifa katika nchi yoyote ndani ya kipindi cha miaka miwili iliyopita.

(4) Kocha Mkuu ndiye mkuu wa shughuli zote za kiufundi za timu kuanzia usajili wa wachezaji, uandaaji na usimamiaji wa timu katika ligi, kuzungumzia masuala yote ya kiufundi ya timu na mengine yanayohusiana nayo.

(5) Kocha Msaidizi na kocha wa timu ya vijana (U20 na U17) wa klabu ya Ligi Kuu awe na Leseni ya chini kuanzia B Diploma ya CAF au inayolingana nayo iliyotolewa na Mashirikisho ya Mabara mengine yanayotambuliwana FIFA. Kocha msaidizi wa timu ya vijana (U20 na U17) kutoka nje ya bara la Afrika anatakiwa kuwa na angalau A Diploma au inayolingana nayo.

(6) Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kuwa na kocha wa walinda mlango, kocha wa viungo (Fitness Coach) wenye ujuzi, klabu itakayokosa kocha wa walinda mlango itakabiliwa na adhabu kwa mujibu wa kanuni hizi.

(7) Makocha wote Shiriki kwenye Ligi Kuu ni lazima wakidhi mahitaji ya Leseni ya Kocha inayotolewa na TFF na kupatiwa Leseni husika baada ya kutimiza pia Masharti maalum kutoka TAFCA na kupata Uthibitisho wa TAFCA.

## Kanuni : 80 Daktari wa Timu

(1) Kila klabu ya Ligi Kuu inawajibika kuwa na daktari wa timu mwenye ujuzi na sifa za kutosha kama daktari kamili pamoja na mtaalamu wa tiba ya viungo watakaotambuliwa na kuthibitishwa na TFF walio na vifaa tiba kamili na stahiki.

(2) Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayoanza msimu mpya na kucheza mchezo wa Ligi bila kuwa na daktari mwenye ujuzi kwa kanuni ya 78:1 au/na mtaalam wa tiba ya viungo itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na daktari anayehitajika, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja.

2.1 Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayopoteza daktari mwenye ujuzi kwa kanuni ya 78:1 au/na mtaalam wa tiba ya viungo baada ya kuanza msimu itaruhusiwa kutumia daktari wa muda mwenye sifa za kuwa daktari msaidizi kwa mujibu wa kanuni au/na mtaalam wa tiba ya viungo msaidizi, kwa michezo isiyozidi sita (6) ya Ligi Kuu.

2.2 Kama itakuwa haijapata daktari mkuu mwenye ujuzi au/na mtaalam wa tiba ya viungo hadi baada ya michezo hiyo sita (6), itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na daktari anayehitajika kikanuni au/na mtaalam wa tiba ya viungo, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja.

(3) Daktari wa timu anawajibika kuhakiki afya za wachezaji na viongozi wa timu kabla ya maombi ya usajili wa wachezaji kuwasilishwa.

(4) Madaktari wote Shiriki kwenye Ligi Kuu ni lazima wakidhi mahitaji ya Leseni ya Daktari inayotolewa na TFF na kupatiwa Leseni husika baada ya kutimiza pia Masharti maalum kutoka TASMA na kupata Uthibitisho wa TASMA.

# SURA: XVI

## MAMLAKA

| SURA : XVI | MAMLAKA |
|---|---|

## Kanuni : 81 Maamuzi Yasiyokatiwa Rufaa

Maamuzi yote kwa mujibu wa vipengele vya kanuni za Ligi Kuu katika kanuni ya 81 hayatakatiwa rufaa katika ngazi yoyote, mhusika yeyote kuhusiana na maamuzi yaliyotolewa chini ya vipengele hivi anawajibika kutekeleza linalomhusu mara moja.

| | Kanuni | | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | 14 | Leseni ya Klabu | Yote |
| 2 | 17 | Taratibu za Mchezo | Yote |
| 3 | 42 | Udhibiti kwa Wachezaji | Isipokuwa 41:(6,14,16,19,21) |
| 4 | 43 | Udhibiti kwa Waamuzi | Isipokuwa 42:(3) |
| 5 | 44 | Udhibiti kwa Kamishna | Isipokuwa 43:(3) |
| 6 | 45 | Udhibiti kwa Mtathmini Waamuzi | Isipokuwa 44:(3,4) |
| 7 | 46 | Udhibiti kwa Makocha | Isipokuwa 45:2(2.13) |
| 8 | 47 | Udhibiti kwa Viongozi | Isipokuwa 46:(2,8,9,10,11,12,13,14,15,16,17,18,19,20) |
| 9 | 48 | Udhibiti kwa Klabu | Isipokuwa 47:(5,6,15,16,18) |

## Kanuni : 82 Ufafanuzi

Kwa minajili ya kufafanua kanuni hizi TFF itakuwa inatoa WARAKA maalum kila inapoonekana inafaa kufanya hivyo kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wake.

## Kanuni : 83 Marekebisho ya Kanuni

Kamati ya Utendaji ya TFF inaweza kurekebisha kanuni hizi kila inapotokea haja na sababu za msingi za kufanya hivyo, aidha TFF itatoa WARAKA maalum utakaosomeka pamoja na Kanuni hizi kwa marekebisho yoyote yaliyofanyika ambayo hayajaingizwa katika kitabu cha kanuni hizi.

## Kanuni : 84 Kufuta Kanuni

Kanuni hizi zinaweza kufutwa na Kamati ya Utendaji ya TFF pekee.

## Kanuni : 85 Yasiyomo

Mambo yote yasiyokuwemo kwenye Kanuni hizi yataamuliwa na Kamati husika au ya Utendaji ya TFF kwa kuzingatia Kanuni na Katiba ya TFF au Kanuni za FIFA na CAF.

## AZIMIO

Kanuni hizi zimepitishwa kwa Azimio la Kamati ya Utendaji ya TFF iliyokutana Dar es Salaam Agosti 5, 2026.

**Wallace Karia**
Rais

**Oscar Mirambo**
Kaimu Katibu Mkuu